Sasa kuna hiyo mila ya kusema kuwa watu wasiingiliwe mambo ya kutairisha wanawake, sheria hii haijasema wazi wazi kuwa FGM ama kutairishwa wanawake imepigwa marufuku. Kwa sababu, chini ya bill of rights imesema mko na haki ya kuendesha mila yenu, isipokuwa ile mila ambayo iko na madhara kwa hivyo, akija mtu kusema kuwa tunazuia nyinyi kufanya hivi anatakiwa kuonyesha kuwa kuna madhara gani ndani yake. Lakini mila ya watu imeheshimiwa chini ya Katiba. Kwa mfano ikiwa mnaifanya kwa sababu ya mila yenu au dini, hakuna mtu ambaye anaweza kuwaingilia. Kwa sababu, itakuwa ni uhuru wa mila yenu na uhuru wa dini yenu. Kwa hivyo usiwe na wasi wasi kuwa mtainigiliwa katika mila. Mambo ya mila haitaingiliwa kabisa na sheria hii mpya. Nafikiri mngesuburi tuangalie chini ya bill of rights, tunaambiwa nini, haki za kimsingi za watu wote.

Translator: *Muxu yiri carinti xorta kuxisabsaneth guthninta, muxuyiri rer Kenya wala ugsonyaxai rer kasta mise bel kasta daqan ketha ee lethaxai marka shercigan usub ee lakorey muxu cakon sanyaxai iney rer kasta mise qola kasta ee kudacmeyso on laga fara gelineynin destur kothi iyo dintothi, marka xathi sa ee exen buyiri desturkas mise dintas lagu dacmeyo mith divata keynaya, marka kof ala kof kuyiratha uyiri xerka aath kudacaneyso wa dambi xathu kuyiratho buyiri maxath lethaxai cii cathey mexey divata uu keney, marka machirto wala ugsonyaxai oo lacokon sanyaxai nin kasta xerkisi iyo dintisi ayu kudacmeya.*

Xatheysa divato dhathka uu keneynin, wax marakta ee kaxor imani kara oo kudixi kara marakthey waxath sameyneso wa dhambi machirto buyiri xathu kofka kuyirathona xaku catheyo mexey divata kente xathi guth matha man daxno buyiri, xathi uu kofka kuyiraxo uyiri dhambi bath sameynesa, divata ee kentey ma maxai bath weithineysa buyiri. Marka xathi uu guthmatha ee divata keyneso marka dhambi bei nokon buyiri, maxa yelei divata bei keynesa kof ba va lacarka uu dinto marka sas aa chirta chawabtathi xaga kuth matha wa sas. Xathi ee divata keinso guthmatha iyatha dhambi bei nokoneysa, maxa yelei kofka binaadamka waxa divata uu keneya dinta na kuma ficna maxa yelei dintain waxa cathiga divata kuu keneya kuma camreyso, desturkeina na kuma camrayo waxa athig adivato kuu geinayo,

maxa yelei in maraktei aath sifican loo dacmo aya lathoneya.

Com. Lethome: There was a question from a lady?

Translator: *Ya sucal weithineya?* A minute she is saying on the one of those who contributed.

Com. Lethome: That what are we going to give them?

Translator: The idea is included here

Com. Lethome: There here that is the contribution, that is the ..

Translator: *Certificatka lagusiyey maxa waye, rai gaga intu kuchira marakthey, wixi malinti aath divatey xal bu guchira, ulachethatha na tas ee xeth.*

Com. Lethome: Halafu this is a historical process, tell them we are making history and if he contributed infact in history you will be telling your children na wajukuu wako kuwa, hii sheria mimi nili-contribute, nilitoa maoni yangu ndani yake. It is not possible for us to reward physically or materially all the millions of Kenyans ambaao wame-contribute ndani yake, haitawezekana it is not possible.

Translator: *Muxu kuyiri xorta maxath oogata shercigan aath malinti kageb katha tey xorta wa keb dhaxab buu kageley xaga tariktha Kenya. Martka xathu Illahi iyaratho athigi cilmixi aath dashey iyo kuwa aath awowga utaxai, waath kufani karta wath dixi malinti sherciga Kenya lathechinaye aniga rai geiga an kadibtey oo wan kaceikatey, marka mana dici karto buyiri intaso kun oo Kenyan aa ya raigotha dibtey, kulikoth certificateyal lamasini karo mise marakthey lamadixi karno xevel ba kacebkatey an certificate sino, maxa yel wa intaso kof oo Kenyan aya ka cebkathatey, marka athiga maxa sharaf iyo wanag kuxe shercigi aath kaceb kathatey oo beri lagu dacmo ayan kufani karta ooth dixi karta malinti lakoreye sherciga Kenya aniga intan geth dadab xospital ketha an farisaney ayan rai geiga uu dibtey oo wax ala wixi aath divatey uu sherciga manta lagu dacmeyo uu yaxai tas ya athi sharaf kuce uu kuyiri.*

Maryan Hassan: *Bismillahi Rahmani Rahim, waa anigo Maryan Hassan oo kunol wadhanka Kenya magalatha Dadaab North Easter, waxan leyaxai xathalka wa sucal iyo majib, manta xathalkan naloshegayo wa xathal aan kufarax san naxai xathal aan dhoth kawathno ama sucalo an kawathno maxa, wa xathal aan checel naxai on mutha bathan na kudawakeyne on lexen divatathas na xeitasa, divata iyatha exeth na xathi nalala xos tagan yaxai, oo laleyaxai manta wan ithin katheyneyna xorta farxath wein aath ban uu kabna.*

Nin ba se cher uxu yiri yan laga wayin beri salathi afar kuvaxath le, magalatha natha Kenya, wadhanka natha Kenya, wixi an kawaine xoran xathi xatha an kaxeleyno caath ban uu checel na xai, divatoyinka aath shegten in xor noga dawakaney oo dhathka helicoptoinka lagurusheinayo magalatha Garissa guvai, Garissa guvai ban uu bixiney

divatatha kabsatey, abayasha natha macal walalatha natha woviyatha lagu gurey iyago nol nol oo lugaxa kacharan ur kutalathi wei nagu tala, tii iyatha exeth xathi inti laga tovath keney dhowlatha Kenya dib axan ee noguso nocotey ano xatha wax sucal oxo an kacaba machirto ee waxan cathkeyneya on kucala caleya iney divatathi iyatha exeth nagala thayo oo ukolonithi nagala katho oo marakthey divatoyinki dib nogola xasusto sithi aath noo shegten wan ku farax san naxai oo madhax banan naga gido uu cilmaxa naga cafartan iyo shan bei garan kipande lacan wa sitha lashegey isticmarki uu chira ila aminkan ina nalaga thayo oo xormar nalagarsiyo ayan kufarax san naxai intasan leyaxai. Wa-asallam aleikum.

Translator: She is saying that she is grateful that you have said that the past injustices will be corrected according to our new Constitution that people will not suffer. This is what we were aspiring for. We are actually grateful for what you have brought us and we are thankful for those who have carried out this job, another mother.

Com. Lethome: She has no question. Sasa tutaangilia kitu ingine ambayo inaitwa bill of rights, hii ndio ambayo imechukua sehemu kubwa sana, hii ndio sura kubwa sana katika hii Katiba. Haki za binadamu. Sheria yeyote hata ikiwa mzuri namna gani na haiangalii haki ya binadamu, hiyo sheria haifai kabisa. Kwa hivyo kuna haki ambazo haupatiwi na serikali, Raisi, kiongozo hata mama yako hakupatii hiyo haki, umepatiwa na nani? Na Mwenyezi Mungu (S.W.T.). Kwa mfano, haki ya kuishi, haki ya maisha, kuna mtu yeyote ambaye amekupatia? Kuna mahali uliandika application, mimi ninataka kuishi nipatie maisha uhai? Hakuna mahali yeyote.

Haki ya kupata riziki yako ya kukula, hiyo ni haki ya Mwenyezi Mungu peke yake, haki ya wewe kuwa binadamu, hakuna mahali umetuma application ndio wewe ukuwe binadamu. Mwenyezi Mungu ndio amekupatia hiyo haki ya kuwa binaadmu kuna mtu yeyote ambaye anawezakuchukua hiyo haki kutoka kwako? Hiyo haki haiwezi kuchukuliwa, hata ukiwa umeshikwa umefungiwa jela, haki yako ya ubinadamu iko. Uko cell kwa prison, haki yako iko. Uko ndani ya gari unatembea, haki ya binadamu iko, umelala haki yako ya binadamu iko, wewe ni mtoto haki yako ya binadamu iko, wewe ni kiwete kama ule mzee alikuwa hapa na ile gurudumu yake, ni binadamu ama si binadamu? Hizo ndio tunasema haki za msingi haki ambayo hakuna binadamu yeyote anaweza kuchukua, hakuna serikali inaweza kuchukua. Na zote zimewekwa hapa chini ya Katiba, chini ya sehemu ambayo tunaita bill of rights. Hii ni sehemu ya haki ya kimsingi, tumesema sheria hii mpya ya Kenya itahakikisha kuwa kila mmoja ana haki zake za kimsingi. Ikiwa mtu hatapata haki zake za kimsingi, basi serikali iko na jukumu ya kuhakikisha kuwa umepata hizo haki zake. Unaweza kuenda kushtaki serikali kusema nimenyimwa haki zangu za kimsingi. Kwa mfano, kwa nini watu wengine watembe kilometer arobaini kupata maji, biyo peke yake. Jana tumekutana na mama mmoja njiani na mtoto mdogo na jerican ya maji, anasimamisha kila gari inapita, biyo, anaomba maji, ni jukumu ya nani kumpatia huyo mama maji? Serikali ina haki ya kumpatia. Kuna binadamu anaweza kuishi bila maji? kuna binadamu anaweza kuishi bila chakula? Kuna binadamu anaweza kuishi bila kukaa kwa nyumba?

Ni juu ya serikali kuhakikisha kuwa kila mmoja amepata hizo haki, kwa hivyo tunasema kuwa sheria hii ama msingi wa nchi ya

Kenya ni haki za binadamu. Ni wajibu kwa serikali kuhakikisha kuwa haki zimepatikana na uhuru wa kila mmoja umepatikana.

Hebu tuziangalie hizo haki ni gani? Haki ya kwanza ni haki ya kuishi, kila mmoja ako na haki ya kuishi, hauwezi kuuliwa bila ya haki yoyote na mtu yeyote ambaye uhai wake utachukuliwa bila ya haki yeyote, sheria lazima ifanye kazi. Na ndio wamesema sasa chini ya sheria ya Kenya, tunajua mtu akiua akipelekwa kuhukumiwa hukumu yake ni nini? Ananyongwa ama sivyo? Sasa wamesema mapendekezo ni kuwa ile hukumu ya kunyonga iondolewe kwa sababu uhai Mwenyezi Mungu ndio anapeana na yeye pekee yake ndio anaweza kutoa uhai.

Kwa hivyo, wanasema chini ya sheria mpya hakuna kuhukumiwa kuuliwa ama kunyongwa. Haki nyingine ni usawa, hakuna binadamu ambaye ni bora kuliko mwingine, ndio kuna wengine ni matajiri, wengine maskini, wengine ni wakubwa, wengine ni wadogo, lakini wote ni binadamu. Kwa hivyo, tunasema kuwe na usawa mbele ya sheria baina ya mkubwa na mdogo, hiyo ni haki ya msingi kwa hivyo ukipelekwa kotini na mtu tajiri sheria isipendeleo upande moja kwa sababu huyu ni tajiri au huyu ni kabila fulani na huyu ni kabila nyingine mbele ya sheria sisi sote tuko sawa.

Halafu kuna kitu kingine ambayo tumeumia sana kwa sababu yake, discrimination ubaguzi, utasikia ukitembea Nairobi ukienda Eastleigh jioni, utakuta polisi ni wengi sana, wanazunguka huko ni kwa nini? Wanaenda kutafuta woria, kwani woria si Mkenya?

Woria ni Mkenya ama si Mkenya?

Audience: Ni Mkenya.

Com. Lethome: Ni Mkenya lakini kwa nini ubaguzi kama huo? Ukitembea na mimi Nairobi, tukisimamishwa na polisi mimi nitaenda na wewe utabaki ukiulizwa maswali kwa nini? Kwa sababu wewe ni woria mimi si woria, hiyo discrimination inasemekana hakuna au tunasema huyu ni mwanamke kwa hivyo hana haki, huyu ni mwanaume ako na haki au huyu ni kiwete hana haki huyu mwingine ako na haki, hiyo tunaita discrimination. Sheria mpya inasema hakuna mambo ya discrimination kwa sababu ya dini au kwa sababu ya kabila yako au rangi yako au ni tajari au maskini, ni haki yako kama binadamu ufanyiwe usawa uwe na usawa kwa watu wote.

Haki za wanawake, tunajua wanawake wamedhulumiwa na tunaposema wamedhulumiwa sio sheria ya Kiislamu imedhulumu mwanamke. Sheria ya Kiislamu haijamdhulumu mwanamke imempatia haki zake zote. Tumekwenda Kisumu, sikilizeni vile Wajaluo wanasema. Wanasema katika sheria mpya hatutaki mtoto wa kike awe na haki ya kuridhi ardhi, hana haki ya kuridhi, tukamuuliza aende wapi? Anasema ataenda kwa bwana yake, haki yake iko kwa bwana yake, na asipoolewa? Wakasema pelekeni kwa mbunga ya kuifadhi wanyama akakae na wanyama huku ikiwa serikali imetenga mbung aya kuhifadhi wanyama basi na wasichana wapelekwe huko wakakae huko na wanyama.

Wengine wanasema, mtoto ni mtoto wa kiume peke yake, sheria ya Kiislamu inasema mtoto ni mtoto wa kiume peke yake?

Audience: Hapana.

Com. Lethome: Hakuna hiyo ni jahiliya, mambo ya jahiliya, kwa hivyo tunasema kila mmoja ana haki, mwanamke ana haki na mwanaume ana haki. Mambo ya elimu, kuna watu wengine wanasema mimi ninapeleka mtoto mwanaume peke yake shule, sheria ya Kiislamu inasema hivo? Lazima wote wawili sawa, na hata Sunna ya Mtume (S.A.W.) inasema, mtu ambaye atakuwa na wasichana wawili ama zaidi, awaangalie malezi mazuri, basi unaambiwa thawabu yake ni Janna, sivyo amesema Mtume (S.A.W.), kwa hivyo tunaposema dhulma kwa mwanamke sio sheria ya Kiislamu imedhulumu, sheria ya kijahiliya ndio imedhulumu na sheria ya kizungu ndio imedhulu, kwa hivyo tunasema kuwe na usawa baina ya wanawake na wanaume.

Watu wazee, kuna watu wengine wanasema aah huyu ni mzee sasa amekuwa mzee huyu asiangaliwe haki yake laa. Watu wazee lazima waangaliwe haki yao na chini ya sheria wamesema mtu ambaye amefikisha miaka sitini na zaidi lazima apewe haki zake. Na watu wengine wanafikiria haki ya mzee ni wa jengewe mahali kama boma. Wazee wote wanakusanywa wanatupwa huko kwenye hiyo boma, hapana, kwanza sheria yetu ya Kiislamu inasema lazima uangalie wale wazee nyumbani, wako na haki zao. wamekulia mpaka umekuwa mtu mzima nao lazima waangaliwe, kwa hivyo, wako na haki chini ya sheria mpya, waangaliwe wazee.

Haki za watoto, kila mtoto ana haki katika nchi hii lazima asikizwe. Kila mtoto ana haki ya kupata elimu ya msingi ambao itakuwa ni bure, kwa kila mtoto. Kwa hivyo, hakuna kubaguliwa kwa sababu huyu ni mtoto. Mtoto pia ana haki lakini haina maana kuwa wasifanyiwe adhabu lazima wafanyiwe adhabu waweze kulewa malezi mazuri. Lakini mtoto pia ako na haki za binadamu.

Kuna haki za family na lazima haki kama hizo ziheshimiwa. Kwa mfano, kuja kuingiliwa mambo yenu ya family hakuna kitu kama hiyo. Family lazima iwe ni yenye kuheshimiwa. Watu ambao ni viwete, persons with disability. Katika community nyingi na ninajua wasomali pia wana hiyo, mnawaita majina mabaya ama sivyo. Mimi nimeishi na wasomali unasikia wanaitwa Omar farur. Omar farur kwa sababu pengine ako na hiyo. Wengine wanaitwa turle, ama wengine wanaita jina mbaya, ni makosa kuita hivyo. Kama ana macho moja anatukanwa, au kama ni kiwete watoto wanatukana wanamchezea. Chini ya sheria mpya, kila mmoja ako na haki kwa sababu huyo mtu ni binadamu. Ni binadamu ama si binadamu? Ako na haki za msingi za kibinadamu, wale vipofu wale ambao hawezi kuzungumza wapewe haki zao, wapelekwe shule wakasome, kuna watu kama sisi, Vice Chairman wetu mmoja, first Vice Chairman, Dr. Oki Ooko Ombaka ambaye amefariki hivi sasa alikuwa haoni ni kipofu, amesoma, ni mtu ambaye amehifadhi sheria amekuwa ni mtu doctor katika mambo ya sheria, amekuwa first Vice Chair, ile kukosa macho haina maana kuwa yeye sio binadamu na hana akili, tumeona watu hata viwete anatambaa hivi, unamkuta ni director au ni manager, lazima apewe nafasi ya kufanya kazi na kupata elimu ya kutosha ili aishi kama binadamu wengine. Ndio maana tunasema ile majina ya kuwaita kiwete hapana, ama kipofu au bubu, hiyo majina iondolewe yote kwa sababu inawarudisha hadhi yao chini. Wana haki ya kuenda kushtaki kuwa wanabaguliwa. Kwenye mkutano kwa mfano, isiwe mkutano watu wanazungumza tu kwa lugha ambao pengine mtu bubu hafamu, inatakiwa kwenye mkutano kama hii tuwe na mtu ambaye ana-interpret sign language.

Makaratasi kama hii iwe imeandikwa kwa Braille mtu kipofu anaweza kusoma. Tuweke mkutano mahali ambapo hata mtu kiwete anaweza kufika. Nyumba zikijengwa za serikali inajengwa wakijua kuwa kuna mtu ambaye pengine hawezi kutembea kwa miguu, hawezi kupanda ngazi kufika mpaka huko juu. Choo cha public zikitengenezwa ijulikane kuna watu wengine wataingia kwenye hiyo choo wakitembea kwa mikono yao. Kwa hivyo, hii mambo yote lazima iangaliwe tuwe sisi wote ni sawa, kama ni telephone booth, ijulikane kuna watu wengine hawawezi kufika hapo juu kwa sababu ni viwete kwa hivyo kusiwe na discrimination yeyote kwa sababu mtu hana uwezo.

Katika bunge, tuwe na watu ambao wanawakilisha persons with disability, watu ambao ni vilema. Lazima tuwe na watu ambao wanawakilisha katika bunge. Mambo yao isiwekwe kando kuwa yule ni kiwete, ni kiwete ndio lakini ni mwanadamu na ni Mkenya na ako na haki sawa. Heshima ya binadamu, lazima kuwe na heshima, binadamu aheshimiwe kila mahali, mpaka maiti ya binadamu lazima iheshimiwe.

Kisha uhuru, hakuna ruhusa mtu kunizuia uhuru wangu kama sijafanya makosa. Hakuna ruhusa mtu kunizuia kuenda mahali fulani. Mimi nikitaka kwenda Garissa, hakuna ruhusa mtu yeyote kuniuliza unaenda kufanya nini huko niko Kenya, niko na uhuru, sijafanya hatia yeyote, ni haki yangu ya kibidadamu. Nina uhuru ya kwenda mahali popote.

Haki ya kulindwa, hasa watu wa North Eastern Province, ndio tunasikia kuna insecurity ya hali ya juu sana, ni juu ya serikali kuhakikisha ya kuwa mimi kama Mkenya, wewe kama Mkenya, na mali yako umepewa security ya kutosha. Mali yako ikija ikiliwa na simba, serikali waje wakulipe. Mtoto wako akija akiuliwa na bandits ni juu ya serikali kuhakikisha kuwa umelindwa na kukitokea matatizo imekulipa. Hiyo ni jukumu na ndio sababu umeweka serikali hapo kwa hivyo tunasema freedom and security of the person. Lazima kuwe na uhuru na pia kuwe na usalama wa kila mwanadamu.

Hakuna mambo ya utumwa, unajua maana ya utumwa ni nini? Utumwa maana yake mnajua ni nini? Mnaitaje kwa Kisomali utumwa?

Audience: *Cadhon.*

Com. Lethome: Sasa cadhon maana yake ni mtu anakuchukua anakulazimisha kwa sababu wewe ni maskini utafanya kazi hakupatii mshahara, hakupatii mahali mzuri ya kulala, umekuwa wewe ni mtumwa wake ni haramu chini ya sheria kufanya mtu yeyote *cadhon*, hakuna *cadhon*. Kama ni dereva yako umemuandika kazi ni mfanyikazi, kama ni mtu umeandika kazi ya kufua nguo nyumbani kwako umemuandika kazi, yeye si *cadhon* yako hakuna *cadhon* katika sheria. Hata sheria ya Kiislamu imekataa mambo ya *cadhon* ama sivyo?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Hakuna pia kulazimishwa unaambiwa wewe woria Mohammad shamba ya waziri pale lazima ukafanye kaze,

usipo fanya kazi utafungwa, unalazimishwa kufanya kazi. Kazi ufanye kwa hiara yako kwa mapenzi yako. Kwa hivyo, tumesema pia mambo ya kazi kulazimishwa hakuna, kitu kama hiyo mnasikizana na mtu. “Waria mimi niko na lorry yangu hapa utafanya kazi ndani yake ama haufanyi? Mnasikizana nikitaka nitafanya kama sitaki ninakwenda. Hii hoteli yangu utafanya kazi ya kushafisha vyombo, mshahara kiasi fulani unakubali? Nimekataa niko uhuru wa kuenda, hauwezi kuniambia utaona waria umekataa kufanya kazi kwangu utaona, hakuna kitu kama hiyo hakuna kulazimishana.

Privacy, tunasema kuna ile kuingiliwa undani wako, kwa mfano ndani ya nyumba yako. Sheikh unakubali mtu hata kama ni polisi aiingie kwa boma yako vile anata?

Shiekh: Wanaingia bila kutaka.

Com. Lethome: Ee wanaingia ndio tunasema hakuna ruhusa kuingia sasa, kwa mfano..

Shiekh: Wanaingia hata wa leo wanaingia kwa ma nyumba watu.

Com. Lethome: Sasa ndio tunasema hakuna lazima iheshimiwe ama kwa mfano unapita pale kwenye barrier, waria kuja hapa mzee, anaanza kukushika shika wewe kila mahali, hiyo ni kuingilia privacy yako. Lazima aheshimu au polisi mwanaume anashika shika mwanamke Muislamu, ana haki kufanya kitu kama hiyu? Kama anataka ku-search, kama wanafikiria pengine amebeba bomb ama bunduki ama nini, watafute polisi mwanamke aende akamuangalie na afanye adabu pia, afanye adabu yake. Kwa mfano, umeshikwa na polisi kwa vile wewe umeshikwa sasa uko chini ya polisi unasema mimi ninataka kwenda choo, unaambiwa hapa hapa kwenye cell iko ndoo hapo, hapo hapo mbele ya watu wengine.

Hiyo ni kuingilia heshima yako, privacy yako. Kwa hivyo privacy yako lazima iheshimiwe, au simu yako inasikizwa kwa sababu wanafikiria wewe ni fundamentalist au wewe ni Muislamu mwenye siasa kali, simu yako inakuwa tapped, ukizungumza hata pengine unazungumza na bibi yako mambo ya siri, au unazungumza na mtoto yako mambo ya nyumbani, hiyo simu inakuwa tapped inasikizwa na mtu mwingine. Barua yako Posta inafunguliwa wanaangalia siri baina ya mume na mke kwa sababu ile maneno mimi ninazungumza na bibi yangu, ninaweza kutaka mtu mwingine asikie?

Audience: Hapana.

Com. Lethome: Hapana hiyo ni haki yangu na lazima serikali ihifadhi hiyo haki yangu. Kwa hivyo mahali nyumbani au unapozungumza maneno yako ya siri, hakuna haki wewe kusikizwa na mtu mwingine. Chief akuje aseme ulikuwa unasema nini wewe na bibi yako, nimesikia jana usiku mkipigiana kelele. Ako na haki kama hiyo?

Audience: Hapana.

Com. Lethome: Hakuna haki kama hiyo lazima aheshimu kitu kama hiyo. Uhuru wa dini, hiyo ni haki yangu ya msingi. Hakuna ruhusa mtu yeyote kuja kuniambia kwa nini umelea ndevu, wewe ni muislamu, kwa nini .. nyoa hiyo ni chafu, wanaita chafu, ukiwa katika polisi kuna polisi yeyote hapa? Kama kunayo utakuta amenyoa kabisa.

Muhammed: Askari yote anaambiwa anyoe.

Com. Lethome: Anaambiwa ni chafu, hiyo unaingilia dini ya mtu. Nataka mimi nikivaa kanzu yangu ama kikoi nisiingiliwe na mtu yeyote, ni uhuru wa dini yangu. Ninataka kwenda kuabudu time ya swala imefika, nipewe hiyo uhuru ya kwenda kuabudu, siku ya ijumaa nipatiwe ruhusa mapema kutoka kazini niende nikaabudu. Nikienda huko nisikatwe mshahara kwa sababu nimeenda kusali, mwezi wa ramadhani nimefunga lazima niheshimiwe kwa sababu ni mwezi wangu mtukufu.

Mwanamke Muislamu amevaa hijab kwa sababu ya dini yake. Lazima iheshimiwe hiyo ni uhuru ya dini yake. Hawezi kusema kwa vile wewe sasa ni mwanamke Muislamu umeandikwa kazi ya polisi lazima uvae hiyo shorts, nimeona huko Garissa wanawake wawili Waislamu, apewe uniform ambayo inakubaliana na dini yake, uniform ya watoto wa shule iwe kulingana na dini, kwa hivyo dini pia iheshimiwe.

Freedom of expression, kueleza vile unavyotaka, kwa mfano Rais ni mbaya, una haki ya kusimama na kusema Rais ni mbaya, sio kuanza kupiga makofi, amesema kitu mbaya na unapiga makofi. Inatakiwa usimame useme mtukufu Rais, ile umesema ni makosa, DO umefanya makosa, serikali ni mbaya, serikali ni mzuri, unaandika kwenye gazetti ukitaka, unaandika barua kwa mtu yeyote ukitaka bora tu usivunje sheria. Ni haki yako ya kimsingi kujieleza vile unavyotaka. Am I going very slowly?

Translator: And I want to leave you because the last bus is about to leave.

Com. Lethome: Ngoja kidogo tuendeleo, kisha kuna mambo ya information kupata information. Kwa mfano baada ya kutokea fujo Likoni, kumefanywa Commission ya kuchunguza na kuandika report, kuna kasisi mmoja wa katoliki ameuliwa, imesemekana hiyo mambo itachunguzwa, watu walipouawa Wagala, ilisemekana hiyo mambo itachunguzwa, iko watu wanachunguza hiyo mambo.

Kukitoka vujio yeyote mtu ameuliwa itachunguzwa hiyo mambo, matokeo yake tunajua mpaka sasa tunajua, nafikiri hakuna Commission ingine ambao report yake imepatikana isipokiwa hii yetu. Commission baada ya ingine inafanywa lakini ile information unaambiwa hiyo ni siri ya serikali, kwanzia sasa tumesema chini ya sheria mpya, kila Mkenya ako na haki ya kujua hiyo uchunguzi imefikia wapi reporti yake imesema nini.

Serikali imesema kitu gani ni haki ya kila Mkenya kupata hiyo information. Kwa hivyo, serikali isiseme mambo ingine hii hatuwezi kuwajulisha na hii tutawajulisha lazima watujulishe.

Freedom of association umetaka kwa mfano leo uko KANU kesho unasema mimi sitaki kuwa KANU nataka kuwa DP ama SAFINA, ama FORD Kenya. Uko na hiyo uhuru ya kujiunga na kikundi hiyo yote ambayo unataka. Mimi ninataka kujiunga na kikundi ya Waislamu, una hiyo uhuru, kikundi ingine ya wakina mama niko na uhuru, kikundi ya youth niko na uhuru. Freedom of association, uko na haki ya kujiunga na mahali popote, zamani pia unaambiwa mkikaa kwenye mkutano kama hii hivi, lazima upate barua ya nani? Barua ya Chief, hiyo ni kuingilia haki yetu ya kukusanyana na kuzungumza vile tunataka bora

tusivunje sheria.

Na pia ndio kuna hiyo haki ya assembly yaani kukusanyana pamoja au wafanyi kazi, kuna walimu hapa ama hakuna?

Audience: Wako.

Com. Lethome: Mwalimu mmoja yuko hapa hivi mimi ninajua wamegoma sasa kwa sababu ya haki yao. Isijie waziri anasema hiyo mgomo ni haramu, si ndio amesema sasa waziri?

Audience: Mmh.

Com. Lethome: Tunasema chini ya sheria mpya wako na haki ya kufanya demonstration, wamenyimwa haki yao. Ni haki ya kibinadamu unapodhulumiwa, ufanye demonstration na kupiga kelele ili upatiwe haki yako chini ya sheria mpya lakini usi vunje vunje vitu mwalimu, usi umize mtu lakini mna haki ya kujieleza. Freedom of demonstration and petition na kusema serikali wametudhulumu, hiyo ni haki yenu.

Political rights, kila mmoja ako na haki ya kisiasa. Kila Mkenya ako na haki yake ya kisiasa. Freedom of movement and residence, kama Mkenya uko na haki ya kuenda mahali popote unapotaka kuenda. Ukitaka kuenda Baringo kuishi huko una haki, ukitaka kuenda Nairobi ukaishi huko uko na haki, na pia uko na haki ya kuishi mahali popote katika hii nchi. Freedom of residence, uishi mahali popote ambapo unataka.

Kisha tuna haki pia ya wakimbizi, kwa sasa Kenya haina sheria ambayo inasimamia wakimbizi, refugees, hatuna sheria. Sheria ambayo tunatumia ni ile international law, kwa hivyo tunasema Kenya lazima iwe na sheria ambayo inaanalia haki ya wakimbizi. Na pia kuna haki ya ukimbizi, mkimbizi akitoka nchi nyingine kuja kukimbilia Kenya, ni binadamu lazima apewe haki kama hiyo.

Na mimi ninajua watu wa Dadaab watasema, mkimbizi asije kutuumiza. Ndio tunasema lazima kuwe na sheria ambao itaangalia kuwe na balance, yule mkimbizi kwa sababu ni binadamu apewe haki zake, na yule local pia apewe haki zake. Environment pia isiharibiwe, najua watu wa Dadaab wanalalamika wanasema mazingira imeharibiwa ama sivyo?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Kuwe na balance baina ya refugees na wale wenyeji ambao wako hapo hivyo. Na ndio tunaambiwa mwaka mmoja ikiisha baada ya hii Katiba kutekelezwa lazima bunge ya Kenya ipitishie sheria ambayo italingana na sheria ya kimataifa, international law kuhusu refugees. Wakimbizi ambao wanaishi Kenya wataangaliwa vipi?

Freedom of trade, occupation and profession. Uko na haki ya kufanya biashara yeyote unayotaka, hauwezi kuzuiwa kupatiwa license kufanya biashara fulani lakini biashara ya halali, sio biashara kwa mfano ya kuuza clashing cove, au biashara ya kuuza

bangi ama kuuza vitu vingine ambavyo ni haramu. Biashara ambayo ni halali, uko na haki kufanya biashara kama hiyo.

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi jina langu ni Ahmed Sheikh Hussein na ninaishi Dadaab, ninasema hivi katika Katiba mpya, mumeweka kwamba refugees katika nchi zingine hawawezi kupelekwa katika sehemu zingine za Kenya sio Dadaab peke yake au North Eastern peke yake, kwa sababu hii imetuonyesha kwamba hata refugees kutoka Sudan au pahali popote nchi zingine, huwa wanaletwa North Eastern Province, ni kama damping area.

Sasa katika hii constitution, kuna clause ambayo mumeweka ya kusema refugees, popote wanatoka hata kama ni Somalia wanaweza kupelekwa Nyeri au Rift Valley, unaona kitu kama hiyo?

Com. Lethome: Ni sawa ndio tumesema hapa shida ile ambayo iko sasa Sheikh, mimi ninakubaliana na wewe kwa sababu ukiangalia condition ya North Eastern Province ama ya Turkana mahali Kakuma iko, ni condition ambaye haiwezi ku-support population kubwa halafu mnakuja mnaongeza watu wengine mnakuja mnaharibu, ndio tunasema bunge itengeneze sheria ambayo itaangalia hiyo mas'ala na chini ya hiyo sheria ndio inatakiwa sasa wabunge wetu waweze kupigania sheria hiyo iseme kuwa refugees wanapelekwa sehemu ambayo inaweza ku-support ile population.

Ukienda Mandera kwa mfano, ukiingia tu Mandera ni desert sasa, imekuwa ni desert hakuna miti hata moja, kwa sababu ya wale refugees waliwekwa pale karibu kilometer ishirini yote wamefyeka, kwa sababu wanahitaji kuni, wengine wanakuja na mifugo, refugees sisi tunaona binadamu tu, lakini kuna refugees wanyama pia wanakuja na mifugo yao wanaharibu ile environment kabisa.

Kwa hivyo, tunatakiwa tuwe na sheria ambayo itahakikisha kuna hiyo balance, sio wapelekwe North Eastern peke yake au wapelekwe Kakuma kwa wa Turkana peke yake. Hii malalamishi ya watu wa Dadaab pia tumeenda Kakuma, na Turkana wanalalamika kwa sababu environment yao haiwezi ku-support population kubwa, halafu wameongezewa watu wengine, maji ni shida, kuni ni shida, chakula ya mifugo malisho ni shida. Kunatakiwa kuwe na sheria na ndio ninasema chini ya sheria mpya tuna nafasi ya kuchagua viongozi ambao, wanapopitisha sheria bunge, wanaangalia maslahi ya sehemu yao. Wapitisha sheria ambayo itahakikisha kuwa watu wao hawadhulumii ama hawaumii.

Tutaangalia pia habari ya environment baadaye kwa sababu mambo ya refugees pia lazima tuangalie na upande wa environment mazingira. Tumesema habari ya biashara, mtu ana haki ya kufanya biashara yeyote bora iwe ni halali.

Occupation, hauwezi kulazimishwa wewe tunataka uwe polisi, wewe uwe mwalimu ama wewe uwe dereva, una uhuru wa kuamua ile kazi unataka kufanya. Occupation ile unataka una uhuru ya kufanya hiyo bora tu isiwe ni haramu, profession pia hivo hivo, hauwezi kusema mimi ninataka kuwa professional thief, hapana haiwezekani hiyo ama murderer, no. Profession ambayo ni halali una haki ya kuamua ile ambayo unataka na serikali inatakiwa ikusaidie kuweza kuendeleza hiyo kazi yako

kama ni licence wakupatie kama pengine ni certificate fulani unahitaji ikiwa umetimiza kuwangu fulanu cha elimu, upatiwe hiyo certificate uweze kufanya hiyo kazi yako.

Property, mambo ya mali, mtu kumiliki mali ni haki kwa sababu bila mali hakuna maisha. Kwa mfano, wengine mali yao ni mashamba wengine mali yao kama nyinyi ni mifugo na wa Masaai ni mifugo. Kila mmoja awe na haki ya kumiliki mali yake na isiingiliwe ile mali yake bora awe amepata ile mali yake kwa njia ya halali na serikali iheshimu. Mali yako haiwezi kuchukuliwa kwa nguvu kwa mfano kuna sehemu serikali inasema leo barabara inataka kupitia hapa hivi, hiyo ni mali yako.

Ikiwa ni lazima barabara ipitie hapo, basi serikali kama watachukua hiyo mali yako, lazima ulipwe compensation. Kama ni lazima hakuna mahali ingine ya kupitia barabara ni hapo, barabara ni kitu ya kutumiwa na watu wote ni maslaha ya umma lakini mimi pia hii ni mali yangu lazima serikali inilipe kwa sababu ya kutumia mali yangu. Au mzee ako na lorry yake, serikali imehitaji hiyo lorry ya kufanyia kazi fulani ya serikali, hawezi kuja kwa nguvu mzee upende usipende tunachukua hii, haki ni waje wasikizane na wewe. Serikali inataka kutumia mali yako hii, tunataka kukulipa kiasi fulani, unaweza kusema sitaki nimekataa kwa sababu ni mali yako, that is your property haiwezi kuchukuliwa kwa nguvu.

Labour relations, tunajua mara nyingi wafanyikazi wananyanyaswa sana. Anapewa mshahara ambaye ni ya chini sana na hawezi kulalamika. Sheria inasema lazima apewe house allowance, hapatiwi hiyo house allowance, transport allowance, hapatiwi. Wahindi Nairobi ukienda asubuhi utaona ma lorry ile ya kubeba mchanga ndio unakuta binadamu ndani yake wamesimama, kama mvua imenyeshwa unakuta wamejifunika karatasi. Anawabeba na hiyo lorry kwa sababu hataki kuwapatia transport allowance. Mtu anaamua kwenye kazi unasikia mtu amekatika mkono, mkono mzima umekatika kwenye kazi, miaka na miaka halipwi, anapoteza mkono na anapoteza haki yake ya kulipwa.

Kwa hivyo, tunasema lazima serikali itengeneze sheria ambazo zitamuhifathi mfanyikazi. Haki hizo pia zinaingia ndani yake haki ya dini, mfanyikazi asiwekwe kwenye hali ambayo inakwenda kinyume na ndini yake au hali ambayo ni mbaya sana inamdhuru afya yake. Unaweza kuona mtu anawekwa kwenye factory ya simiti, ukivuta ile vumbi ya simiti unashikwa na ugonjwa wa kifua, athsma au TB au ugonjwa mwingine.

Sheria inasema kuwa lazima upatiwe vifaa ya kukuzuia wewe usipatwe na madhara yeyote katika kazi yako, au unafanya kazi mahali ambapo unashika chemicals inakuharibu mwili yako, sheria inasema lazima upewe kitu ya kukuhifadhi afya yako isiharibike.

Kuna kitu inaitwa social security. Kenya hivi sasa mwenye uwezi, ndio anaweza kuishi, it is survival of the fittest. Yule ambaye hana uwezo pengine kwa sababu ya ugonjwa au kwa sababu ya uzee hakuna mtu anamuangalia. Tumesema lazima kuwe na social security ya kuhakikisha kuwa yule mtu ambaye hawezi kujisaidia yeye mwenyewe, sio kwa sababu ya uvivu lakini kwa sababu ya hali yake, mtu kama huyo lazima asaidiwe, apewe mahali pa kukaa na apewe vitu vingine ambavyo anahitaji kwa

mali ya serikali kwa sababu mali ya serikali ni mali ya watu wenyewe, serikali inatoa wapi pesa, si ni sisi wenyewe tunalipa. Tunatoa kodi, kwa hivyo hiyo kodi isimamie wale ambao hawawezi kujisimbia iwaangalie.

Health, kuna sehemu zingine hapa Alhamdullillah mko na dispensary ile kijiji iko hapa katikati mtu akiwa mgonjwa anapelekwa wapi hospitali?

Audience: Garissa.

Com. Lethome: Anapelekwa Garissa, kilometer ngapi? Wangapi wamekufia njiani? Mama akitaka kuzaa, kujifungua na ako na complication, atangojea mpaka afike Garissa huko, kwa mfano mtu hapo njiani ameumwa na nyoka na iko na sumu, utafanya nini? Kwa hivyo tunasema ni haki ya kila Mkenya apatiwe matibabu. Serikali ihakikishe kuna facilities ya kupatia kila Mkenya matibabu.

Na sehemu zingine ukienda kwa mfano Nairobi, unaenda hospitali ya serikali unaandikiwa karatasi eenda ukanunue dawa kwenye chemist, kama hauna pesa hiyo dawa utapata? Wengine sana utakuta mtu ni mgonjwa anaogopa kwenda hospitali kwa sababu anasema hata hospitali ya serikali utakwenda kuandikiwa tu niende kwa chemist. Au unakwenda na mtu, ambaye amegongwa na gari anatoka damu karibu kufa, unamkimbiza kwenye hospitali unaambiwa bila pesa hauwezi kuingia hapa, si inatokea hiyo?

Audience: Mmh.

Com. Lethome: Hiyo ni makosa, ni haki wakati wa emergency mtu apatiwe treatment mambo ya pesa baadaye unaona. Education, mambo ya elimu. Leo ukiwa maskini mtoto wako atasoma? Mtoto anasoma?

Audience: hapana.

Com. Lethome: Unaambiwa elimu ni free lakini unaambiwa mtoto sijui kuna building fund, sijui kuna pesa ya activity kuna nini, imekuwa hata ni ghali kuliko zamani wakati watu wanalipa school fees. Vitabu, mtoto ananunua vitabu nyingi sana imekuwa ni mzigo, watoto wengi hawaendi kusoma kwa sababu elimu imekuwa ni ghali sana. Kwa hivyo tunaambiwa kila mmoja ako na haki ya elimu ya kimsingi na hiyo ni pre-primary, nursery school hiyo, primary na secondary. Hiyo ni haki unaweza kudai kwa serikali kuwa mtoto wako lazima asome mpaka afikie hicho kiwango.

Na ni haki ya kila mtoto kupata free and compulsory primary education, kwa hivyo hapa angalia, free haulipi chochote, compulsory, unaweza kushtakiwa ukikosa kupeleka mtoto primary school unaweza kushtakiwa kwa hivyo mzee, kama wewe kazi yako ni kupeleka watoto kuchunga tu mbuzi kwa baathia na haupeleki school unaweza kushtakiwa, mwalimu atakupeleka kotini atakushtaki, umekataa kupeleka mtoto kupata elimu.

Housing, mambo ya makaazi mahali ya kuishi. Kila mmoja ako na haki ya kupata mahali ya kukaa, binadamu hawezi kuishi kwenye miti kama ndege ama msituni kama mnyama, kila mmoja ana haki ya nyumba ya kuishi. Nyumba ambayo inakubalika

ki binadamu.

Chakula, tunajua wakati mwingine wakati mvua haijanyesha muda mrefu, kuna watu ambao hawana chakula kabisa hawapati chakula, watu wanakufa kwa sababu ya kukosa chakula, imekuwa ni jukumu ya serikali kuhakikisha kila mmoja anapata chakula. Lazima kuwe na food security, kuwa watu fulani kwa mfano ikiwa hawawezi kujilisha, serikali lazima ikawalishe watu kama hao.

Maji, ndio nilikuwa ninazungumzia habari ya maji, kama hapa North Eastern Province, ninajua shida kubwa ni maji kwa binadamu na mifugo. Sheria mpya inasema hapa, kila mmoja ana haki ya kupata maji ya kumtoshia, tumepitia kijiji moja inaitwa Ola. Wanakuambia kwa wiki moja, wanapewa jerican moja ya litre ishirini per family, twenty litres per week per family. Hebu niambie hao ni Waislamu, wanatawadha na hiyo maji, .

Ali Robe: Hapo ni wapi?

Com. Lethome: Ola, kati kati ya, sio Takaba,

Translator: Dandu?

Com. Lethome: No, no, we were going to Takaba,

Translator: Banisa na .

Com. Lethome: Between Banisa and Takaba, iko kijiji kidogo sana hapo hivi, binadamu utafikiri sio binadamu. Maji litre ishirini kwa wiki moja kwa family. Hebu niambie hiyo ni ya kukunywa, ya kupika ya kufua, ya kuoga ama ya kutawadha? Wiki moja, hiyo ni haki. Tumekwenda mahali ingine, unakuta ile maji imesimama barabarani hivi, Wallahi nimeona nguruwe ikioga ndani yake halafu binadamu wanakuja wanafukuza wanaweka miiba hivi wanakunywa hiyo maji, hebu aangalia.

Takaba kuna wakati Baboons, unajua ile *Dhanyer*? Dhanyer wamepigana na binadamu kwa sababu ya maji, sijui kama mnakumbuka hiyo wakati kwa sababu ile shimu ya maji ni moja hakuna mahali ingine iko maji, binadamu wanakuja kunywa hapo, ngombe inakunywa hapo, dhanyer naye anataka maji hapo. Wamepigana binadamu na dhanyer huko Takaba kwa sababu ya maji. Binadamu wamekuwa kama mnyama. Serikali inalazimishwa kuhakikisha kuwa kuna haki kama hizo.

Haki ya mazingira, serikali lazima ihifadhi mazingira kusiwe na kitu ambayo inaharibu mazingira na haki ya wenyewe kutumia vitu kwa mfano, wale wenye kutengeneza kwa mfano soda au kitu kingine ambayo inatumwiwa na binadamu, lazima wahakikishe kuwa haiwathuru hiyo kitu haiwathuru. Kuna watu wengine wanatengeneza chemicals ambazo zinatumiwa na wakina mama ya kujipaka ya kujirembesha, ni haki yao kujirembesha lakini zingine anaenda kutengeneza kumbe ni kuharibu, kuna wengine wanaenda kutengeneza nywele anakuta imetoka yote imemwagika chini kwa sababu ya chemicals.

Kwa hivyo kuna haki ya kuhifadhi wale wenye kutumia bidhaa, consumer rights lazima wahifadhiwe. Fair administration, utawala lazima iwe ni utawala ambaye haidhulumu watu, kwa hivyo na utawala ambayo ni ya haraka. Kwa mfano, uko na shughuli kwa Chief, unaambiwa kesho kuja asubuhi saa mbili, unaingia hapo saa mbili unaambiwa bwana kubwa bado hajamka yuko nyumbani kwake. Anakuja saa nne saa tano, halafu kuna laini hapo hivi, hauwezi kuingia kwa ofisi yake mpaka saa tisa na ukifika ndani, ana kuambia kuja kesho, si inatokea hiyo?

Ama uko na kesi kotini, kesi inachukua miaka mbili, tatu, nne mpaka unakufa kesi yako bado iko kotini ndio tumesema lazima kuwe na fair administration ambayo inafanyia watu kazi haraka. Watu wengine siku hizi hata akithulumiwa unaambiwa nenda ukashtaki kwa polisi, unambiwa hata kushtaki kwa polisi ni kazi bure, ama siyo? Hii itachukua miaka mingi hata itapotea tu, tunataka fair administration na ambayo itafanyia watu kazi haraka, kama ni kotini kesi inafanywa haraka inamalizwa, sio kuweka miaka na miaka. Kila siku unaenda Nairobi rudi, nenda rudi, unataka karatasi pengine kitambulisho peke yake. Nyinyi mkitaka kitambulisho mnachukua wapi? Kitambulisho mnaenda kuchukuwa wapi?

Audience: Garissa.

Com. Lethome: Garissa, unapanda hapa Galkaan ama Gashaan, unatoka hapa unaenda Garissa huko unashinda mchana mzima, siku mbili tatu unaambiwa urudi siku nyingine unakaa, baada ya mwezi unarudi tena huko. Hatutaki mambo ya administration kama hiyo, kutesa binadamu waKenya wasiteswe. Kwa hivyo, serikali ihakikishe kuna sheria ambayo inahakikisha watu wanatumikiwa vizuri na serikali.

Kuna sheria nyingine hapa hivi, unajua kwa sasa unaambiwa polisi kwa mfano hawa AP au mwanajeshi, akiambiwa piga yule mzee risasi. Sheria ya jeshi inasema piga kwanza risasi, halafu unauliza afande kwa nini nipige risasi, kuna faida yeyote ya kuuliza na ushapiga risasi, kuna faida yeyote ya kuuliza?

Audience: Kama mimi niuawe, hakuna faida.

Com. Lethome: Hakuna faida yeyote, ama polisi anaambiwa ile kijiji fulani nafikiri iko na bandits enda mpige risasi huko yote. Polisi anambiwa aende akapige risasi hawezi kuuliza, sheria imesema kuna haki ya ku-disobey, kukataa kutii. Kwa hivyo ukiambiwa nenda kafanye kitu fulani hata kama ni mkubwa wako unaweza kumuuliza kwa nini nifanye hivo na mimi ninaona ni kunyume na sheria kwa hivyo hakuna Mkenya ambaye ana haki ya kufuata amri ambayo ni kunyume na sheria.

Access to court, lazima mahakama iwe karibu na watu, sio iwe mbali huko na iweze kufikiwa na watu wote. Na tunapozungumzia habari ya access hapa, maana yake ni iwe karibu na watu na watu waweze kufikia hata kiwete aweze kufikia hiyo mahakama na isiwe na gharama kubwa inazuia watu kwenda kotini kushtaki. Mimi ni wakili ninajua leo kwa mfano kama unadai mtu pesa, na unaenda kotini lazima ulipe pesa ndio uweze ku-file kesi yako kotini. Umeteta na mtu fulani unataka kwenda kushtaki kotini lazima ulipe pesa kwanza ndio uende ukadai, mtoto wako amegongwa na gari, unadai insurance ikulipe lazima ulipe pesa ndio uende uka-file kesi yako kotini na pesa ni nyingi na utakuta maskini wengi, wanasema ah wacha tu sina

pesa ya kuenda kotini, si ndio hivyo? Sina pesa ya wakili.

Tunasema sheria lazima ihakikishe kuwa watu wanaweza kufikia mahakama bila ya gharama kubwa au iwe karibu na wao.

Rights of arrested person, mtu akishashikwa na polisi yeye ni binadamu ama si binadamu?

Audience: Ni binadamu

Com. Lethome: Kwa hivyo ako na haki zake pia, bado ana haki. Ndio unakuta polisi akishakushika amesha kufunga mkono yako hapa unakuwa wewe ni kama mbuzi ama punda, si ndio hivyo wanafanya?

Audience: Mmh.

Com. Lethome: Na wengine wanasema ameshikwa, sasa ndio ameshikwa si binaadambu? Kwa sababu ameshikwa yeye si Mkenya? Kwa hivyo tunasema mtu yeyote ambaye ameshikwa ako na haki zake, asilazimishwe kuzungumza kama hataki kuzungumza, asilazimishwe kusema ile maneno ambayo hajasema. Unajua siku hizi vile iko, unapelekwa kotini, fulani bin fulani, umepatikana na hatia fulani unakubali ama hauja kubali? Ukisema sijakubali unaambiwa nini? Rudi rumande ama sio?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Kesi yako itatajwa baada ya mwezi mmoja, *Subhana Llahu*, na hiyo rumande ni kama unaishi kwenye kaburi, choo ni hapo hapo, hauwezi hata kuswali, hauna haki zingine za kibinadamu. Sasa watu wengine wanalazimika wanasema, fulani bin fulani umepatikana na hatia ya kuiba, ndio afande nimeiba. Kwa sababu, unataka uondolewe haraka ama sivyo inatakiwa hivyo. Ama polisi, wewe ukienda kotini lazima usema ulikuwa na bangi, utasema? Unasema sisemi, wanachukua rungu unatandikwa, ndio ndio afande nilikula bangi, niko na bangi, kwa sababu ya nini umelazimishwa kutoa information ambayo si kweli, mambo ya torture hakuna tena.

Kama wewe ni Muislamu umeshikwa una haki ya kupewa haki zako zote kama Muislamu, time ya swalah imefika, lazima nipewe mahali ya kuswali, nipewe maji ya kutawadha. Mwezi wa ramadhani imefika nimeshikwa, nipewe haki zangu kama Muislamu, mimi ninafunga.

Haki nyingine ni mambo ya fair trial, lazima usikizwe kotini sio imesikizwa upande mmoja halafu hukumu inatoliwa au wakati mwingine, una hukumiwa bila ya kusikizwa. Kuna watu wengine unashtukia tu umeletewa warrant, wewe ulihukumiwa tarehe fulani na kesi imekata imekwisha, kwa hivyo wewe pengine hii ni ardhi yako ondoka hapa na haujasikizwa. Kila mmoja lazima apewe haki ya kusikizwa. Kuna watu wengine, kwa mfano mimi ninateta na huyu mzee, mimi niko na pesa nimeweka wakili na wakili wamesoma sheria, huyu mzee hajasoma sheria yeye kwa vile hana pesa, anasema atakwenda kujitetea kotini, unafikiri ataweza kubishana na wakili bila wakili?

Kwa sababu, wakili ndio anajua kuzungumza vizuri zaidi judge anamsikiza na hamsikizi yule mzee. Kwa hivyo tumesema kuwe na haki sawa.

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi ni Ahmed Sheikh Hussein from Dadaab town, Garissa District ninasema katika Constitution ya sasa inapea uwezo mtu kama OCS, Officer commanding police station, aweke remand mtu siku kumi nne, two weeks bila ya kupeleka kotini, katika Katiba mpya, mumesema nini katika Katiba mpya ili ku-safeguard Kenyans from this embarrassment?

Com. Lethome: Nafikiri nilikuwa sitaki kuingia kwenye hiyo lakini tunasema mtu apelekwe kotini within 48 hours, hebu angalia Article 68 sub-article E (i) , tunasema hapo, every person who is arrested for allegedly committing an offence has the right

- a. To remain silent, kunyamaza, wacha tuipitie yote, una haki ya kunyamaza sio lazima uzungumze au
- b. To be informed promptly in a language they understand, lazima ujulishwe haraka haraka kwa lugha ambao unafahamu of the right to remain silent, uaambiwe kuwa una haki ya kunyamaza,
- c. Of the consequences of not remaining silent, unaambiwa na ukizungumza matokeo yake ni kadhaa lazima ujulishwe, halafu not to be compelled to make any confession, hauwezi kulazimishwa kukubali jambo fulani, or admission that could be used in evidence against that person, ambayo itatumiwa kama ushahidi kinyume chako and where any such person really choses to make any confession, such confession shall be made before a court or magistrate. Ikiwa unataka kuzungumza, basi iwe mbele ya kotini au kuwe na magistrate, isiwe ni polisi, kwa sasa unaweza kufunguwa pale kwenye cell, unapigwa hapo halafu unazungumza na ile utazungumza itakuwa ni ushahidi kotini. Haiwezi kuwa ushahidi mpaka ikiwa umefanya mbele ya magistrate au mbele ya kotini.
- d. To be held separately from persons who are serving sentences, hauwezi kufunguwa pamoja na watu ambao wamehukumiwa tayari, kwa sababu wewe unaposhikwa wewe ni suspect bado haujahukumiwa, pengine hautapatikana na hatia ni haki yako usifungiwe pamoja na wale watu ambao wamehukumiwa tayari.
- e. To be brought before a court as soon as reasonably possible, apelekwe kotini haraka iwezekavyo, but not later than 48 hours after being arrested. Hauwezi kufunguwa zaidi ya 48 hours, lazima upelekwe kotini and not later than the end of the first court day after the expiry of the 48 hours au kwa mfano kama ni weekend ikipita ile 48 hours upelekwe kotini haraka iwezekanavyo. Kwa hivyo OCS hana hiyo haki tena, ya hiyo fourteen days.

Kuna hii mambo ya emergency, kwa sasa Rais ako na haki ya kusema nime-declare state of emergency, na akisema kuna state of emergency, maana yake sheria imekuwa suspended, sheria haitumiki, unaona polisi ama jeshi wanaingilia watu ovyo, ni wakati gani ambapo kunaweza kuwa na state of emergency?

Sheria mpya inatuambia emergency inaweza kupatikana wakati ambapo pengine kuna tishio ya vita, Kenya imekuwa na vita na nchi nyingine au imeingiliwa na nchi nyingine au pengine kumekuwa na mchafuko katika nchi au kumetoa pengine mafuriko au

mtetemeko ya ardhi au mambo mengine ambayo si ya kawaida. Hapo tu peke yake ndio kunaweza kuwa na state of emergency.

Na hiyo state of emergency sio kufanya ovyo ovyo, lazima iwe kulingana na sheria ambayo tukiendelea tutaona baadaye. Kuna sehemu ambayo ningependa kuzungumzia ambayo iko pale mwanzo lakini nimeweka mpaka mwisho, tungezungumzia kuhusu hizi haki zote za binadamu lakini kama nilivyowaambia pale mwanzo, hakuna haki ambayo haina mpaka. Kwa mfano, haki ya kumiliki mali sheria imesema, you have the right to own property, lakini jee una haki ya kwenda kuchukua property ya mtu mwingine?

Kwa hivyo iko na limitation zake, na haki hiyo pia, isiwe ni haki ambayo unatumia kudhulumu watu wengine, kwa hivyo you have the freedom of movement lakini hiyo freedom yako ya movement isiwe unaingilia mpaka haki yangu mimi. Au uko na freedom of worship. Haki yako ya ku-worship isiingilie haki yangu ya ku-worship, kwa mfano kuna sehemu zingine watu wanalala wakipiga ngoma usiku wanaimba, kama Nairobi hivi kuna watu kama jumapili usiki wanalala wakipiga ngoma wanaimba, watu hawawezi kulala, wanasema ni freedom of worship. Haki yao isiingilie haki ya watu wengine kwa hivyo kila haki iko na kiwango yake. Isipitishie hicho kiwango.

Na ikiwa umeona kwa mfano haki yako imefunjwa, haki ya kibinadamu, haki yako ya kumiliki mali, haki ya kuishi, haki ya kutembea mahali unapotaka, haki yako ya dini, sheria mpya inasema, una haki ya kwenda kotini au kwa Commission ya human rights, au kwenye tribunal yeyote kwenda kusema kuwa haki yako ya kibinadamu imefunjwa.

Kuna swali lolote kuhusu haki za kimsingi, ni pumue kidogo na nyinyi muulize swali kama kuna swali lolote kabla hatujaingia katika sehemu nyingine ambao ni muhimu?

Translator: *Sucal miye chirta carinta xaqa kofka wadhaniga kuxisabsan ee kaxathleysa oo sucal ee?*

Isaack Abdille: *Magaeiga Isaack Abdille layiraxa oo Dadaab kunol, waxan weidhineya Katibathan xatha usuban xathan muxu nayiri ninkan naxor fadiyo ninki nin dhilo, Katibatha xore ee Kenya wexei exeth in latogto oo lathilo xatha waxa layiri wax lathileya malex carinti wala bethete Katibathi wala bethete, marka ninki nin xatha thilo, katibathan Kenya usuban daxthetha, ninki nin dhilo maxa chisathisi marka, tii xorey xathi labetheley ninki lathili chirey?*

Translator: He is asking in the current Constitution we are using, there was the death penalty and according to our draft the death penalty is removed, what is in place after that is removed?

Com. Lethome: Life imprisonment.

Translator: *Maxa waye kofka xabsi dhain waye.*

Isaack Abdille: *Oo lama toganaye?*

Translator: *Maya.*

Com. Lethome: Mpaka wanakufia huko jela. Tukiingieni sasa mambo ya uchaguzi, mambo ya elections na mambo ya political parties tuangalie, kwanza hapa tunaambiwa kuwa itakuwa ni haki ya kila Mkenya kupiga kura na pia kusimama kuchaguliwa. Ukitaka kusimama kuwa Rais, kama umetimiza ile masharti iko, uko na haki, ukitaka kuwa mbunge uko na haki, kupiga kura ni haki yako. Kwa hivyo serikali pia lazima ihakikishe kuwa kila mmoja yule ambaye amefikisha umri wa kupiga kura, akitaka ile card ya kupiga kura anapata. Kitambulisho anapata kwa urahisi, kura itakuwa kwa siri, secret ballot si ile mambo ya acclamation ya kuinua mkono na kupiga kelele, kwa siri.

Unaamua vile unataka kwa sababu kama hapa North Eastern nimesikia ikiwa kwa mfano mnasema leo kura yetu tutapigia yule jamaa Degodia, unaambia mpaka mama, unamuambia sikiza, hoyo lazima na wewe umpigie huyo, usimpopigia utaona. Mama ako na haki ya kupiga kura vile anataka kwa siri yake, mtoto ana haki ya kupigia kura mahali anataka, sio unasema lazima upigie mlango yetu ama mtu fulani, hapana. Ni secret ballot kila mtu apige kwa siri, itakuwa ya uhuru na uadilifu na pia kutakuwa uakilishi, watu wanawakilishwa kwa njia ya uadilifu na pia tutahakikisha kuwa wanawake pia wanawakilishwa katika Council na katika bunge lazima waweko.

Na pia Electoral Commission, unajua watu wengi sana wanalalamika kuhusu hiyo Electoral Commission, wanasema inapendelea upande mmoja. Chini ya sheria mpya, Electoral Commission lazima iwe independent, ninaona mkono huko juu, ngoja, njoo karibu wewe ni kijana bwana bado uko na nguvu.

Idhil Abdi: Mimi ninaitwa Idhil Abdi ninatoka Dadaab. Swali ninayouliza ni ya kwamba, shida nyingi ni kutoka polisi,

Com. Lethome: Polisi, ndio.

Idhil Abdi: Sasa kuna mambo za torture, kuna mambo ya kunyanganya watu mali yao wenyewe na hauwezi ukaenda kueleza shida zako na hakuna kitu ya kusaidiwa. Sasa ningeliza ni sheria gani ambayo mumewekea polisi wakisumbua watu ama wakifanya shida kama hizo isiyo kwenye sheria, mumetengeneza gani inayoweza kusaidia watu?

Com. Lethome: Nafikiri ni vile haukuwako, tumezungumzia hiyo, umeondoka hapa. Tumesema kuwa kwanza mamlaka ile ambao polisi wako nayo au kiongozi yeyote katika serikali ni mamlaka ya watu. Lazima aitekeleze kulingana na sheria, na jee akikudhulumu? Kwa sasa hakuna mahali unaweza kuenda si ndio?

Audience: Mmh.

Com. Lethome: Tumetengeneza Commissions ambayo unaweza kuenda kumshtaki hata polisi, Inspector hata Abongo, Commissioner of Police unaweza kuenda kumshtaki chini ya hii sheria mpya.

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi ninaitwa Ahmed Sheikh Hussein, naishi hapa Dadaab. Ninauliza kuhusu njia ya election hapa, hasa Electoral Commission, ninaona Electoral Commission of Kenya wamedhulumu watu wa North Eastern Province, hiyo Commission haifanyi fair services vile inafanywa katika sehemu zingine za Kenya kwa mfano, Electoral Commission iko na ofisi katika Districts level na haina ofisi katika divisional levels. Kama tuseme kuna malalamishi fulani kuhusu nomination hapa, tuseme hapa kuna election ya Councillors katika division au location, mpaka uende Garissa akutane na District Co-ordinator huko ndio atoe malalamishi, hakuna ma ofisas katika divisional level ambao wanafanya chini ya Co-ordinator huyo. Na hakuna communication baina ya Commission na wananchi, sasa katika Katiba hii, imetupatia nini sisi watu wa North Eastern ili tuweze kuondolewa katika hiyo shida?

Com. Lethome: Sasa hapa hatuwezi kuzungumzia habari ya North Eastern kwa sababu hatutarajii kuwa kwenye Katiba tutasema Electoral Commission lazima ifanyie watu wa North Eastern kitu fulani. Hapa tunasema wanapewa muongozo wa kisheria. Tumesema hapa kuwe na Electoral Commission ambayo ni independent ambayo haiegemei upande mmoja, ambayo itakuwa ina-treat watu wote sawa.

Na tunaambiwa katika kazi zake ni ku-conduct and supervision of elections. Wawe kazi yao wanasimamia mambo ya elections, sasa nafikiri haya mapendekezo yako yanaingia kwenye sheria, lazima kutakuwa na Act ambayo inasimamia Electoral Commission na ikiwa kwa mfano mnaona kuwa ofisi ziko mbali sana na watu, sasa chini ya hiyo sheria unaweza kusema kuwa lazima wa-establish offices katika kila constituency, sio katika District peke yake. Kwa sasa unasema ofisi ziko kwenye District peke yake?

Ahmed Sheikh Hussein: Yes.

Com. Lethome: Watu wanaweza kusema iwe kwenye constituency, kwenye division hata mpaka location, hayo ni mambo ambayo yanaweza kuwa, sio katika Katiba, katika sheria, Act of Parliament ndio wanaweza kuangalia hivyo. Lakini tumesema hapa katika kazi zao ni ku-manage elections kwa njia iliyo sawa, na njia iliyo sawa ni pia kuhakikisha kuwa wanafikia watu wote, wako karibu na watu wote. Hiyo haiwezi kuingia kwenye Katiba, because that is a detail, inaingia kwenye sheria ambayo inahusia mambo ya elections.

Mambo ya uchaguzi, Parliament itatengeneza sheria ambayo itasimamia mambo ya uchaguzi wote. Kama ni mambo ya Councils, kama ni mambo ya Parliament na kama ni mambo ya nomination. Kwa hivyo sheria hii ambayo itaundwa na bunge ndio itakayo simamia lakini Katiba imesema bunge itatengeneza sheria kama hiyo.

Haki ya kupiga kura, unaambiwa Mkenya yeyote ambaye amefikisha miaka kumi na nane na zaidi ako na haki ya kupiga kura, hauwezi kuzuiwa na mtu yeyote kupiga kura. Watu wengine watasema sisi hatuwezi kupiga kura kwa sababu sina kadi ya

kupiga kura si ndio? Na hauwezi kupata kadi ya kupiga kura bila kitambulisho, na kitambulisho kupata ni kazi kubwa. Ndio tumesema serikali lazima iweke sheria na mipango ya kuhakikisha kuwa kila mmoja anapewa kitambulisho na kila mmoja anapewa kadi ya kupiga kura.

Kufanya registration ukiwa na miaka kumi na minane ama zaidi, basi una haki ya wewe kupewa registration ya kupiga kura, na bora uwe Mkenya, basi una haki ya kupiga hiyo kura. You want to change? Ile kupiga kura yenyewe, watu wengine hawajui wapige kura namna gani, iko complicated yaani ni ngumu zaidi kupiga kura, kwa hivyo chini ya mapendekezo ya sheria mpya, tunasema kuwa lazima ihakikishwe mambo ya kupiga kura ni rahisi ni nyepesi kila mmoja afahamu. Hata yule *ayeyo* ambaye hajasoma aweze kupiga ile kura.

Pia mnasikia kunatokea uizi ya kura, si mnasikia kura inaibiwa, kura inaibiwa, wakati mwingine mnapiga kura mnapigia mtu fulani, mwenye kushinda ni mwingine ama haijatokea mambo kama hiyo?

Audience: Imetokea.

Com. Lethome: Inatokea, ballot box kwanza, nchi zingine unakuta ballot box ni transparent ni ya kio, yaani unaweza kuona ndani yake iko namna gani. Sasa hizi ballot box ambayo tunaletewa ni rangi gani?

Audience: black.

Com. Lethome: Unaweza kuona ndani?

Audience: Hapana.

Com. Lethome: Tunaambiwa kuwa zingine inakuja iko na makaratasi ndani imejaa, hauwezi kuona, mnaambiwa angalia hii debe namna hii lakini huko ndani haujui iko kitu gani ama sivyo?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Sasa imeambiwa lazima iwe transparent. Kama tutapiga kura chini ya Katiba hii, lazima ije kama glass hivi, unaona ndani iko kitu gani watu waonyeshwe hakuna kitu ndani yake na mnaangalia kura vile zinaingia ndani yake. Ndio tunasema hivyo transparent. Halafu kuna shida nyingine inatokea, kwa mfano mnapiga kura hapa, mwaka ya 97 mlipigia kura wapi?

Audience: hapa.

Com. Lethome: Imehesabiwa wapi?

Audience: Modogashe.

Com. Lethome: Wapi, Modogashe, mnapiga hapa inabebwa inapelekwa Modogashe si ndio?

Audience: ndio.

Com.Lethome: Hapa katikati ya barabara mnajua ile kitu inatokea?

Audience: Hapana.

Com. Lethome: Kwa nini isihesabiwe hapa, kura ya watu wa Dadaabu inahesabiwa hapa hapa, Modogashe inahesabiwa huko huko, Sabuli inahesabiwa huko huko. Kwa hivyo sheria inasema kura ihesabiwe katika polling station, sio kubebwa. Imejulikana hapa katikati wakati inasafirishwa, ingine inapotea ingine inazaa. Kuna ingine inazaa na ingine inakufa hapa njiani kwa hivyo hiyo imeondolewa.

Halafu tunaambiwa ikiwa mahali kuko na mtu mmoja tu amesimama, tunasema un-opposed candidate, mtu ambaye hajapingwa na mtu mwingine, basi tunaambiwa kuwa watu waende wakapige kura, lazima kura ipigwe hata kama yuko un-opposed, kwa sababu anaweza kuwa un-opposed hakuna mtu mwingine amesimama na yeye lakini he is not popular, tunataka tujue hata kama ni un-opposed lakini ni watu wangapi wamemuunga mkono.

Kwa hivyo hata akisimama kwa mfano Lagdera, amesimama mtu mmoja peke yake, hatuwezi kusema he has been declared the winner, no. kwanza ipigwe kura tunataka kujua strength yake ya kura ni ngapi ambao wamempigia kura, na tutatangaza ushindi wake baada ya kura kuhesabiwa.

Tunaambiwa pia lazima kuwe na Commission Commission hii hivi sasa watu wengi wanasema hii Commission inapendelea upande gani? Upande wa serikali ama sivyo?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Kwa sababu Chairman wa Commission amechaguliwa na nani?

Audience: President.

Com. Lethome: Na President mwenyewe. Tunataka an independent Commission, na ambayo itakuwa na wawakilishi kutoka vyama vyote vya kisiasa na wawakilishi kutoka sehemu mbali mbali za Kenya. Tunasema wawe watu sio chini ya nane na sio zaidi ya kumi.

Tuanguie Chairman wa Commission atachaguliwa na nani? The Chairperson of the Commission and other member shall be appointed by the President and approved by Parliament. Lazima ipelekwe Parliament wapitisha, Parliament wakikataa uchaguzi wa Rais, lazima achague mtu mwingine. Kwa hivyo Parliament ndio itaamua nani atakuwa Chairman wa Commission.

Halafu pia Commission yenyewe ndio watachagua Vice Chairman vile watakavyo fanya kazi. Na kazi ya Electoral

Commission, sikizeni sasa hapa hivi muangalia tofauti baina ya sheria ile iko sasa na hii mpya. Kwa mfano tarehe ya uchaguzi mwaka huu ni tarehe ngapi?

Audience: 29th December.

Com. Lethome: Nani anakumbia, unajuaje? Nani alikuambia ni tarehe ishirini na tisa December?

Audience: Sio hii, the other elections.

Com. Lethome: The other election, who decided it is 29th?

Audience: Moi.

Com. Lethome: The President, who will decide the elections this year?

Audience: Ni yeye tena.

Com. Lethome: Ni yeye tu. Inakuwa ni siri ya mtu mmoja, yeye ndio anaamua, kwa mfano kama sasa tuko hapa, tunazungumza habari ya Katiba, waKenya wengi wanasema wataka uchaguzi chini ya Katiba mpya, lakini sisi sote tunajua kuwa itafanyika chini ya Katiba mpya President akitaka. Kwa sababu anaweza leo leo tuko hapa, avunje bunge na atangaze tarehe ya uchaguzi. Hii Katiba ya zamani hajavunja sheria, Constitution ya zamani imempatia hiyo haki lakini sasa tunataka kuweka hayo mamlaka chini ya Electoral Commission. Kazi yao sikiza,

Registration ya watu wenye kupiga kura na sio mara moja, saa hii ukitaka ku-register as a voter unaweza ku register, unaambiwa umefungwa si ndio? Kuna wakati fulani wanafungua kuna wakati wanafunga. Chini ya sheria mpya tunasema lazima iendelee, continuous registration.

Demarcation of electoral constituencies, mipaka ya sehemu ya kupiga kura, wao ndio watakuwa wanapanga hiyo mipaka kulingana na idadi ya watu na kulingana na ukubwa wa ile sehemu.

Wao ndio watakuwa wanasimamia elections,

Wao ndio watahakikisha kuwa uchaguzi umefanyika kwa njia ya sawa sawa,

Wao ndio watasimamia political parties,

Na wao pia ndio watasimamia kutakuwa na political party's fund, kutakuwa na funds ambayo ni ya political parties. Electoral Commission ndio watasimamia.

Ikiwa kuna matatizo kuhusu mambo ya uchaguzi wao ndio watasimamia,

wao pia ndio wataelemisha watu kuhusu haki zao za kupiga kura,

wao pia ndio watasimamia mambo ya observation, kuna watu wanatoka nje wanataka kuja kuangalia uchaguzi imefanyika kwa njia ya haki ama la. Wao ndio watasimamia.

Na pia mambo ya monitoring na evaluation,

Electoral Commission itakuwa ni independent Commission ambayo itakuwa inafanya kazi kulingana na hii

Katiba. Kwa hivyo mambo ya uchaguzi yote itakuwa inasimamiwa na Electoral Commission bila kuingiliwa na mtu yeyote mwingine.

Na wafanyikazi wa Electoral Commission watakuwa wanaajiriwa na Public Service Commission.

Public Service Commission nafikiri tutafikia baadaye tutaanglia Public Service Commission ni wakina nani? Kuna haki ya political parties, una haki ya kutengeneza chama chochote cha kisiasa ambacho unataka katika chini ya sheria hii mpya. Na pia political party yeyote kwa mfano leo hii, ni political party gani ambayo ni tajiri sana Kenya?

Audience: KANU.

Com. Lethome: KANU, zingine kina SAFINA, kina nani utakuta hata ofisi pengine hakuna ama sivyo. Wakati wa uchaguzi hata gari ya kupeleka watu kufanya campaign hakuna, utakuta mwingine mpaka helicopter ya kufanya campaign ako nayo ama sivyo? Kwa hivyo tunataka political parties zote wawe wanasimamiwa na serikali, ziwe funded.

A political party is entitled to financial support from the state on the basis prescribed in an Act of Parliament. Lakini si kila political party, unajua tukiambiwa kila moja itapewa pesa, mimi na bibi yangu na watoto tutatengeneza yetu, si ni pesa inatoka kwa serikali. Huyu Shiekh na vijana wenzake, ile football team yenu mnasema hii ni political party si mnapata pesa, lakini kuna sheria ya kusema ni gani ambayo itakuwa funded sio kila political party, itakuwa nyingi sana.

Halafu, hakuna ruhusa kutumia mali ya serikali au ya taifa ku-support political party yeyote, sasa inatokea au haitokee hivo? Kuna political ambayo inatumia mali ya serikali, yaani hauwezi kutafautisha baina ya mali ya serikali au mali ya party. Kwa mfano tunajua Raisi ndio Chairman wa KANU, wakati anaenda mkutano wa KANU, si mkutano wa taifa, anabebwa na gari ya?

Audience: serikali.

Com. Lethome: Bodyguard, state, ile mali yote wanatumia pale ni ya state. KBC ambaye inakuja kum-cover ni state. Tunataka kuwe na tofauti baina ya political party na state lazima iwe tofauti tofauti na ndio sasa watu wengine wanalalamika, hawajui KICC ni mali ya serikali au ni mali ya chama, hajjulikani mpaka sasa, ile nyumba kubwa iko Nairobi mnajua?

Audience: Kenyatta Conference.

Com. Lethome: Kenyatta Conference hajjulikani kwa hivyo lazima kuwe tofauti baina ya state na political party. Na kutakuwa na sheria ambayo itapitishwa bunge ya kusimamia political party. Isiwe political party zingine wanavunja sheria na wengine hawavunji sheria, watakuwa chini ya sheria moja, political party zote.

Registration of political party, leo hii nani na register political parties, inafanyiwa wapi registration? Registrar of Society ndio wana-register political party. Sasa tunaambiwa kuwa, the Electoral Commission is the Registrar of political parties. Yeye ndio

atafanya registration ya political parties.

Halafu tunaambiwa bunge itapitisha sheria kuhusu mambo ya political parties ile ambayo inaweza kuwa registered, ile ambayo haiwezi kuwa registered kutakuwa na sheria. Unajua kwa mfano IPK imekata kuwa registered inasemekana kuwa ni chama ya kidini. Registrar of Societies ndio amesema hivyo, sio Electoral Commission, sasa tumetoa mamlaka kutoka kwa Registrar of Society kwa sababu political party is different from a Society, inawekwa chini ya Electoral Commission, wao ndio watakuwa wanafanya registration.

Kuna qualification ya registration sio chama yeyote ambayo inaweza kuwa registered. Wale wataangalia kama ime-qualify ama haija-qualify ni Electoral Commission. Hata cancellation pia itakuwa ni chini ya Electoral Commission.

Kisha tuingia katika political party's fund. Tunaambiwa kutakuwa na fund ambayo itajulikana kama political party's fund, itakuwa chini ya Electoral Commission, wao ndio watasimamia hiyo fund. Na hiyo fund itatoa wapi pesa? Tunaambiwa itakuwa inatoka Parliament, kwa hivyo kutakuwa na budget ya political party's fund, it will be by Parliament, kila mwaka itakuwa inatolewa na tunaambiwa itakuwa ni 0.3% of the national budget.

Kwa hivyo 0.3% of the national budget itakuwa ni budget ambayo itaenda katika hii political party's fund.

Ya pili itakuwa ni donations, kama pengine kuna watu wanataka kufanya donations, kwa sasa tunajua kuwa kila chama inajitafutia donations. Kwa hivyo chama zingine zinapata zingine hazipati, lakini sasa kutakuwa na fund ambao kila chama itaweza kupata hizo funds. Hiyo fund kazi yake itakuwa ni nini? Itakuwa ni ya ku-cover elections expenses, ile gharama yeyote ambayo kila party inatumia katika elections itakuwa inasaidia ama itakuwa inalipiwa na hiyo fund. Kwa mfano wengine wanataka kununua airtime katika radio au katika magazeti, hiyo itatumika kwa hiyo.

Civic education katika kuwalemisha watu, na katika ku-promote democracy katika nchi kwa sababu mpaka sasa watu wengi hawajui haki zao za kupiga kura, haki zao za kuchagua wachague mtu wa aina gani. Kwa hivyo kuna umuhimu wa political parties kufundisha watu haki zao za kisiasa. Gharama wanaotumia itakuwa inatoka katika hiyo fund.

Halafu 10% ya kusimamia mambo yao ya ofisi, mambo yao ya administration itakuwa inatoka katika hiyo fund. Katika party discipline, tunajua hivi sasa kuna party zingine wakiingia mkutano mahali fulani lazima kutatokea fujo ama sivyo? Watu wapigane kwa mawe, watu wavurugane, watu waumizane. Kwa hivyo, kila party itatakiwa ionyeshe Katiba yake kama ina-promote hiyo mambo ya discipline ama sivyo, na wakivunja hiyo Katiba wanaweza kuchukuliwa hatua.

Article no.100 inasema hivi, The President and public officials and above the rank of a Deputy Secretary shall not hold office in a political party. Rais, au mtu yeyote ambaye ana mamlaka katika serikali hadi kufikia kiwango cha Deputy Secretary, hana

haki ya kuwa na cheo chochote katika political party. Kwa mfano leo tuko na Rais, he is the President, he is the Chairman of KANU, au unakuta mtu pengine Vice President ndio Vice Chairman wa KANU au mtu pengine ni Governor wa sehemu fulani, pengine Permanent Secretary wa Ministry fulani, unakuta yeye pengine ndio secretary wa chama fulani. Lazima itenganishwe baina ya cheo katika serikali na cheo katika party.

Kwa hivyo kuanzia serikali mpya chini ya hii Katiba, hatuwezi kuwa na President au Prime Minister ambaye pia ni Chairman wa political party. Akichaguliwa tu, anawacha hiyo kiti, party inachagua mtu mwingine kwa sababu kuna abuse of power. President leo hii hawezi kujua kwa mfano leo yuko upande za Western kwenye campaign huko, haujui ameenda huko kama President ama Chairman wa KANU, haijulikani, Raila Odinga juzi alikuwa Garissa, hatujui kama alikuwa huko as a Secretary General of KANU or as Raila. Ama Minister, he is a Minister of Energy. Hatujui amekuja huko kama Minister au kama Secretary General wa KANU, lazima tutofautishe hizo vyeo.

Sasa tuingie katika mas'ala ya bunge, sijui kama mnataka tuvunje kikao kidogo watu waende wakaswali halafu warudi ama vipi? Sheikh unaonaje? We take a rest of 1 hour?

Translator: most of them have moved out, wameenda msikitini.

Com. Lethome: Tutarudi saa nane Inshaallah halafu tutaendelea. Sasa hiyo muulize huyu bwana kwa hivyo saa nane Inshallah tutarudi tutaendelea. Sasa tutaendele na mazungumzo yetu kuhusu mambo ya Katiba hii mpya. Asubuhi tumeangalia tukasema, hii Katiba mpya imepatia nguvu wananchi na ikasema hiyo nguvu itapelekwa kwa bunge na ingine itapelekwa kwa mahakama na ingine itapelekwa kwa Executive, wale wenye kutekeleza hiyo sheria.

Sasa nataka tuangalie habari ya bunge, chini ya sheria mpya hii bunge itakuwa namna gani. Sasa bunge itabadilika haitakuwa kama vile sasa tunajua bunge moja. Itakuwa bunge mara mbili, bunge ya kwanza ndio tunaita National Council, Council ya umma au ya taifa na nyingine itaitwa National Assembly kama ile ambayo iko sasa. Halafu yote mbili wakikaa pamoja ndio tunaita Parliament, sasa tutaangalia kila moja itakuwa na kazi ama itaundwa namna gani. Ama kazi ya bunge kwanza kabla hatujaangalia hiyo National Council ni kitu gani na National Assembly ni kitu gani?

Kazi ya bunge itakuwa ni kuwakilisha wananchi, kwa sababu sisi wote hatuwezi kutengeneza sheria, sisi wote hatuwezi kutawala wale ambao wanatuwakilisha katika hiyo mambo ya kutengeneza sheria ndio bunge, na pia bunge itakuwa ni alama ya umoja ya nchi ya Kenya na hiyo ndio itakuwa inaamua sheria ambayo itatumika katika nchi.

Kwa hivyo watatengeneza sheria lakini kwanza watakuwa wakizungumza na wananchi kabla ya kutengeneza sheria. Pia itakuwa ni nafasi kwa mfano watu wa Dadaab, mko na mbunge wenu wa Lagdera kule, ikiwa mko na maneno yeyote ambayo inawahusu ninyi, yeye ndio anatakiwa kuja kuwasikiza nyinyi halafu anapeleka huko. Hiyo ndio kazi ya bunge kusikiliza malalamishi ya wananchi au matakwa ya wananchi.

Ile pesa ambayo inatumika na serikali inapitishwa kwa bunge hata sasa budget inasomwa kwa bunge, bunge ndio inapitisha hiyo. Na pia bunge ndio itakuwa inaangalia serikali, serikali inafanya kazi ama haifanyi kazi halafu katika hii sheria mpya, waziri hatachaguliwa na President. Unajua sasa President ndio anachagua na sasa kwa vile hawa wanajua kuwa President ndio anachagua kila mmoja anajipendekeza kwa President. Kila mmoja anataka kujifanya yeye ni mzuri kwa President ndio achaguliwe akuwe Minister lakini chini ya sheria mpya, minister hachaguliwi na President, atakuwa anachaguliwa na bunge, President atakuwa tu ana-confirm.

Kuna hawa watu wanachaguliwa kama Attorney General, Director wa Parastatal hizi kampuni za serikali, Chairman wa Coffee Board na zingine, wale wote wanachaguliwa na President sasa, watakuwa wanachaguliwa na President lakini bunge ndio inapitisha, yaani bunge akikataa hakuna mtu anaweza kupita.

Bunge pia itakwua inaangalia Raisi anafanya kazi vizuri ama hafanyi kazi vizuri, kwa sasa bunge haina hiyo uwezo na pia itakuwa inaangalia Vice President, inaangalia Prime Minister na wale Ministers wote, ma jaji wote, yeye ndio anawaangalia na watu wengine wote ambao wako katika ofisi kubwa watakuwa chini ya bunge. Bunge ndio inaangalia hao, sasa ni President peke yake ndio anaangalia, na ndio sababu unaweza kufungulia habari ya saa saba unasikia waziri fulani amefutwa kazi, si mnasikia hiyo kila mara?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Ukikosana na Raisi tu anafutwa kazi, kwa sababu yeye ndio amechagua, yeye ndio anafuta. Yule mwenye kuchagua ndio anafuta pia lakini sasa hiyo nguvu ametolewa kwa President amepatiwa Parliament.

Hebu tuangalie ni mambo gani ambayo Parliament pia itakuwa inafanya katika ku-approve ama watu wale ambao watakuwa wanachaguliwa na bunge. Kuna Prime Minister ambaye ndiyo atakuwa ni mkubwa wa serikali, yeye lazima uchaguzi wake upitie kwa bunge. Kuna deputy Prime Minister, yule msaidizi wa Prime Minister, yeye pia lazima achaguliwe na apitishwe na bunge.

Kuna Ministers watachaguliwa, Deputy Minister, hakuna Assistant sasa, hakuna Assistant Minister, tunasema Deputy Minister. Unajua tofauti iko hivi, ukisema assistant, maanake wewe ni msaidizi tu, wakati minister hakuna yeye ndio unafanya hiyo kazi hauna kitu wewe lakini u-deputy unakuwa uko na powers pia. Kwa hivyo sasa tumeondoa Assistant tumeweka deputy vice chair. Ni kama vile Deputy ya shule, ako na kazi pia anafanya, si anaongoja tu wakati Headmaster hakuna ndio anafanya, hata wakati Headmaster yuko, Deputy pia ako na kazi yake. Kwa hivyo sasa hakuna Assistant Minister tena, iko Deputy Minister.

Kuna Permanent Secretary, sheria hii ambayo iko sasa, President ndio anachagua ni nani Permanent Secretary, Ambassadors na High Commissioners, Electoral Commission, Commission ya uchaguzi, yote itapitia bunge. Auditor General, yeye ndiye

anahesabu pesa ya serikali inatumiwa namna gani. Controller of Budget, huyu ndio anasimamia budget ya serikali pesa inatumiwa namna gani.

Director of Central Bureau of Statistics, mahali iko ile maelezo ya serikali ya nchi nzima yule anasimamia hiyo atachaguliwa na bunge pia. Governor wa Central Bank pia atapitishwa na bunge, hapitishwi na mtu mmoja.

Kuna Commissions zingine ambayo haiwezi kuchaguliwa mpaka ipitie kwa bunge ya kwanza ni:-

- Judicial Service Commission. Hiyo Judicial Service Commission ni ile ambayo inasimamia kuchaguliwa kwa ma jaji, hiyo pia lazima ipitie bunge,
- Ethics and Integrity Commission, kuna Commission ambayo inasimamia wafanyikazi kama wanafanya kazi kulingana na sheria ya hiyo kazi,
- National Land Commission, ile inasimamia Ardhi yote, unajua sasa kuna Commissioner of Lands, mtu mmoja tu ndio anasimamia mambo ya ardhi yote Kenya nzima, sasa itakuwa Commission. Hiyo pia itakuwa inachaguliwa kupitia kwa bunge,
- National Environmental Management Commission, ile ambayo inasimamia mazingira, msiharibu msitu, msiharibu miti, msilete kitu ambayo inaharibu maisha ya wanyama ama vitu vingine,
- Teachers Service Commission, ile ya kusimamia walimu pia itakuwa inachaguliwa kupitia kwa bunge,
- Kutakuwa na Commission ya Mshahara, unajua kwa sasa mumesikia wabunge wamejiongezea mshahara si ndio? Kwa mfano leo hii nikikuambia jiongeze unataka mshahara kiasi gani utaweka ngapi yako mwenyewe?

Audience: Ile mimi ninataka.

Com. Lethome: Ile wewe unataka. Wananchi wamelalamika wakasema hatutaki, hatutaki wabunge wenyewe wajiwekee mshahara, sasa bunge itachagua Commission, hiyo Commission ndio itaweka mshahara. Unajua haiwezekani mtu kujichagulia yeye mwenyewe, kila binadamu ni *hunguri* unajua *hunguri*, sasa ukiwa ni *hunguri weine* ukiambiwa ujiwekee chakula utaweka ngapi?

Audience: mingi mingi.

Com. Lethome: Kila binadamu iko na hiyo tamaa.

- Halafu kuna Commission ya Constitution. Hii kazi yake ni kuangalia kuwa hii Constitution inafuatwa na imetekelezwa yaani imekuwa implemented kwa kizungu tunasema hivyo.
- Kuna Commission on Human Rights and Administrative Justice, ya kuangalia haki za kibinadamu na kuhakikisha mtu yeyote ambaye amedhulumiwa ameangaliwa haki yake.
- Ofisi ya Attorney General, Mkuu wa Sheria, uchaguzi wake pia utapitia kwa bunge.
- Kuna yule mtu ambaye anasimamia mashtaka, yule anashtaki upande wa serikali, tunamwita Director of Public

Prosecution pia uchaguzi wake unapitia kwa bunge,

- Kuna ofisi moja tunaita Public Defender, Public Defender ni mlinzi wa raia. Unakumbuka asubuhi tumesema chini ya sheria ya sasa mtu wa serikali akikudhulumu hakuna mahali utapeleka, Chief iko mahali unapeleka wewe? Polisi, hakuna. Sasa tumeweka Public Defender kazi yake ni kulinda haki ya raia, raia akithulumiwa, hiyo inaangalia. Sasa yule atachagua hii ni bunge kwa sababu ikichaguliwa na mtu mmoja, itapendelea wacha ichaguliwe na bunge. Nchi zingine wanaita hii Ombudsman lakini Kenya tumeamua kuiita Public Defender. Ukithulumiwa na Chief, askari ama mtu yeyote katika serikali unakwenda huko kulalamika. Hiyo ni ofisi ambayo ni independent na polisi ama watu wengine.
- Halafu kuchagua Police Commissioner. Leo nani anachagua Police Commissioner?

Audience: Moi.

Com. Lethome: President ndio anachagua, hata Moi akiondoka mwingine ndio atachagua kwa sababu Katiba imemupatia hiyo haki. Na ndio unaona anapendelea watu wanasema huyu ni mtu wa Moi, kwa sababu yeye ndio amechagua. Sasa uchaguzi wake pia utapitia kwa bunge.

Ma jaji wote watachaguliwa na bunge sasa na Chief Kadhi wa Kenya. Unajua Chief Kadhi wa Kenya sasa anachaguliwa na mtu mmoja hata Waislamu hawaulizwi mnataka huyu mtu ama hamtaki? Na ndio mnaona anaharibu mambo ya Waislamu kwa sababu hatujamchagua sisi wala hajachaguliwa na bunge amechaguliwa na mtu mmoja.

Kwa hivyo Chief Kadhi na Judge wa High Court wote watachaguliwa kupitia kwa bunge. Tumesema matumizi ya bunge yote, na ya serikali yote lazima ipitie kwa bunge. Sasa hebu tuangalie hiyo Parliament itakuwa namna gani? Tumesema kutakuwa na bunge mbili, sasa swali ambayo tunajuliza namna gani bunge mbili? Sasa tusikilize vizuri kabisa.

Tunaambiwa kutakuwa na bunge mara mbili, ile ya juu tutaita National Council hiyo hakuna sasa, itaitwa National Council na ya pili itaitwa National Assembly kama ile iko sasa. Yote ikiungana pamoja ndio inaitwa Parliament, sasa tuangalie hii National Council ni kitu gani. Sikilizeni makini kwa sababu hii ndio itawawakilisha nyinyi huko.

National Council itakuwa na watu sabini, na hawa watu watakuwa wanachaguliwa on the basis of single member constituencies, watakuwa wanachaguliwa kutoka kwa wilaya ama katika District. Sasa tuko na District sabini, watakuwa wanachaguliwa watu sabini kutoka huko. Halafu kutakuwa na viti vingine thelathini za wanawake na hawa watakuwa watatoka katika mikoa, katika sehemu mbali mbali na Nairobi pia. Hawa ndio watakaa katika National Council.

Kwa hivyo National Council hii maana yake watu kutoka katika District huko mbali mbali wanachaguliwa mtu mmoja mmoja, tuko na wilaya sabini. Halafu kwa vile wanawake wanabaki nyuma sana, kutakuwa na viti thelathini, hizi viti thelathini watapatiwa wanawake, wawili peke yao ndio watatoka Nairobi na wengine watatoka katika sehemu zingine za Kenya. Kwa hivyo watakuwa watu mia moja, sabini halafu na wale wengine thelathini. Kwa hivyo kutakuwa na watu mia moja.

Sasa hawa ni wawakilishi wa watu kutoka katika mikoa na katika District ambao watakaa katika National Council. Wanawakilisha matakwa ya watu kutoka katika kila sehemu wanakaa katika ile National Council. National Assembly watakuwa ni wale wajumbe ambao tunawajua kwa sasa, wale wanachaguliwa kutoka katika kila constituency. Sasa wakikutana hao wawili wote ndio inakuwa Parliament.

Tunaambiwa kuwa, katika kuchagua hawa watu wote, lazima tuhakikishe pia katika kila nyumba, ile National Council na National Assembly, one third lazima iwe wanawake, thuluthi moja lazima wawe ni wanawake. Kwa mfano, yaani ukigawanya mara tatu sehemu moja lazima wawe ni wanawake kwa sababu wanawake wamebaki nyuma sana. Kwa mfano kama sasa ukiangalia bunge yetu iko na watu mia mbili ishirini na mbili, wabunge wote, wanawake sijui ni wangapi, mnajua wangapi katika bunge?

Haya ngoja, tuna Martha Karua, tuna Kittony, tuko na Mariam Matano, Tabitha Seii, nani mwingine?

Translator: Mwarere

Com. Lethome: Mwarere wa Mwachai nani mwingine ako huko? Charity Ngilu na nani mwingine? yaani hawajafika kumi, they are less than ten I think naam hawajafika kumi hata tukiwa hesabu wote kwa hivyo tunataka wanawake wawe ni wenye kuwakilishwa kwa thuluthi moja katika bunge.

Kuna kitu muhimu hapa tuangalie, wale ambao wanachaguliwa kuwa huko;

Mtu kuchaguliwa kuwa huko lazima awe ni Mkenya, hauwezi kuchagua mtu ambaye si Mkenya kuenda katika bunge, Awe na miaka thelathini na tano kama anachaguliwa kutoka kwenye National Council wale ambao wanawakilisha District na Provinces, awe amefikisha miaka thelathini na tano, na kama ni ile National Assembly hii bunge ya kawaida, miaka ishirini na moja, kama sasa, umefikisha ishirini na moja? Sasa wewe unaweza kupigania kiti ya Lagdera, wewe pambana na Shidiye, ukiweza kutoa Shidiye unaingia huko na kama umefikisha thelathini na tano kama wazee hawa, sasa wanaweza kupigania kitu ya ile National Council wanaenda huko.

Halafu lazima uwe ni mtu ambaye ako na kitambulisho ya kupiga kura. Hauwezi kuchaguliwa kama wewe hauna kitambulisho ya kupiga kura. Uko nayo wewe? Ya kura, ya kupiga kura, hauwezi sasa kuchaguliwa hiyo kiti umepoteza sasa wewe.

Jumla ya bunge, is it three hundred plus ninety. Ngoja tutaangilia tutaona.

Mbunge yeyote lazima awe amesoma mpaka Form four na awe pia amepita, sio Form four tu lakini hajapita, awe amepata pass na awe anajua Kiswahili na Kiingereza.

Lakini pia kuna watu ambao ni bubu, hajui Kiswahili hajui Kiingereza, hajui lugha yeyote, anajua ile sign language. Pia mtu kama huyo anakubaliwa kuwa mbunge ama kuingia katika bunge,

Na pia mtu atakuwa anaangaliwa tabia yake, sio mtu alikuwa ni mwizi, mkora halafu mnamchagua mnampeleka huko. Mtu atachunguzwa tabia yake, kuna watu wengine wanaiba pesa ya watu, mali ya watu halafu anachaguliwa anakwenda bunge huko badala ya kutengeneza ana kwenda kuharibu.

Halafu unaambiwa mtu hawezi kuchaguliwa kama yuko katika cheo ingine, pengine mtu amechaguliwa kiti ingine mahali halafu unachaguliwa tena kuwa mbunge, haikubaliwi hivyo kwa sababu tunataka kugawanya kazi. Mtu asiwe katika cheo kingine cha kuchaguliwa halafu pia unachaguliwa kwenda bunge, sasa mtu atagawanya kazi mara ngapi. Utafanya hili ama ufanya hii? Kwa hivyo tunasema mtu asiwe ana ofisi nyingine ambayo amechaguliwa kutumikia wananchi.

Na mtu awe na akili timamu, ukipeleka mtu *maj'nun* atafanya kazi gani, hawezi.

Na pia awe ni mtu ambaye si bankrupt, mnaitaje kwa Kiarabu tunaita *mufilis* mtu ambaye amefilisika na pia asiwe ni mtu ambaye amefungwa. Kwa mfano mtu amefungwa kwa sababu ya amefanya hatia na amefungwa yuko jela lakini kwa sababu mnampenda mnamchagua, hawezi kutumikia watu na afungwa jela.

Mtu ambaye alikuwa amefungwa miaka kumi iliyopita. Huyo mtu alikuwa amefungwa katika hiyo miaka kumi iliyopita kwa sababu ya makosa, makosa ambayo ilimfunga kwa muda ya miaka mitatu ama zaidi. Mtu kama huyo ambaye ameonja jela miaka hii kumi iliyopita, tunasema mtu kama huyo hafai.

Na isiwe ni mtu ambaye amefukuzwa kazi, kwa mfano mtu alikuwa anashikilia mamlaka kwa serikali, amefutwa kazi kwa sababu ya kufanya mambo mabaya ndani yake. Mtu kama huyo hawezi kuchaguliwa kwa hivyo ukisikia mjumbe anasimama anataka kuchaguliwa na unajua huyu mtu alikuwa anafanya kazi sijui kwa DC, ama kwa Ministry fulani ama kwa bank fulani amefukuzwa kwa sababu ya kuiba, au ya kufanya mambo mabaya. Mtu kama huyo hawezi kuchaguliwa kuwa huko.

Hebu tuangalie wakichaguliwa wanakaa muda gani kwa bunge. Tunasema mtu atakaa huko bunge na hawezi kutoka isipokuwa itokee moja kati ya haya mambo yote;

1. Yeye mwenyewe akiandika barua anaomba anataka kutoka, resignation, anaomba hataki kufanya hiyo kazi unajua hauwezi kulazimisha mtu, kwa hivyo akiandika barua kwa Speaker wa bunge aseme mimi ninawacha kiti yangu, lakini hiyo mnafikiri mjumbe wowote atafanya hivyo? Hakuna hawawezi labda awe anashikiwa bunduki hapa ndio atafanya hivyo, lakini hiyo ni njia moja.
2. Kutokee sababu yeyote ambayo inamfanya mtu kama huyo awe hafai kuwa ni mbunge. Kwa mfano tumemchagua amekwenda bunge halafu tunagundua yeye si Mkenya, lazima atoke wakati huo.
3. Amechaguliwa halafu anajulikana baadaye kuwa huyu mtu alikuwa mwizi, anatoka bunge,
4. Sababu nyingine yeyote ambaye ingemzuia kupigania kile kiti ,
5. Bunge ikivunjwa kwa mfano kama sasa tunaongojea wakati wowote bunge inaweza kuvunjwa, bunge ikivunjwa yule MP anaweza kusema hapana mimi ni MP bado, MP ya wapi na hakuna bunge, bunge imeshavunjwa. Kama sasa wote roho iko mkononi hawajui itavunjwa saa ngapi, ikivunjwa tu wote wanapoteza kiti yao.

6. Mtu akipotea kwenye bunge vikao vinane, ambayo inafuatana bila ya kuwa na sababu. Unajua kwa sasa kuna wengine wanafanya ile kitu tunaita technical appearance, anaenda tu anaonyesha uso yake halafu anatoka. Mwingine haendi bunge kabisa, haendi, sasa tunasema hapa, akichelewa kwa kikao nane na hana ruhusa kutoka kwa Speaker wa bunge, basi mtu kama huyo anakosa nafasi yake kwa bunge.
7. Pia akipatikana kuwa, kwa sababu sasa huku nyuma kuna kitu tunaita leadership code, kuna sheria ya viongozi, lazima viongozi wote wafuate hiyo sheria. Basi akivunja hiyo sheria ya uongozi, kiongozi anatakiwa kufanya hivi, kiongozi anatakiwa kufanya hivi, akivunja sheria kama hiyo basi pia anaweza kuondolewa. Kwa sababu viongozi wengine, kwa mfano leo ikiwa kuna msaada wa kuja hapa, viongozi wengi wanafanya nini, kwa mfano wamepewa msaada pelekea watu wa Dadaab Lagdera, viongozi wengi wanafanya nini? Hivi ni nini mzee, sema tu usiogope.

Sheikh Hassan: Anarusha.

Com. Lethome: Anarusha, mara nyingi anaanza kukula yeye ndio anapelekea watu wake. Sasa hiyo ni kinyume na kiongozi, kiongozi anatakiwa anapatia kwanza watu wake sio yeye mwenyewe anajiangalia kwa sababu yuko pale kwa niaba. Ni kama baba, tuseme wewe ni baba kwa nyumba yako, halafu iko chakula kidogo, unaambia watoto kwanza *sug* mimi mpaka nishibe kwanza, wewe ni baba mzuri kweli?

Audience: Hapana mzuri.

Com. Lethome: Unakula halafu ukishiba ile imebaki kidogo unapatia watoto ama hakuna kitu unatoka, huyo ni baba mzuri?

Sheikh Hassan: Sio Baba huyo

Com. Lethome: Sasa kiongozi pia tunataka wafuate sheria ya kiongozi, kiongozi anatakiwa afanye nini. Inginge hapa hii ni mpya sasa sikilizeni, if recalled by the electorate in the members constituency in accordance with the Constitution. Ikiwa wananchi wale wamemchagua wamemuambia rudi, haufai, sasa yule mbunge wenu yuko huko, unaweza kumrudisha hapa?

Audience: Mbeleni hakuna.

Com. Lethome: Mpaka amalize miaka tano ndio anakuja tena sasa anawaambia mzee nipatie kura tena, si ndio mwaka hii wanakuja sana?

Audience: Eh.

Com. Lethome: Hii mwaka kwa sababu ni mbaya wanataka kura, ukishachagua basi, mpaka miaka tano. Kuna sehemu moja sitaki kusema ni wapi, wale Commissioners, hapana mahali ingine mbali, Kenya tu lakini mbali sitaki kusema jina ya mahali mtajua ni nani, Commissioners wameenda huko wakati wameenda, mbunge amefuatana na wao, wale wananchi wa hapo wameambia Commissioners, asante sana umeletea mbunge wetu, sisi hatujamuona tangu miaka tatu, tunashukuru umetuletea

sasa ndio tunaona sasa. Sasa wananchi chini ya hii Katiba mpya, wana haki ya kumuita, kusema wewe haufai, hautufanyii kazi unaweza kurudi sasa wanamuitisha unaona. Yes, kabla ya kuisha ile miaka tano wana haki ya kumuita arudi.

Halafu kuna hii shida nyingine kwa mfano, mbunge wenu mumechagua kwa tikiti ya KANU si ndio? Akifika huko bunge anahama anaingia party ingine, huko huko bungune, basi inasemekana akitoka party ile imemchagua aingie party nyingine, hiyo kiti yake atakosa na lazima arudi tena akapigiwe kura. Infact wabunge wengine wanatumia maneno machafu wanasiasa wanasema political prostitution, umesikia hiyo, wanaita prostitution, yaani anatanga tanga kila mahali.

Kama umechaguliwa kwa tikiti fulani, wewe vumulia miaka yako ikikwisha utaenda party nyingine kwa sababu hiyo ni kama kudanganya wananchi. Wananchi wamepigia kura kwa sababu ya party fulani, wameridhika na hiyo party. Wewe unakwenda huko bunge unaruka ingine haujauliza wananchi wale wamekuchagua ni kama umewadanganya wale wananchi.

Ndio tunasema hapa they will be subjected to a leadership code of conduct, hata saa ile ukikuja ndio nilikuwa ninazungumzia hiyo. Kutakuwa na code of conduct ambayo nafikiri iko katika one of the schedules hapa nyuma, wanasema kuwa kutakuwa na code of conduct hebu angalia, look at Article 111, are you there 111 umepata hiyo?

Ahmed Sheikh Hussein: Yes.

Com. Lethome: Haya twende mpaka mahali utaona E, kwa sababu kuna 1 halafu A,B,C mpaka E. Umeona mahali iko E?

Ahmed Sheikh Hussein: Yeah.

Com. Lethome: Hebu soma hiyo E.

Ahmed Sheikh Hussein: If a member is found guilty by a tribunal of violation of leadership code of conduct the punishment is or through the vacation of office of a Member of Parliament.

Com. Lethome: So there will be a code of conduct, yaani kutakuwa na sheria ya kuangalia tabia ya viongozi. Kiongozi akienda kinyume na hiyo code of conduct anatolewa, mbunge akienda kiyume na hiyo code of conduct anaondolewa. Sasa ni muhimu pia tujue hiyo code of conduct itakuwa namna gani. Hiyo imefahamika, sababu nyingine ya kutoka bunge, mtu akiwa amechaguliwa kama independent candidate, hakuna party yeyote, halafu ukifika huko bunge, unaenda unajiunga na party na wewe wakati umechaguliwa uko independent kwa mfano Sheikh Mohammed amechaguliwa hana party yeyote, kwa hivyo watu wamekuwa na imani na yeye, sio kwa sababu ya party, kwa sababu ni Muhammed.

Akienda huko anaenda anabadilika anaingia kwenye party basi ile kiti amepoteza kwa sababu pengine ameingia ile party ambayo wananchi wa Dadaab hawataki na yeye ni mwakilishi wa watu wa Dadaab, kwa hivyo atapoteza kiti yake. Nafikiri hiyo ni mzuri.

Sasa hebu tuangalie mtu anaweza kuitwa wakati gani, ni wakati gani mnaweza kurudisha mbunge wenu na mumuambie kuja

hapa. Angalia 112. Mtu anaweza kuitwa kurudishwa kutoka bunge ya kwanza;

1. Ikiwa mwili yake au akili yake imekuwa na upungufu fulani hawezi kutimiza ile kazi yake, kwa mfano mtu amekuwa mgonjwa kabisa, hawezi kufanya kazi, au ameingia akili yake imepunguka amekuwa *maj'nun* huyo mtu anaweza kuwakilisha wananchi? Basi mtu kama huyo mnaweza kusema arudishwe,
2. Mtu amevunja ile sheria ya viongozi, yaani amefanya mis-conduct, hafanyi vile kiongozi anavyotakiwa kufanya,
3. Analeta chuki baina ya watu,
4. Anafanya ile ofisi ya mbunge idharauliwe, kwa mfano unasema ah mbunge gani huyu tunamuona anafanya mambo mbaya amefanya ile ofisi idharauliwe. Basi yule mtu mnaweza kumuita tena,
5. Anakaa mbali na watu wale wamemchagua kwa muda mrefu, nyinyi mumechagua mumempeleka bunge, anafaa kila wakati kuja kuwatembelea, mko na shida gani, ndio apelele huko bunge. Amekaa tangu mumechagua anakuja wakati wa kura tu ndio anakuja. Basi mkiona anakaa sana mtu kama huyu, na hakuna sababu yeyote, basi mtu kama huyo mnaweza kusema hapana huyu mtu arudishwe hapa.

Lakini sasa mtafanya namna gani kwa sababu tunajua hii inaweza kutumiwa vibaya. Kwa sababu kwa mfano, tuseme mimi na huyu Muhammed tunapigania kiti ya kura ya hapa ya bunge, yeye amenishinda mimi nitafurahi?

Audience: Hapana.

Com. Lethome: Nitakuwa nakasirika kwa hivyo nitafanya bidii huyu atolewe ama sio?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Sasa sheria inaangilia watu wasitumie vibaya hiyo nguvu itakuwa ile kitu tunaita kwa kizungu witch-hunting, ati huyu amenishinda ataniona lazima nitoe yeye, nitaenda kufanya fitina mpaka atolewe. Sasa tunasema hapa, ili kumrudisha mbunge kwanza;

- Lazima kuwe na maandishi petition kwa maandishi, msem sababu kwa nini mnamtaka yule mbunge arudishwe hapa sio bila sababu yeyote lazima kuwe na sababu.
- Halafu lazima kupatikane signature asili mia thelathini, 30% signatures ya wale watu ambao walimpigia kura, unaona, signed at least by 30% of the registered voters of the constituency and shall be delivered to the appropriate Speaker. Yaani asili mia thelathini ya watu wote walikuwa wamejiandikisha kupiga kura kwa mfano kama ni Lagdera basi lazima upate signature ya 30%. Kwa mfano kama watu wale wamejiandikisha kupiga kura Lagdera yote ni elfu tatu, unatakiwa upate kura ya watu wangapi? Elfu moja, 30% unagawanya mara tatu, unaona lazima upate watu kama hao. Halafu utapeleka hiyo petition kwa Speaker, kama ni National Assembly, utapeleka kwa Speaker wa National Assembly, kama ni National Council, utapeleka kwa Speaker wa National Council.

Halafu akishapata, tunajua kwa sasa mara nyingi yule Speaker kwa sababu hajui wewe anajua yule mbunge, anaweza kufanya mambo ingine anakalia ile petition yenu ama sivyo? Sasa Katiba inasema nini, Katiba inasema hivi mkishapeleka hiyo petition iko na signatures ya watu elfu moja hiyo yaani 30%, anapewa siku saba peke yake, yule Speaker lazima

aambie Electoral Commission, iende ikachunguze ni kweli hii maneno ama si kweli. Okay?

Sasa Electoral Commission inaambiwa lazima ifanye haraka sana iende ikachunguze halafu ilete report kwa Speaker wa bunge. Speaker hawezi kukalia anapeleka kwa Commission, Commission naye hawezi kukalia lazima aende akachunguze halafu alete report. Wakishaleta report kwa Speaker na Speaker akiona ni kweli huyu mtu

- Haendi kwa watu wake,
- Huyu mtu akili kuisha haribika,
- Miraa imeharibu akili ama kitu ingine mbaya imeharibu akili yake,
- Huyu mtu ana mambo mabaya anafanya basi mtu kama huyo reporti yake ikisharudi kwa Speaker, yule Speaker atasema hiyo kiti yake imekuwa empty, ata declare ile kiti ya mbunge ya Lagdera sasa imekuwa vacant hakuna mtu hapo, kwa hivyo lazima tupige kura nyingine sasa okay.
- Na kama pengine wameenda kufanya uchunguzi na wameona kuwa si kweli, yule mtu hawezi kupoteza kiti yake, kwa hivyo lazima uchunguzi ifanyewe, kwa sababu ni fursa nzuri kwa wananchi lakini inaweza kutumiwa vibaya pia. Itakuwa watu saa zote ule anashindwa kura anaanza kuchokora, anaanza kutafuta yule mwingine atolewe ama sivyo? Kwa sababu hata kama ni mimi tumeshindana na wewe, umeingia bunge mimi nimebaki, sitakufurahia nitajaribu nitakuambia utaniona nitakutoa. Nitaanza kuzunguka huko kutafuta signature ya watu, hata nitalipa pesa si ndio? Unalipa pesa watu waweke signature umtoe ndio uitishe huko. Kwa hivyo kumewekwa hiyo taratibu yote.

Halafu bunge itaweka sheria ya taratibu ile ambayo itafuatwa, Katiba haiwezi kuweka taratibu yote, bunge imeambiwa hapa lazima itawekwa katika sheria zake. Tunaambiwa Speaker na Deputy Speaker ndio watakuwa wanasimamia shughuli za National Council na pia katika ile National Assembly kutakuwa na Speaker na Deputy Speaker wake.

Nafikiri ni muhimu tuangalie hawa watu wanachaguliwa vipi. Unaambiwa katika ile National Council, yule ambaye atakuwa anaongoza mkutano ya National Council ile ambayo itakuwa bunge ya juu, the upper house ya wakilishi katika mikoa na katika wilaya, basi atakuwa ni Speaker. Wakati Speaker hayuko, kutakuwa na Deputy Speaker ndio atasimamia hapo, na kama Deputy Speaker hayuko basi member yeyote ambaye anaweza kuchaguliwa na wale wengine ataweza kusimamia hiyo mkutano ili iweze kuendelea.

Kutakuwa na Clerk of National Assembly ambaye pia atakuwa amechaguliwa na Parliamentary Service Commission na mapendekezo yake yatapitishwa na Council yenyewe.

Tunaingia katika National Assembly, kama ile ambayo iko hivi sasa. Tutakuwa na Speaker na Deputy Speaker na utaratibu utakuwa vile vile kama National Council. Speaker anasimamia kama hayuko Deputy Speaker, kama hayuko mmoja katika wabunge anachaguliwa kusimamia vikao kama vile

Tuangalie mshahara ya wabunge, Section 121, Emoluments of Members of Parliament. Hii kila mahali tumeenda wananchi wamelalamika sana, mshahara au malipo ambayo wanapata wabunge. Tunaambiwa hapa, mbunge atalipwa mshahara na allowance na marupurupu nyingine ambayo itaamuliwa sio na wao wenyewe. Kwa hivyo kutakuwa na hiyo Commission ndio itaamua mshahara na benefits za wabunge.

Halafu pia, tunaambiwa mbunge yeyote hatakubaliwa kufanya kazi ingine nje ambayo itagongana na kazi yake kama mbunge. Sisi tumechagua aende bunge akatuwakilishe lakini yeye kazi yake kubwa ni kwenda ku-import sukari kutoka nje, anafukuzana na ma-lorry yake huko ya sukari, atatuangalia sisi ama ataangalia ma-lorry yake huko? Si atafanya biashara yake? Kwa hivyo, kazi yeyote ambayo itagongana na kazi yake kama mbunge amezuia kufanya kazi kama hiyo.

Kuna shida nyingine ambayo inatokea, angalia Section 124, unajua bunge ndio inapitisha sheria, inatengeneza sheria halafu wanapeleka kwa Rais. Rais ndiye anayeweka signature yake, akiweka inapita, asipoweka haipiti. Sasa wakati mwingine, anaweza hasiipende ile sheria, akiletewa hawezi kuweka signature na anyamaze nayo na kulingana na sheria mabaya iko hivi sasa hamuezi kumlazimisha yeye kuweka signature.

Sasa hebu tuangalie katika hii sheria mpya tunasema hii. wanasema hapa, bunge ikipitisha sheria yeyote basi yule Speaker atapeleka kwa President kufikia kwa siku ngapi? saba. Kufikia siku saba anapeleka kwa President ili aweze kuwesa sign yake.

Tunaambiwa mwiongoni mwa hizo siku saba, yule President lazima afanye kitu, hawezi kukaa tu, lazima afanye kitu. Kitu moja ambayo anaweza kufanya anaweza kupeleka hiyo bill kwa ile mahakama kubwa iangaliwe pengine anataka ichunguzwe. Ni sawa ama sio sawa ama inavunja Katiba ama sio vipi, na mahakama itapewa siku kumi na nne ya kumuambia Rais hii sheria ni mzuri ama si mzuri. Hiyo ni kitu ya kwanza ambayo lazima Rais afanye.

Ya pili, anaweza kurudisha hiyo bill siku saba kabla haijaisha kwa Speaker na awaambie angalieni hiyo sheria mara nyingine mpya. Okay? Kwa sababu pengine, ameona kuna kitu fulani ambayo pengine ni mbaya ndani yake ama ni kitu ambayo hawezi kupitisha kwa hivyo atarudisha au apitisha hiyo sheria. Kwa hivyo, amepewa siku saba ya kuchagua mambo tatu afanye, moja apelikote kotini ikaangaliwe au arudishe iangaliwe tena au akubali. Kwa sasa sio hivyo, anaweza kukaa kwa muda mrefu sana bila kupitisha anayamaza tu, na unaambiwa ikipita miezi kadhaa, inapotea hiyo sheria, lazima irudishwe tena bunge. Kwa hivyo hapa tunaona kuwa kuna control ya President.

Hebu tuangalie Section 127 tumejua sasa kuna wabunge mbili. Kuna ile bunge ya kawaida kama hii na kuna ile nyingine ambayo tumeita National Council. Wakati wa kupitisha sheria hebu tuangalie hii bunge ya National Council inatusaidia namna gani. Tunaambiwa ikiwa sheria imepitishwa na bunge moja, basi yule Speaker lazima apeleke kwa ile bunge nyingine iende

ikaangaliwe kwa sababu bunge moja inawakilisha watu kutoka katika mikoa, National Council kwa hivyo haiwezi kupita sheria bila kupitisha kwa bunge ile nyingine. Kwa hivyo sheria ikitoka kwa bunge ya chini lazima ipitishwe kwa bunge ya juu au ikitoka kwa bunge ya juu lazima ipitishwe kwa bunge ya chini kabla haijapelekwa kwa Rais.

Wakati mwingine sheria inaweza kutoka kwa nyumba ya chini ikipelekwa kwa bunge ya juu imekataliwa au itoke juu ikipelekwa chini imekataliwa. Sasa utafanya nini hapa na sheria lazima ipitishwe wananchi pengine wanangojea hiyo sheria. Kutachaguliwa kamati ya watu kutoka kwa bunge zote mbili wakae pamoja waweze kuangalia ni namna gani wanaweza kusikilizana ili hiyo sheria iweze kupita.

Na hiyo Committee ikikataa kusikizana basi watapiga kura na thuluthi mbili, two thirds wakiweza kupiga kura kukubaliana na hiyo bill inapita. Thuluthi mbili, wanasemaje kwa Kisomali thuluthi mbili? Mzee waambie kwa kisomali, two thirds kwa kisomali?

Audience: *Hal lava mel*

Com. Lethome: Basi, nafikiri sasa mumefahamu hiyo amewaambia kwa Kisomali. Na wakikubaliana basi itapita, lakini wasipokubaliana itapigwa kura hiyo. Hebu tuangalie Article 129 inasema nini? Rights to petition Parliament. Ikiwa kwa mfano kuna hivi sasa kuna sheria yeyote ambayo wananchi hawapendi, kuna kitu unaweza kufanya kwa sasa? Kama kuna sheria ambayo inawadhulumu wananchi, hakuna kitu unaweza kufanya. Lakini chini ya hii sheria, unaambiwa, the right of every person to petition Parliament to enact amend or repeal any legislation is reserved.

Kila mwananchi ako na haki ya kuandika barua kwa bunge kutaka bunge iondoe sheria fulani au iweke sheria fulani au ibadilishe sheria fulani. Kwa mfano ukiona sheria ambayo inahusiana na mambo ya immigration au mambo ya vitambulisho ni mbaya, mwananchi yeyote ako na haki ya kuandika barua kwa bunge ili waweze kubadilisha hiyo sheria. Kwa hivyo hapo imepatia mwananchi pia haki ya ku-petition bunge iweze kupitisha sheria yeyote na hii ni haki ambayo tulikuwa hatuna kama wananchi.

Kuna taabu nyingine ambayo inapatikana bunge sasa, mnasikia kitu fulani haijapitishwa bunge kwa sababu hakuna quorum, unajua maana ya quorum? Sheikh Muhammad hebu waambie quorum kwa Kisomali ni nini?

Sheikh Muhammed: Kama hatoshi watu

Com. Lethome: Ki sheria, kwa mfano sheria ile ambayo iko sasa, wambunge ni mia mbili ishirini na mbili, quorum yao ni thelathini peke yao, thirty only. Na wakati mwingine sheria inakataa kupitishwa kwa sababu hakuna thirty kwenye bunge. Kwa hivyo quorum ni matatizo makubwa sana wananchi humia kwa sababu wabunge wamekataa kwenda bunge kupitisha.

Na pia ni hatari kuweka thirty peke yake kwa sababu kama kuna sheria ambayo itadhulumu watu fulani, wakijikusanya

wabunge thelathini waende bunge, watapitisha hiyo maneno. Iko chini sana hiyo quorum, ama sivyo? Si iko chini sana? Ukiangalia thirty kwa mia mbili na ishirini ni kidogo sana. Wanaweza kupitisha mambo yeyote, sasa hapa tunasema the quorum of either house shall be 30% of all members of that house, sasa imepekwa juu imekuwa 30% badala ya ile ya thirty people.

Lugha ya bunge, kutatumika lugha tatu bunge, ya kwanza ni Kiswahilin, ingine ni ya Kiingereza na ingine ni sign language. Kwa sababu kuna watu ambao hawasikii ama hawawezi kuzungumza wanatumia sign language. Kwa hivyo katika bunge lazima kuwe na sign language interpreters wale ambao wanatafsiri, kwa sababu tumesema hatutaki mtu yeyote abaguliwe. Asubuhi tumeangalia bill of rights, tukasema mtu hawezi kubaguliwa kwa sababu yeye ni kiwete, kipofu, kiziwi, ama bubu.

Katika bunge wanapiga kura namna gani? Ikiwa jambo lolote wanataka kupitisha kule kura itakuwa ni majority, wale wengi wakipiga kura kuunga mkono jambo kama hilo, linapita katika bunge.

Kama kuna swali lolote kuhusu bunge kwa sababu ninataka kuingia katika sehemu nyingine ambayo ni muhimu sana ya Judiciary. Kuna swali yeyote kuhusu mambo ya bunge?

Mohammed Abdow Hashi: Mohammed Abdow Hashi, ilikuwa system yetu ya Presidential sasa imebedilishwa?

Com. Lethome: Imebadilishwa sasa itakuwa Parliamentary. Prime Minister na bunge ndio itakuwa na nguvu ya kupitisha mambo nyingi kwa hivyo itakuwa Parliamentary sasa naam. Umefahamu hiyo sasa? Tuangalie kitu kingine,

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi Jina langu ni Ahmed Sheikh Hussein. Chama cha NDP ya Raila, ilikuwa ni chama kusema ukweli ya kabila moja na ni mfano ya kuonyesha kwamba kunaweza kutengenezwa chama cha kikabila, halafu chama hiyo wakati ilivunjwa iliingia katika KANU, walikubaliana kwa sababu walikuwa ni watu kabila moja, wakasikizana waingie kwa KANU, si ku-represent wa Kenya lakini wale watu ambao wamechagua hawa kabila yao.

Sasa katika Constitution hii mpya, katika kuunda political parties, kumeangaliwa mambo kama hiyo party isiwe ni ya kikabila?

Com. Lethome: Sasa hiyo tutarudi asubuhi mahali tumeangalia political party. Imesema party isiwe ni ya kikabila au ya kidini au ambayo itabagua watu wakabila zingine ama sehemu zingine. Iko ukiangalia under political parties utaona hiyo iko.

Sasa kuna hii mambo ya kuvunja bunge, ni mambo ambayo inasumbua wananchi sana kwa sasa kwa sababu kulingana na hii sheria ya sasa, nani ako na mamlaka ya kuvunja bunge? President peke yake, yeye ndiye anaamua kuvunja na atavunja wakati gani ako na hiyo haki. Pengine wiki hii tunaweza kusikia bunge imevunjwa, wananchi wengine wanasema tunataka uchaguzi chini ya Katiba mpya. Lakini tunajua haiwezi kuwa mpaka President mwenyewe akitaka, asipotaka atavunja bunge wakati wowote. Na maoni ya wananchi wengi hata hapa tulipokuja, wamesema hawataki bunge ivunjwe kwa mapenzi ya mtu mmoja.

Hebu tuangalie mapendekezo hapa imependekeza kitu gani? Angalia 142, kwanza tunaambiwa hapa, National Council ile bunge ya pili itakuwa inakaa kwa muda wa miaka nne, itachaguliwa kwa muda wa miaka nne.

National Assembly hii ambayo tunachagua wabunge, itakuwa miaka ngapi? Tano kama vile iko sasa ile itakuwa miaka nne na hii miaka tano. Sababu ya kuweka hivo hatutaki uchaguzi yote iwe mara moja, kwa sababu ikiwa mara moja yote itafika wakati ambapo itakuwa kwanza gharama ni kubwa sana mara moja. Na wakati wa uchaguzi watu wanajishughulisha sana na mambo ya uchaguzi, kwa hivyo tunataka iwe kuna tofauti ya mwaka mmoja.

Na wakati mwingine muda inaweza kuongezwa kwa mfano, ikiwa Kenya iko katika vita, Kenya iko na vita na nchi ya jirani kama Somalia, Tanzania ama nchi nyingine yeyote, hatuwezi kuenda kufanya uchaguzi na lazima bunge ibaki hata kama muda yake imekwisha, wanaweza kupiga kura wakipata asili mia sitini na tano, basi ile bunge inaweza kuendelea hata kama muda wake imekwisha. Lakini haiwezi kuendelea kwa zaidi ya miezi sita, wanaweza kuongeza miezi sita peke yake.

Na unaambiwa haiwezi kuongezwa zaidi ya miezi kumi na mbili. Kwa hivyo tunaongeza miezi sita ikiwa vita pia bado inaendelea tunaongeza ingine sita, zaidi ya hapo haiwezi kuongezwa. Sasa kuvunja bunge, sio Rais ameambiwa avunje bunge sasa kwa sababu ya uchaguzi, temeweka tarehe ya bunge kuvunjwa, imesema hapa kuwa, bunge itakuwa inavunjwa tarehe thelathini mwezi wa November ile mwaka ambayo uchaguzi imefika. Kwa mfano kama huu ni mwaka wa uchaguzi wa National Assembly, ikifika tarehe thelathini November, basi bila ya mtu kusema wanajua tu bunge umekwisha wakati wake.

Halafu bunge mpya itakuwa wakati gani? Imeweka pia katika Katiba mpya, kwa hivyo kutakuwa na calender unaweza kujua, tarehe hii bunge inaondoka, tarehe hii kutakuwa na bunge mpya. Sasa unajua hatujui, hatujui bunge itavunjwa siku gani na ni tarehe gani kutakuwa na bunge mpya kwa sababu hatujui uchaguzi itakuwa siku gani lakini hapa tumeambiwa tarehe thelathini November, ile mwaka ya uchaguzi bunge imevunjwa halafu unaambiwa siku ya jumanne ya kwanza ya mwezi wa February, miaka ijayo, lazima bunge mpya ikae, lazima. Kwa hivyo kuna calender ambayo inajulikana, hapa imeondolewa ile mamlaka ya mtu mmoja tu ndio anajua siku ya kuvunjwa bunge, siku ya uchaguzi na bunge mpya itakuwa siku gani. Sasa imeondolewa hapo imewekwa kwenye Katiba.

Kuna kitu kingine ya kutokuwa na imani na kiongozi, vote of no confidence. Unaambiwa hapa National Assembly inaweza kupitisha na kusema kuwa hatutaki kiongozi kama vile kiongozi wa serikali, Prime Minister. Wanaweza kumuonda through a vote of no confidence. Na wakati huo Prime Minister akiondolewa, basi President atachagua mtu mwingine ambaye atapeleka jina yake kwa bunge wapitisha wachague mtu mwingine mpya.

Nafikiri sasa ninataka kuingia katika sehemu nyingine kama kuna swali yeyote kuhusu mambo ya bunge pengine kuna sehemu zile ambazo nimewacha tunaweza kuziangalia lakini ninaona tuingia katika sehemu nyingine sasa. Kama hakuna swali nafikiri tutaingia katika Executive. Naam ngoja alete hii machine hapo.

Adan Hassan Roble: *Aniga waxa layiratha Ali Hassan Roble, marka waxan sucalaneya ninka xathi bunge caxatho ama Councillor caxatho xathu uu ketiga kufaristo muxu nadexa anigu umba xor iyo dib uu mamuleya, waxan rabna iney xathi layiratho lavatha meloth ama Councillor caxatho ama mjumbe dhath committee oo lashaqeya in naloyelo, shercigi xorey na dhe wava kol xorey an bethelney wavath ogeith, intasan sucal kacava?*

Translator: He says we want those elected Members of Parliament at the grass root level be people who will work with them. Let's say elders who will work with them should also be catered for.

Com. Lethome: Okay, that is a recommendation it has been noted, hiyo tunachukua hiyo, I think that is a recommendations from the constituencies to work together with the representatives. Grassroot representation, ni sawa hiyo. Sasa tuingie kwenye Executive.

Abdi Hussein Hassan: Mimi ninaitwa Abdi Hussein Hassan, sasa tuseme kama bunge ikivunjwa any time, na hii Katiba mpya haikupelekwa mbele ya Conference, wananchi wako na haki ya kusema itumike uchaguzi ujao kwa hii Katiba mpya?

Com. Lethome: Hii swali ingawa haihusiani na hii tunazungumza lakini ni muhimu kwa sababu bunge ikivunjwa kama sasa, hata hii kazi yetu tunafanya kwanza itasimama mpaka bunge ingine iweze kupitisha hii. kwa sababu ile Conference ambayo itapitisha hii lazima iwe na wabunge. Hatuwezi kuwa na wabunge bila ya kuwa na bunge, kwa hivyo bunge ikivunjwa kama leo, hiyo Conference ambayo tunataka ifanywe kuanzia tarehe ishirini na nane mwezi hii haitafanyika, ina maana hii kazi itasimama. Na Rais ako na haki kulingana na hii Katiba ya sasa, ako na haki ya kuvunja sasa kivunja swali lake ni, wananchi je wana haki ya kusema kuwa itumike, uchaguzi ufanywe chini ya hii?

Sasa hawana haki kwa sababu, mpaka hii ipitishwe na Conference halafu ipitishwe na bunge sio sheria ni mapendekezo tu. Na ndio mnaona hata hapa juu hatuwezi kuandika Constitution of Kenya, tunaandika Draft, ni mapendekezo tu. kwa hivyo haiwezi kutumika kwa sababu hii si sheria. Saa hii ukivunja hii ambayo iko hapa hakuna mtu anaweza kukushtaki, hii ni mapendekezo kwa hivyo sasa, we are at the mercy of the President sote, of course, we are at the mercy of Allah (S.W.T.) but as far as this is concerned we are at the mercy of the President, because the old Constitution gives him those powers to do that. And this one is not a Constitution until it goes through the Conference and then through Parliament and without a Parliament no Conference no Parliament of course to approve the draft. Kwa hivyo we shall be suspended until there is a new Parliament.

Tuingie katika Executive, tunajua Executive hapa ni wale ambao wanatawala nchi kabisa, hao ndio wenye mamlaka ya kutekeleza sheria katika nchi. Unaambiwa kwanza kutakuwa na President na Vice President, kwanza tunaambiwa the National Executive kutakuwa na President, Vice President halafu na cabinet, mawaziri. Hebu tuangalie Rais na Vice President wake na mamlaka ya kila mmoja.

Article 150 tunaambiwa President ndio atakuwa head of state, kiongozi wa taifa yeye ndio atakuwa amri mkuu wa majeshi

yote, Commander in Chief of the Armed Forces, na yeye ndio atakuwa Chairman ama Chairperson, tumeweka Chairperson kwa sababu ya nini? Ahmed kwa nini tumeweka Chairperson?

Ahmed Sheikh Hussein: Anaweza kuwa mwanamke.

Com. Lethome: Anaweza kuwa mwanamke President ndio tumesema Chairperson. Unajua wazee ndani ya roho wanasema *maya* lakini ndio hivyo. Tumesema anaweza kuwa mwanamke kwa hivyo Chairperson of the National Security Council and the Chairperson of the Defence Council. Kutakuwa na Council ya Defence, yeye pia ndio atakuwa Chairperson wa hiyo Defence Council baadaye tutaangalia Defence Council ni gani hiyo.

Halafu yeye ndio atakuwa ni ishara ya umoja wa nchi, na yeye itakuwa kazi yake ni kujaribu kuwaunganisha wananchi. Unajua historia ya Kenya ni kuwa yule ambaye uko hapo juu ana angalia kabila gani kwanza, yule ambaye yuko juu kabisa? Wale wamemupigia kura na kabila yake ama sivyo?

Audience: Ndio

Com. Lethome: watu wengine wote wanabaki nyuma na ndio sababu leo hii kila mmoja anapigania ile kiti kwa sababu anajua kabila langu akiingia pale basi tumekula ama sivyo? Sasa tunasema yeye awe ni

Mtu ambaye ataunganisha wananchi wote, sio kupendelea upande mmoja unaona

Awe anahifadhi utukufu wa nchi na heshima ya wananchi wote wa Kenya.

Awe ndio anasimamia haki za kibinaadmu za watu wote.

Lazima aheshimu Katiba na ahakikishe kuwa Katiba inafuatwa.

Na ile mamlaka ambayo tutampatia lazima atumie kulingana na sheria. Asubuhi tulisema no one is above the law. Si mlionyeshwa ile picha President anatembea huko chini na sheria iko juu, inatakiwa hivyo afuate sheria.

Na tunaambiwa President hatashikilia kazi ingine yeyote kama leo President wetu ndio President, na ndio Chairman wa the ruling party. Akiingia tu mtu President, hiyo kiti ya Chairman of ruling party unatoka, unawaachia mtu mwingine kwa sababu utachanganya baina ya kazi ya Raisi na kazi ya party. Lazima iwe tofauti.

Na huwezi kuchaguliwa kiti nyingine yeyote lazima uwe ni President peke yake.

Na unaambiwa kuwa President atakuwa anazungumza bunge, kila wakati bunge ikichaguliwa yeye ndio anazungumzia bunge na atakuwa anazungumzia bunge mpya.

Na kila mwaka at least mara moja kwa uchache sana atakuwa anazungumzia bunge,

Ana haki ya kuzungumzia bunge wakati wowote,

Na anaweza kuvunja bunge kulingana na sheria peke yake. Kuna sheria section 142, ile ambayo inampatia nguvu ya kuvunja mbunge, lazima avunje kulingana na hiyo sheria kwa hivyo lazima turudi kwenye section 142 tuangalie ni wakati gani ambapo anaweza kuvunja bunge.

Ahmed hebu tusomee hiyo sehemu 142 yote, soma moja moja.

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi ninaitwa Ahmed Sheikh Hussein.

1. The term of the National Council is four years,
2. Unless sooner dissolved, the National Assembly shall continue for a term of five years,
3. At any time when Kenya is at war both houses may from time to time by resolution supported by the votes of not less than 65% of all members of each house extend their respective terms for not more than six months at a time,
4. The life of each house of Parliament shall not be extended under clause 3 by more than twelve months,
5. Subject to this Article both houses of Parliament shall stand prorogued on 30th November in every year and the next season shall commence on the 1st Tuesday of February in the next year.

Com. Lethome: Kwa hivyo sasa kulingana na hiyo section 142 Ahmed, did you see anywhere where the President has the right to dissolve Parliament?

Ahmed Sheikh Hussein: Yes.

Com. Lethome: Where, under Section 142, there is nothing at all, hakuna kabisa hana haki, it will only dissolve itself time yake ikiisha au by extension so lazima afuate hiyo sheria. Ina maana kuwa haki ya kuvunja bunge imetolewa kwa Raisi hakuna, hiyo nguvu ya kuvunja bunge hana tena.

Tunaambiwa hapa sasa, nguvu za Rais pia. Atachagua kulingana na Katiba na pia kufuta kulingana na Katiba watu wafuatao, hawa watu ambao tutasoma sasa hapa watachaguliwa na President na yeye ndiye anaweza kuwaondoa lakini kulingana na katiba si kwa mapenzi yake:-

1. Cabinet, yaani mawaziri. Atachagua Prime Minister ambaye yeye ndiye atakuwa ni kiongozi wa ile chama ambaye imepata kura nyingi sana, yeye ndiye atakaye mchagua kuongoza Parliament.
2. Atachagua Deputies wa Prime Ministers wawili,
3. Ministers watakuwa sio zaidi ya kumi na tano, Ahmed umeona hapo hivi, not more than fifteen Ministers ambao watachaguliwa na Prime Minister.
4. Deputies watakuwa not more than fifteen, kwa hivyo kila waziri atakuwa na msaidizi wake mmoja, Deputy sio Assistant, Deputy Minister mmoja, kwa sasa tuna Assistant Ministers wawili, watatu na kwingine unakuja Minister ana ma Assistant karibu watatu wanne, watano. Hakuna kazi wanafanya, kwa hivyo hapa wamewekwa limit, Ministers kumi na watano, Deputies kumi na watano.
5. President ndio atakaye wachaguwa Judicial Officers, kama ma judge lakini tumesema pale mwanzo, lazima hii appointment yote iwe approved na Parliament kwa hivyo hawezi kuwafuta au kuwachagua mpaka ipitie Parliament.
6. Any other public officer who the Constitution requires the President to appoint lakini subject to the Constitution again, lazima iwe kulingana na Katiba.

7. Tulikuwa tunazungumzia hapa asubuhi habari ya Commissions of inquiry. Kwa mfano kumetokezea matatizo fulani mahali, President anachagua Commission ya kuchunguza, sasa laziwe iwe pia ipatikane consent ya Cabinet. Lazima azungumze na mawaziri kabla haja form hiyo Commission ya inquiry ama pia anakwenda nje kuna mikataba ya kimaita, international agreements, Raisi hawezi kukubalia hiyo isipokuwa kwa hiari ya waKenya. Lazima waKenya wakubali kwanza.

Hapana tu-sign instruments of consent by Kenyans to be bound by international agreements. Lazima ashauriyane na bunge kabla kwanza hajaweka sign kwenye mkataba wa kimataifa ambayo itawahusu wa Kenya. Kwa mfano, tuseme kuna mkataba wa kimataifa ambao unasema, mtu yeyote ambaye atapatika na hatia fulani katika nchi nyingine, anaweza kusafirishwa arudishwe katika nchi yake ili afungwe. That is under international law, sasa yeye hawezi kuweka sign kuwa ninakubaliana na hiyo mambo bila kushauriana na cabinet, na cabinet ni mawaziri ambao watakuwa wanawakilisha wakenya.

Kwa hivyo itakuwa ni kuwa ameshauriana kwanza kabla hajaweka sign. Kwa mfano, ile agreement ya Beijing kuhusu haki za wanawake, zingine ambazo tunaona ni kinyume ya mila ya kiafrika au mila zetu kama waKenya. Hawezi kuweka sign mpaka kwanza ashauriyane na cabinet, yaani mawaziri.

Na pia hawezi ku-declare state of emergency bila kushauriana na mawaziri na pia hawezi kutangaza vita, tuseme Kenya sasa itapigana na Somalia ama na Ethiopia bila kwanza kushauriana na cabinet. Kazi yake pia ni kupokea wageni kutoka nje na pia atakuwa akipata ushauri kutoka kwa mahakama kuu. Na pia kama ile kutoa heshima, kuna watu wengine wanapewa medals za heshima hapa Kenya, President ndio anaamua zile tunaziita Presidential awards.

Yeye ndio anatoa kwa mapenzi yake, lakini tunaambiwa chini ya Katiba mpya atakuwa ana shauriana na Prime Minister, waziri mkuu kwa sababu yeye ndio mkuu wa serikali, ni nani anafaa kupewa tuzo kama hiyo, Presidential honours. Kwa sasa ni yeye mwenyewe tu, kama wewe ni mtu wa kumpigia makofi saa zote na nini ama unatingisha sana unapewa ama sivyo? Lakini itaondolewa hiyo yote sasa itakuwa lazima a-consult na Prime Minister.

Halafu tuangalie katika kutengeneza sheria, haki zake ni nini, ama mamlaka yake ni nini? Tumesema ku-approve ku-assent to the bills. Yeye ndiye amepewa mamlaka ya kupitisha sheria, ikitoka kwenye bunge anapitisha, lakini tumesema amepewa masharti fulani Ahmed unakumbuka masharti yenyewe, apitisha kwa muda gani?

Ahmed Sheikh Hussein: apitisha kwa seven days.

Com. Lethome: Yeah seven days, lazima achukuwe hatua pengine apelike kotini akashauriwe au arudishe au apitisha kwa muda wa siku saba. Nafikiri hatuna haja ya kurudia tena kazi ya Presidency hiyo. Nafikiri tuangalie sasa Prime Minister, kuna swali yeyote kuhusu President?

Mohammed Abdow Hashi: Mimi ninaitwa Mohammed Abdow Hashi, sasa ile sheria ya mbele President alikuwa Commander in Chief of the Armed Forces isn't it? Sasa ninauliza kama bado inaendelea ama imekatwa?

Com. Lethome: Tumesema hapa pia bado ni Commander in Chief of the Armed Forces, amepewa bado hiyo mamlaka. Amepewa hiyo mamlaka lakini mkono pia imefungwa kwa sababu ameambiwa hawezi ku-declare emergency mpaka urudi kwa bunge, hauwezi ku-declare vita na ile defence forces si ndio wanaenda kwa vita, hauwezi ku-declare mpaka urudi kwa Cabinet.

Kwa hivyo amepewa ile ni kama symbolic tu, yeye ndio msimamizi ya hii majeshi yote, lakini hawezi kutoa amri mpaka arudi kwa bunge kwanza ndio atoe amri. Umefahamu hiyo sasa?

Audience: Ndio hana uwezo.

Com. Lethome: Hana uwezi juu ya ile lakini amepewa hicho cheo unaona. Hebu tuangalie, haya uliza .

Abdikadir Abdi Farah: Mimi ninaitwa Abdikadir Abdi Farah, swali yangu ni hii. nilikuwa nataka kuuliza wewe, President is he still above the law or what?

Com. Lethome: Nafikiri kwa vile haukuwa asubuhi wacha niwaachie wazee wakujibu hiyo. Tumesemaje wazee kuhusu hiyo, is he above the law, yeye yuko juu ya sheria? Tumesema no, he is below the law, hata I was showing the others here a cartoon ya kuonyesha kuwa sheria iko juu kila mtu yeyote inclung the President yuko chini and that is why you can even take him to court under the new Constitution, if he is in breach of the Constitution.

Hebu tuangalie sasa qualification ya President anatakiwa awe mtu wa aina gani? Hii ni muhimu sana, angalia Article 156 Ahmed. Qualifications for the election as a President. Ni mtu gani ambaye anaweza kuwa President wa Kenya, kwanza

Awe citizen by birth, sio citizen by registration au by naturalization or through marriage, Amezaliwa hapa Kenya, amezaliwa kuwa ni Mkenya ndio huyo anaweza kuwa President wa Kenya.

Awe amefikisha umri wa miaka thelathini na tano na asipitishie umri wa miaka sabini, kwa hivyo kuna wengine ambao wanapigania sasa ambao wamepitisha hiyo, kwa hivyo asiwe ni mdogo sana asiwe ni mkubwa sana. Uhuru amefikisha sasa lakini, yeye ako 42, lakini kuna wengine wamepitisha, wako 74, kama Kibaki chini ya hii sheria mpya anaweza kuwa disqualified.

Awe ni mtu ambaye tabiya yake haina kasoro. Hana matatizo fulani ambayo unaweza kusema kuwa huyu *akhlak* yake ni mbaya,

Awe ni graduate from a recognized university, awe na degree. Kwa hivyo kuna wengi ambao hawawezi ku-qualify, sasa unajua hata mtu ambaye hajaenda shule kabisa bora tu ajue Kiswahili na Kizungu anapita anakuwa President, lakini sasa tumesema lazima awe graduate ndio anaweza kuwa President. Kwa sababu tunataka mtu ambaye anafahmu mambo yanaendelea vipi katika nchi. Akisoma kitu anafahamu, hatutaki kuongozwa na watu ambao hawaelewi.

Awe amekuwa nominated by a registered political party. Anaweza kuwa amependekezwa na chama fulani,

Awe ni mtu ambaye anaweza kuwa ni independent candidate lakini awe amungwa mkono na watu wangapi Ahmed?

Watu elfu moja, kwa hivyo Ahmed wewe kama hapa Dadaab iko watu elfu moja wanakuunga mkono and you want to stand as a presidential candidate kama independent unasimama bora tu uweze kupata ile pesa ya kulipa huko. Lakini wasiwe ni watu wa mkoa moja, upate mia moja kutoka kila mkoa.

Kwa hivyo tuna mikoa mingapi Kenya, 8, kwa hivyo hawa watu elfu moja lazima upate at least mia saba kutoka katika ile mikoa nyingine halafu wao wengine wanaweza kutoka kwenye mkoa yako. Hawa mia mbili ambao wamebaki wanaweza kutoka kwenye mikoa yako, sababu yake ni nini? Kwa nini imewekwa hiyo clause from each Province, when you are a President which Province do you represent? When you are a President of Kenya?

Audience: The whole country.

Com. Lethome: The whole country, so you must have support from all the Provinces. Kwa hivyo ukisimama lazima uwe unaungwa mkono na watu kutoka sehemu zote okay.

A person is not qualified for nomination as a Presidential candidate if the person is under an oath of allegiance to a foreign state. Pale tumekubali kwanza, dual citizenship imekubaliwa katika hii sheria mpya, unaweza kuwa mwananchi wa Uganda na mwananchi wa Kenya.

Halafu hapa tukaongeza tukasema, as a Presidential candidate you must be a citizen of Kenya only kwa sababu by birth, sasa hii ya pili imeondowa mtu ambaye ako na dual citizenship. Kwa mfano kama uko na citizenship ya Uganda na ya Kenya, you are a Kenyan citizen by birth lakini you cannot be a Presidential candidate kwa sababu, you owe allegiance to another country. Uko chini ya sheria ya nchi nyingine, na hatutaki President ambaye anatawaliwa kutoka nchi nyingine. Kwa sababu, when you are holding a Passport of Somalia or Ethiopia or Uganda and you are a Kenyan, you have to obey also Uganda or Ethiopia and we don't want a President who will be obedient to another country. Ndio tukasema asiwe yuko chini ya sheria ya nchi nyingine yeyote.

Asiwe katika ofisi yeyote ya umma, kwa mfano asiwe ni Judge, huwezi kuwa ni judge na wewe ni President wa Kenya, au Magistrate au ofisi nyingine yeyote au katika defence. Kwa mfano, wewe ni Commander wa jeshi halafu unataka kuwa President, haiwezekani ama uwe katika Local Government Authority, haiwezekani. Kwa hivyo kama uko katika hivyo vyeo and you want to vie for the Presidency lazima kwanza u-resign halafu upigania hiyo viti. Kwa sababu tunataka President awe kazi yake ni moja peke yake, iwe ya Presidency na asiangalie mambo mengine. Halafu tunaambiwa pia

Asiwe member of any Constitutional Commission or other Constitutional institutions. Hawezi kuwa yeye ni member kwa mfano wa Land Commission na ni President. Ama ni President na yeye ni member wa Commission kama hii yetu, ama Commission ingine yeyote ambaye imeundwa na Katiba haiwezekani.

Is a Member of Parliament. Kwa mfano huwezi kuwa ni President na wewe ni Mbunge wa Baringo Central, haiwezekani, kwa sababu mbunge katika hii Katiba mpya tumesema lazima ahudumie watu wake ama si hivyo tumesema. Akichelewa sana kuenda kuona watu wake, wako na haki ya kumrudisha. President sasa umempatia

kazi ya nchi nzima na ni lazima umuondolee kazi ya constituency yake. Kwa hivyo hatakuwa MP, he/she sorry nimekosea wakina mama hapo kwa sababu wanaweza kuwa wamama pia, is not a Member of Parliament okay.

Ahmed Sheikh Hussein: Part two authority of the President, Article 150, inasema the president also is the Commander in Chief of the Defence forces,

Com. Lethome: wapi?

Ahmed Sheikh Hussein: 151, na hapa imesemekana kwamba Article 156 2(B) inasemekana hawezi, he could not hold or act in any office in the public service including the judge, magistrate or other judicial officer or an office in which Article 108 applies in the defence forces of the Republic, so ...

Com. Lethome: Unaona kama kuna-contradiction hapo?

Ahmed Sheikh Hussein: Yes.

Com. Lethome: Sasa ukiangalia hapa hivi, ile section ambayo umesoma kwanza 150 imekupatia mamlaka ya Rais, once the President has been appointed, those are his authority, he will be the Commander in Chief of the defence forces okay. Lakini tunaambiwa hapa, under the Article you are reading now, a person is not qualified for nomination as a Presidential candidate, umeangalia hapa, umeona tofauti hapa. Sasa tofauti hapa ni kuwa under section 150 ameshachaguliwa tayari, tumemchagua tunampatia hiyo authority wewe ndio Commander in Chief wa majeshi yetu.

Hii ya pili hapa ni mtu ambaye anataka kupigania hiyo kiti ya Rais, mtu yeyote ambaye ako na ofisi kwa mfano katika mahakama, yeye ni judge ama ni magistrate hawezi kusimama sasa mimi ninataka mnichague. Lakini mtu ambaye ameshachaguliwa tayari, anapewa na Katiba Commander in Chief unafahamu hiyo sasa. Hebu tuangalie anachaguliwa vipi? Section 157 tunataka kuangalia President anachaguliwa namna gani kwa sababu ni muhimu.

Ikiwa kuna mtu mmoja tu ambaye amekuwa nominated, hakuna mpinzani wake amekuwa nominated for that seat, basi mtu kama huyo atakuwa amechaguliwa kama Raisi. Yaani ile tunasema un-opposed, hakuna yule mtu ambaye amemupinga. Halafu ikiwa kuna zaidi ya mmoja kama sasa tuko na wangapi ambao wanataka kuwa Rais, ni wangapi?

Audience: Wengi

Com. Lethome: Hapana sio wengi tunawajua, wanajulikana kuna Uhuru Kenyatta, kuna Nyachae, kuna Raila Odinga, Saitoti, kuna Moody Awori, kuna nani mwingine Charity Ngilu, no Charity hataki Kibaki, na kuna moja ambaye nimesahau Raila Odinga. Kwa hivyo tuna saba. Kwa hivyo tunaambiwa if more than one candidate for the President is nominated, a poll shall be taken in each constituency for the election of the President, kwa hivyo itakuwa kuna kupigiwa kura okay.

Tunaambiwa hapa atapigiwa kura na watu wote ambao wamejiandikisha kama wapiga kura, itakuwa ni secret ballot. Kulingana na vile tumesoma chini ya Article 155, ile siku ambayo itakuwa imepangwa ya kupiga kura. Halafu baada ya zile kura kuhesabiwa na tulisema kura zitahesabiwa mahali gani, asubuhi tulisema kura zitahesabiwa wapi?

Audience: Kwa polling station.

Com. Lethome: Polling station, kama ni hapa, mumepegia haipelekwi Modogashe, hapa hapa inahesabiwa. Halafu inahesabiwa inapelekwa kwa Electoral Commission na Electoral Commission ndio wata declare ile results. Sasa wakati mwingine tunakuta President ukihesabu kura ile amepata nchi nzima haijafika hata 40% ya ile kura yote imepigwa nchi nzima lakini yeye anakuwa ni President. Lakini chini ya Katiba mpya tunataka awe ni a popular President, a President ambaye amechaguliwa na watu wengi, sio kutoka sehemu moja peke yake, lakini sehemu nyingi za Kenya. Hebu tuangalie imekuaje.

Tunaambiwa the candidate for President who receives more than 50% of all the votes cast in the election and who in addition receives a minimum of 20% of the votes cast in more than half of the Provinces, shall be elected as President. Kwanza, apate kura zaidi ya asili mia hamsini, kwa mfano kama kura zote ambazo zimepigwa Kenya ni elfu kumi, anatakiwa apate ngapi? Elfu tano, lakini hiyo elfu tano isitoke sehemu moja lazima kutoka mikoa yote ya Kenya ni ngapi?

Audience: nane

Com. Lethome: Nane pamoja na Nairobi ni nane. Unaambiwa hapa lazima apate 20% ya kura ambazo zimepigwa katika zaidi ya nusu ya hiyo mikoa, nusu yake ni mikoa mingapi? Nne kwa mfano tuseme mimi ni Presidential candidate kutoka North Eastern Province, this is my Province, nimepata kura elfu tano kutoka kura zote za Kenya nzima ukihesabu hizo kura zote. Lazima tuangalie kama nimepata 20% at least kutoka mikoa nne ya Kenya kwa mfano Coast Province, Nairobi Province, Central Province, Rift Valley, au Western Province, yaani mikoa nne nusu ya mikoa yote ya Kenya. Sababu ya kufanya hivi ni kuwa we want a President ambayo ni popular nchi nzima. Kwa sababu leo Ahmed ukisimama sehemu yako hapa unajulikana, ukienda Nairobi iko mtu anakujua, na ukienda kwa wa kalenjin, kabisa hawajui ni nani huyu, wanaona tu ni woria anapita barabarani ama sivyo? So we want a popular President under the new Constitution.

Na jee ikiwa hakuna mtu ambaye amepata hizo 50% votes na 20% kutoka four Provinces, kunafanywa fresh elections, kuna kuwa na run off ya ile mpaka kupatikane yule ambaye atakuwa popular President. Halafu kuna hii shida ya watu kusema kuwa huyu hakuchaguliwa kwa njia nzuri amechaguliwa vibaya, hebu tuangalie Katiba mpya inapendekeza kitu gani Article 158, questions as to validity of Presidential elections.

Unaambiwa hapa katika hii sheria mpya tutakuwa na koti ambaye Supreme Court, the Supreme Court shall determine any question arising as to whether any provision of the Constitution or other law relating to Presidential election has been complied with or whether any person has been elected as President under Article 188. Ukiwa na malalamishi yeyote kuwa huyu President vile amechaguliwa ni kinyume na sheria, uamuzi utafanywa na Supreme Court, hiyo ni mahakama mpya ambao

tutaunda chini ya Katiba hii, hiyo ndio itaangalia.

Ni wakati gani ambapo Raisi anaingia kwenye ofisi anaanza kazi yake Article 159, assumption of office of the President. Tunasema ataingia katika ofisi yake sio wakati amechaguliwa, hapana mpaka kwanza achukue kiapo ya ofisi okay. Na hiyo kiapo yake iko huko nyuma ukiangalia kuna Schedule inaitwa 4th Schedule atakuwa anafanya hivyo mbele ya Chief Justice ama Judge wa Supreme court. Tarehe ya mwisho ya yule President wa zamani ndio itakuwa tarehe ya President mpya kuchukua kiapo ya ofisi ili aweze kuanza kufanya kazi. Na president atachaguliwa kwa muda gani? Kwa sasa tunamchagua kwa muda gani chini ya Katiba?

Audience: 5 years.

Com. Lethome: Five years, renewable once kwa hivyo a maximum of ten years si ndio, maximum of ten years. Chini ya Katiba mpya tunaambiwa the President shall hold office for a term not exceeding five years beginning from the date of assumption of office, kwa hivyo miaka tano kuanzia ile tarehe ambayo amechukua kiapo ya ofisi. Halafu tunaambiwa a person shall not hold office as President for more than two terms of five years each, kwa hivyo miaka kumi peke yake. Ikifika miaka kumi, ndugu yangu patia nafasi wananchi wengine wapigania hiyo kiti, sio miaka ishirini na nne mtu yuko kwenye kiti moja.

Sijui kama kuna swali yeyote kuhusu President kabla sijaingia kwa Vice President na namna ya kumuondoa President? Haya Ahmed ngoja.

Ahmed Sheikh Hussein: Jina langu mimi ninaitwa Ahmed Sheikh Hussein na ninakaa mji wa Dadaab, ninauliza hivi, Rais aki retire kama tuseme Rais Moi anataka ku-retire hapa Katika Constitution mpya, kumewekwa preventive measures na priviledges yake vile ataishi na vile ataangaliwa hali yake katika new Constitution, imeandikwa..

Com. Lethome: Unauliza ama

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi ninauliza because I am not seeing it here.

Com. Lethome: Okay hiyo sasa unajua hivi sasa kuna bill ambayo iko bunge mpaka sasa haijapitishwa, ile ya package ya a retiring President mpaka sasa haijapita. Hiyo itakuwa chini ya an Act of Parliament, haiwezi kukua chini ya Katiba unaona itaangaliwa na sheria nyingine, kwa hivyo, sisi hapa hatujapendekezwa atapewa kitu gani, ma body guard wangapi, mshahara yake pension yake itakuwa ni kiasi gani, itakuwa ni chini ya a retiring President's package ambayo hivi sasa kuna bill ambayo iko bunge sijui kama itapitishwa kabla bunge haijavunjwa ama vipi, hiyo iko uko.

Lakini hapa tuna ile protection ya President wakati yuko ofisini kama hiyo Article ambayo iko hapo 161 inasema. No criminal proceedings may be instituted or continued in any court against the President or a person performing the functions of that office during their tenure of office. Wakati Rais yuko pale kwenye ofisi yeye ni President, basi hauwezi kumshtaki kwa sababu ya criminal offence kwa sababu, tunataka President at least wakati yuko pale ofisini asiwe na wasi wasi ya kufanya kazi yake.

Kwa hivyo, anakua protected hapo hivi, lakini it is subject to clause 2 of this Article. Hebu tuangalia Clause 2 inasema nini?

Inasema, *“No civil proceedings may be instituted in any court against the President or the person performing the functions of that office in respect of anything done, or don in the exercise of their powers under the Constitution during the tenure of office unless such proceedings are wholly of a private nature”*. Hapa tunasema hivi President anapokuwa anafanya kazi yake as a President amekuwa protected against criminal and civil proceedings, lakini ikiwa amefanya hayo makosa in his private capacity as Ahmed not as the President of Kenya, anaweza kuchukuliwa hiyo hatua unaona.

Lakini unakuwa protected if you do it as a President, lakini pia unaambiwa hapa according to the Constitution iwe umefanya hiyo kitu kulingana na sheria. Isiwe ni nje ya sheria, ikiwa ni nje ya sheria utashtakiwa kwa sababu wewe mwenyewe umevunja Katiba, si pale mwanzo tulisema President pia yuko chini ya hii Katiba.

Kwa hivyo, akifanya chini ya Katiba sio ikiwa ametoka nje ya Katiba. Tunaambiwa at least 30 days notice of the proceedings has been served on the President or the person performing the functions of the President then the nature of the proceedings, the cause of action, the name and address of the claimant and the release sort, are specified in the notice.

Kwa hivyo hapa unaambiwa you can bring in action, criminal or civil lakini kuna procedure yake hapo umeambiwa, mpatie notice ya siku thelathini. Although he is the President lakini amevunja sheria, kwa hivyo, unaweza kumshtaki ukifuata hiyo sheria ambayo imewekwa hapo. You cannot say he is above the law, I am answering the question ambayo imeulizwa hapa, he is not above the law lakini kuna protection fulani ambayo amepewa, lakini haina maana kuwa hawezi kushtakiwa. Anaweza kushtakiwa ikiwa tutafuata sheria fulani hapa unaona.

Tunaambiwa under sub-clause 3, Parliament shall enact a law to provide for the operation of clause 2. Kwa hivyo bunge pia inatakiwa itengeze sheria ambayo itasaidia ukitaka kumstaki Rais utafuata utaratibu gani. Na tumesema hiyo sheria ambayo tunataka bunge itengeze, itengeze within what time, asubuhi tuliizungumzia, within? No two years, tulisema within two years lazima Parliament iwe imepitisha haya mambo yote.

Rais anaweza kuondolewa pia, Article 162, inasema pia Rais anaweza kuondolewa kwa mfano ikiwa yeye ana incapacity hawezi kufanya kazi yake, hawezi kukaa pale kama Kamuzu Banda, Kamuzu Banda wakati akiondolewa ilikuwa hata kutembea hawezi anashikiliwa ndio aweze kutembea na ni Rais wa nchi, anashikwa hapa na hapa. Burkeba, alikuwa wa Tunisia, kuna wakati mmoja anashuka kwenye ndege ametembea akaanguka hawezi kutembea na ni President.

Sasa ikiwa hana uwezo ama akili imeharibika imepungua, unajua mtu akizeeka akili inaenda ikipungua sio madharau lakini ni Mwenyezi Mungu ameumba mwanadamu hivyo, inafika wakati fulani akili imepungua, sasa tunasema anaweza kuondolewa kwa sababu ya kutokua na uwezo wa kufanya kazi. Kwa mfano, Article 162, sub article 1 inasema hivi, “ nusu ya National

Assembly, wakipitisha kuwa huyu mzee inaonekana hana uwezo wa kuendesha hii kazi, au akili yake imepungua, basi kutafanyiwa investigations, halafu hiyo investigation ikishafanywa anaweza kuondolewa lakini kuwe na certificate kutoka kwa daktari, kuonyesha kuwa hana uwezo.

Hiyo section ni muhimu sana tuangalie yote inasema hivi, “if it is resolved by one half of the members of the National Assembly, kwa hivyo kupatikane nusu ya bunge, that the question of the physical or mental capacity of the President to discharge the functions of the question ought to be investigated, au wanasema tunataka huyu mtu achunguzwe akili yake tunaona siku hizi, huyu mzee akili imeharibika au hana nguvu ya kufanya hii kazi.

Kwa hivyo tunataka achunguzwe watamjulisha Judge Mkuu, Chief Justice. Halafu Chief Justice kufikia muda wa siku saba, ata appoint tribunal, kutakuwa na tribunal ya watu. Na wao watu hao kutakuwa na watu watano ambao watakuwa ni medical practitioners kama madaktari, kwa sababu leo hii ukiambia watu, Ibrahim inaonekana akili yake si mzuri, wewe ni daktari, daktari ndio anaweza kunichunguza ajue akili yangu si mzuri ama ni mzuri ama Ibrahim ako na maradhi mbaya hawezi kuwa President. Wewe si daktari lazima madaktari wachunguze wajue ni kweli ama si kweli.

Kwa mfano mimi ninagombana kiti ya President na Ahmed, halafu nimemshinda, unafikiri Ahmed hawezi kutumia hii kusema huyu ni wazimu mumechagua, si atatumia hiyo? Lakini lazima ithibitishwe na medical practitioners kuwa ni kweli huyu mtu ana ugonjwa au akili yake si timamu.

Halafu wana report kwa Chief Justice wakihakikisha kuwa ni kweli, inarudishwa bunge tena, ipitishwe na two thirds ya Parliament, wanapiga kura wanasema kweli huyu mtu aondolewe kwa sababu afya yake haimruhusu kuendesha ile kazi ya urais. Kuna mambo ya impeachment of President, kuweza kumuondoa Rais hapo tumesema kwa sababu ya hana uwezo kwa sababu ya afya yake ni mbaya ama akili. Hapa pia kuna impeachment ya kumuondoa Rais.

Kukupatikana kura ya thuluthi mbili, two thirds, pia wanaweza kumuondoa President wakiweza kupitisha motion kama hiyo. Ahmed hebu tusomee hiyo ndio nipumzike kidogo Article 163.

Ahmed Sheikh Hussein: Jina langu ni Ahmed Sheikh Hussein na ninatoka mji wa Dadaab. Impeachment and remove of President, Article 162 Clause 1. “If two thirds of the members of the National Assembly approve a motion for the impeachment of the President for violation of the Constitution or gross misconduct the Speaker of the National Council shall convene a meeting of the National Council to hear charges against the President”.

Com. Lethome: Kwa hivyo kuna taratibu ya kumuondoa Rais, thuluthi mbili ya walioko bunge wakipitisha motion kwa sababu kuwa President huyu amevunja Katiba au amevunja ile sheria tulisema ya uongozi, basi President anaweza kuondolewa kwa sababu hiyo. Hiyo ndio utaratibu na kuna details ya vile ambavyo anaweza kuondolewa. Hapo ni kuonyesha kuwa

akivunja sheria anaweza kuondolewa, hiyo ni kitu ambayo ni muhimu sana tumewekewa katika hii Katiba mpya. Hebu tuangalie ofisi ya Vice President Article 165, kuna swali hapa, huyu ana swali?

Abdikadir Abdi: Mimi ninaitwa Abdikadir Abdi from Dadaab town, nilikuwa nataka kukuuliza kama Chief Justice amekataa kuchagua hiyo tribunal itafanywa namna gani?

Com. Lethome: Sasa bila shaka utaangalia hapo hivi, ni mahali ya kumuondoa kwa sababu ya incapacity ile ambayo tumesoma pale mwanzo, bila shaka ime provide hapo namna ya kufanya, haiwezi kuwa amewachiwa hivi hivi kwa sababu Chief Justice lazima atakuwa ana jukumu chini ya sheria kufanya hiyo kazi, kwa hivyo lazima afanye hiyo kazi.

Ngoja tuangalie, *“if the Chief Justice does not appoint a tribunal within the period specified in clause one, the National Assembly may by a resolution supported by two thirds of all its members authorized the Speaker of the National Assembly to appoint the tribunal.”* Kwa hivyo akikataa inarudishwa kwa bunge yenyewe na ni Speaker atachagua tribunal, kwa hivyo hakuna njia ya kuponyoka hapa.

Turudi katika ofisi of the Vice President, ina shida sana nani anachagua Vice President sasa hapa Kenya?

Audience: President

Com. Lethome: Nani anaondoa yeye?

Audience: President.

Com. Lethome: Who is our Vice President today in Kenya?

Audience: Saitoti

Com. Lethome: Nani anasema Saitoti we have no Vice President. We have no Vice President kwa sababu amechaguliwa na Rais anaondolewa na Rais, hapa tunasema atakuwa running mate wa President, unajua kama America vile wanafanya ama nchi zingine, wakati mnachagua President mnachagua na running mate wake as the Vice President sio yeye ndio anamchagua no, anachaguliwa na wananchi wenyewe, anapigania kiti ya Vice President, kwa hivyo hawezi kuondolewa, aondolewe na wananchi wenyewe.

Kwa hivyo Vice President amekuwa protected under this new Constitution, hapo mwanzo alikuwa ni kibaraka tu, hawezi kuzungumza, akizungumza anaondolewa kama vile ambavyo mumeona nyinyi wenyewe.

Ahmed Sheikh Hussein: Are they from the same party?

Com. Lethome: Of course they have to be from the same party, unajua kama wewe ndio President kwa mfano, you are the Presidential candidate, hauwezi kuchagua running mate from a party that is opposing you, he has to be from...

Tuanguilie mshahara ya Rais na ya Vice President, 169, mishahara yao kama vile wabunge, tumesema itawekwa na Salaries and Remuneration Commission. Si wao wenyewe ndio watakua wanajichagulia, yeah. Itakuwa imewekwa na hiyo Salaries and Remuneration Commission ambayo pia inaweka mshahara ya wabunge. Sio wao wenyewe wanajiwekea, halafu kunakuwa na pension baada ya yeye kutoka na gratuity na other retirement benefit ambayo zitaamuliwa na Salaries and Remuneration Commission.

Mnaambiwa pia mshahara yake na allowance yake ambayo inapewa President ama Vice President na ambayo atapewa baada ya ku-retire pia, itatoka kwa Consolidated fund. Katika ofisi ya Prime Minister, hii ndio mpya sasa hakuna Kenya, tumependekeza kuwe na ofisi ya Prime Minister, yeye ndio atakuwa anaongoza Cabinet, kwa sasa who is the head of Cabinet? Ni President mwenyewe unaona, sasa hapa tutakuwa na Prime Minister na hawa ndio watakuwa wanaendesha serikali.

Tunaambiwa hapa, “the Prime Minister and the other members of the cabinet exercise executive authority within the Republic by developing and implementing national budgets and policy, preparing and initiating government legislation for introduction in Parliament yes, kuna mtu ameliza kitu? Ni Article 170, hiyo ya Prime Minister. “Performing any other executive function provided for by the Constitution or an Act of Parliament except those functions assigned to the President”. Kwa hivyo kuendesha serikali, mkuu wa serikali ambaye atakuwa anaongoza cabinet, ambaye atakuwa analeta policy za serikali, itakuwa ni Prime Minister na cabinet.

Atachaguliwa na nani? President tumesikia anachaguliwa direct na wananchi, na Prime Minister je? Tunaambiwa, “*within seven days following the summoning of the National Assembly or whenever necessary to fill a vacancy in the office of the Prime Minister, the President shall propose to the Speaker of the National Assembly the appointment as a Prime Minister of the leader of the party with the majority members in Parliament*”, ndio watachaguliwa, au anaweza kuwa leader wa coalition of parties, vyama fulani kama vile NARC, NARC is not one party, it is a coalition of parties. Kiongozi wao pia anaweza kuchaguliwa kama Prime Minister.

Na pia tunaambiwa anaweza kuwa leader of a minority party, kwa hivyo tumeambiwa leader of a majority party lakini pia under clause B, tumeambiwa, *leader of the minority political party or coalition of parties represented in the National Assembly if the leader of the majority party or coalition has been unable to command or retain the confidence of the National Assembly.*” Kwa hivyo inawezekana pia mtu ambaye ni kiongozi wa minority party akue Prime Minister pia, ikiwa yule ambaye anaongoza ile chama kubwa ameshindwa kupata confidence ya wale wengine katika National Assembly.

Kwa hivyo mtu wa party ndogo anaweza kukusanya wengine na akaweza kukua yeye ndiye Prime Minister. Na ikiwa hakuna mtu ambaye ni kiongozi wa majority party au wa minority party C inatuambia, “*if neither party contemplated in paragraph A or B has been able to command or retain the confidence of National Assembly, then any other member of the National*

Assembly who in the President's opinion may be able to command or retain the confidence of the National Assembly."

Kwa hivyo anaweza kuna mtu mwingine yeyote katika bunge, anaweza kuwa hata ni yule independent candidate. Ikiwa wabunge wengine wote wako na confidence na yeye, anaweza kuwa Prime Minister.

Term of office of the Prime Minister, akichaguliwa kama Prime Minister na akiwa confirmed by the National Assembly basi ataendelea kufanya hiyo kazi, hebu soma hapa Article 172 Ahmed.

Ahmed Sheikh Hussein: Jina langu ni Ahmed Sheikh Hussein kutoka Dadaab. Term of office of the Prime Minister, Article 172 clause 1. *" A person whose appointment as a Prime Minister has been confirmed by the National Assembly assumes the office of Prime Minister by swearing or affirming faithfulness to the people and the Republic of Kenya and obedience to the Constitution in accordance with the fourth schedule before the Speaker and members of Parliament."*

Kwa hivyo akichaguliwa lazima ataendelea kushikilia ile ofisi na kwanza atachukua kiapo, na tunaambiwa hapa Prime Minister atakaa kwenye ofisi yake mpaka afe au bunge ifike mwisho wake, na tulisema National Assembly muda wake ni siku ngapi, ni mwaka ngapi? Five years, so you will stay there for five years unless maybe he resigns under Article 173, ama pengine amekuwa dismissed under Article 174, he can be dismissed also by a vote of no confidence. Ikiwa imepitishwa na more than 50% of the Members of Parliament, wanaweza kumtoa pia. So nobody is safe from being removed, Prime Minister anaweza kuondolewa kama vile President anaweza kuondolewa .

Cabinet, hapa pia ni mpya tumependekeza mpya. Leo hii Cabinet Ministers ni watu gani? Wanachaguliwa kuwa Cabinet Ministers?

Ahmed Sheikh Hussein: The President appoints them.

Com. Lethome: Okay the President appoints them from where are they appointed?

Ahmed Sheikh Hussein: From Parliament.

Com. Lethome: From Parliament, but they are from Parliament. All of them are MPs either elected or nominated, hauwezi kuwa Minister kama wewe hauko bunge si ndio? Sasa hapa kuna mabadiliko kidogo na ndio unasikia watu wengine wanalalamika hapo, nyinyi mtaangalia ni nzuri ama si nzuri. Tumesema hapa, *"the President shall appoint the remaining members of the cabinet in accordance,* kwa nini tunasema the remaining members? Kwa sababu ashamchagua mmoja, the Prime Minister, sasa the remaining fifteen, mnaambiwa hapa, *"the remaining members in accordance with the recommendations of the Prime Minister and with the approval of the majority of the members of the National Assembly.* Hiyo kazi bado tunamwachia President lakini lazima iwe na approval ya Prime Minister na National Assembly.

Mnaambiwa hapa, *" the President shall not appoint a Member of Parliament to the office of Minister or Deputy Minister.* Kwa hivyo MP wote, ukiwa MP forget about Minister, unajua siku hizi, wakati watu wanapigiwa kura wanasema

mkinichagua, nitakuja hapa na benderea, mara hii hakuna mambo ya kuambia watu bendera, bendera ile ya Minister itapatiwa watu ambao si MP sasa. Ndio mapendekezo ambayo tumepata hapa, na kuna sababu yake, kwanza, malalamishi ambayo tumepata kwa wananchi wengine ni kuwa MP mumemchagua, amechaguliwa Ministers, wakati umechaguliwa Minister unatakiwa uhudumie watu gani, as a Minister?

Ahmed Sheikh Hussein: The whole country.

Com. Lethome: The whole country not your people, lakini leo hii wewe ukiwa ni MP wa Lagdera umechaguliwa kuwa Minister unaambia watu wenu unaona nimeleta benderea Lagdera. Umepeleka bendera ya Kenya nzima, na unawaambia watu wa Lagdera hiyo ni yao, instead of using your ministerial authority or powers to serve the whole country, you are using that to serve your people, what will happen to the others ambao hawana Ministers.

Halafu pia tatizo ingine ni kuwa, unakuta mtu yeye ni retired Chief of the General Staff, halafu anachaguliwa kuwa Minister of Health, si mumeshasikia kitu kama hiyo imetokea? Minister of Health, mtu ambaye hata Kiingereza cannot speak, amekuwa Minister of Health. Atazungumza na madaktari lugha gani. PS wake kwanza is a qualified doctor ama Professor in medicine, halafu yeye ndio Minister wake anaenda kuzungumza kitu gani? Ama mtu is a businessman, I don't want to say from where, amewekwa yeye ndio Minister of Medical Services, ama mtu ambaye hajasomea kabisa mambo ya Agriculture ametoka North Horr, anaambiwa wewe ndio Minister of Agriculture.

Kwa hivyo tunasema sasa we want technocrats, watu ambao umesomea kazi fulani, you will be the Minister in an area relevant to your profession. Kwa nini hatuchagui Attorney General mtu ambaye hajasoma sheria, hivo hivo ambao tunachagua Attorney General mtu amesoma sheria tunataka pia kama ni Minister of Agriculture ako na degree katika Agriculture, kama ni finance awe ni mtu amefanya economics. Lakini sio uchukue tu mtu ambaye hajasomea hiyo kazi unampatia hiyo kazi. Ndio tunasema hapa to avoid hiyo imbalance kuwa MPs of certain areas wanakuwa Ministers, kwa hivyo tunasema Ministers will be appointed from outside Parliament, hawatachaguliwa from Members of Parliament.

Mzee: Kuna watu wachache tu wanasikia Kiingereza, wengi hawasikii Kiingereza, ongea Kiswahili.

Com. Lethome: Pole mzee, tunasema hivi waziri hatachaguliwa kutoka kwa wabunge, waziri anachaguliwa kutoka nje, kwa sababu wakati mwingine tunaona waziri akichaguliwa, manufaa yote anapeleka watu wake, kwa hivyo tunataka sasa waziri awe ni mtu ambaye yuko nje ya bunge. Na pia tunataka waziri ambaye amesomea kazi ya wizara yake kwa mfano kama ni waziri wa afya, awe amesomea mambo ya Afya, kama ni waziri wa Livestock awe ni mtu amesomea kazi ya mifugo anajua, kama ni waziri wa fedha, Finance awe amesomea mambo ya fedha ndio uchumu uweze kuendelea vizuri.

Halafu tunaambiwa kwamba, *“the President shall not appoint a Member of Parliament to the office of Minister or Deputy Minister.”* Hiyo tumemaliza. Ya pili, *“ the President shall not appoint a person other than a Member of Parliament to the office of the Deputy Prime Minister.”* Kwa hivyo Prime Minister na Deputy watakuwa ni Members of

Parliament lakini the other fifteen Ministers watakuwa ni outsiders, watakuwa ni watu wa nje.

Kwa hivyo Ahmed hata usipochaguliwa mbunge, unaweza kupigania na uchaguliwe kuwa Minister ikiwa umesomea kazi fulani.

Kama ni mambo ya Livestock unajua mambo ya ngamia, ngombe na nini unaweza kuchaguliwa pia.

Article 178 conduct of Members of the Cabinet. Wao watu wakichaguliwa kuwa Ministers wanatakiwa wawe watu wa aina gani, kwanza, ningetaka kuangalia qualification ya.. Hapa tunaambiwa member of cabinet yaani waziri yeyote, atajiepusha na hali yeyote ambayo italeta mgongano baina ya maslaha yake ya kibinafsi na kazi yake kama waziri. Asiingize mambo yake ya uwaziri katika kazi yake ya kibinafsi kwa sababu itatokea mgongano, lazima ajiepushe na mambo kama hayo.

Halafu pia asifanye kazi ama asiwe na mwenendo ambayo haikubaliani na ofisi yake akama waziri, unasikia mara nyingi unasema yule ni waziri kweli na anafanya mambo kama hii. Waziri hafai kufanya mambo kama hii, tumesikia mara nyingine waziri ama Assistant Minister ameshikwa akijaribu kutafutia watu fake Passports, wasafiri nje. Haifai mtu ambaye anashikilia ofisi kama hiyo kujihusisha na mambo kama hayo, au waziri pengine amepatikana na vitu vya magendo ni kama kuwa ametumia ile mamlaka yake kufanya mambo kama hayo unaona.

Na ameambiwa pia, asitumie ile mamlaka yake ya ofisi ili kujitajirisha, siku hizi Kenya unaambiwa ukiwa wewe ni waziri halafu hauna mali, watu wanasema huyu mjinga huyu, alikuwa waziri na hakuna kitu, si ndio watu wanasema hivyo? Inafahamika Kenya ukipatiwa hiyo bendera lazima ukule ama sivyo, sasa unaambiwa usitumie hiyo ifisi ili kujitajirisha nafsi yako. Halafu kuna sheria ile ambayo lazima wafuate na ile tulisema pia ya uongozi lazima wafuate.

Hebu tuingie katika judiciary sasa, mambo ya mahakama, mengine mtajisomea baadaye kwa sababu sasa ni karibu saa kumi na moja na bado tuko mbali sana. Mambo ya Judiciary, angalia Article 185, koti zitakuwa namna gani? Hierarchy of courts, kutakuwa na makoti na judges na magistrates na watu wengine wanafanya kazi katika hiyo idara ya Mahamaka kulingana na sheria ambayo imewekwa hapa hivi.

Kwanza juu kabisa kutakuwa na Supreme Court, halafu kutakuwa na Court of Appeal, halafu chini yake kutakuwa na High Court, hizo tunaziita Superior Courts of records. Hizo ndio koti zile kubwa, kwanza kabisa, Supreme Court, Court of Appeal halafu High court, halafu tunakuwa na koti zingine za chini ambazo tunaziita Subordinate courts. Hizo zitakuwa Magistrates and Kadhis' courts. Halafu chini yake Ahmed hebu soma hapo.

Ahmed Sheikh Hussein: Jina langu ni Ahmed Sheikh kutoka Dadaab. The Superior courts of record are the Supreme Court, the Court of Appeal and the High Court. The Subordinate courts are:

- a. The magistrates courts and the Kadhis' courts,
- b. Any other court established by an Act of Parliament subordinate to the High Court and

- c. Any traditional or local tribunals with limited jurisdiction in issues of local significance that may be established by an Act of Parliament.

Com. Lethome: Kwa hivyo hizo ndio koti ambazo tutakuwa nazo, Supreme Court, Court of Appeal, High Court halafu chini yake kuko na Magistrates' Court na Kadhis' Court. Halafu zaidi ya hapo kutakuwa na koti zingine kama vile za kimila kama vile mliniambia hapa asubuhi, wasomali katika mila yao, kuko na koti ya wazee ama sivyo?

Audience: kweli.

Com. Lethome: Lakini lazima iwe inatambuliwa na sheria ama nyingine yeyote ambaye Parliament wanaweza kupitisha sheria ya kutengeneza koti kama hiyo. Halafu tunataka judiciary ambayo iko na uhuru, mnafahamu uhuru wa judiciary, yaani wasiwe wanapendelea upande wowote kama sasa kwa mfano, watu wengi wanalalamika wanasema koti inamapendeleo, koti haina independence, haina uhuru kwa sababu pengine wanaogopa akitoa hukmu ambaye haimridhishi mtu fulani ambaye ni mkubwa, anaweza kufutwa kazi.

Kwa hivyo, chini ya sheria mpya, tunataka mahakama ambaye ni uhuru ambaye haitaogopa mtu yeyote itafanya kazi ya uadilifu. Tuangalie Supreme Court, nani atakuwa kwenye Supreme Court. Supreme Court ndani yake kutakuwa na Chief Justice ambaye atakuwa ni mkuu wa mahakama zote, halafu tutakuwa na majaji wengine ambao sio zaidi ya sita, hao ndio watakaa katika Supreme Court.

Kazi ya Supreme Court ni nini? Wanaweza kusikiza kesi zingine bila ya kutoka kwenye mahakama zingine, ndio tunaita original jurisdiction. Kesi inakuja direct to the Supreme Court, kwa mfano kama kesi za election petition, itakwenda direct to the Supreme Court. Halafu wanaweza kuwa pia wanamu-advice President, kama pale kuna wakati mmoja tulisema kuwa President atataka advice ya Supreme Court, Ahmed unakumbuka ni sehemu gani? Sehemu ambayo ameletewa bill na anatakiwa aweke sign yake, seven days anaweza kupeleka kwa Supreme court kupata opinion yake.

Kwa hivyo, it will be an a legal advisor to the President. Halafu watasikiza Presidential election petitions na watasikiza pia mambo yeyote ambayo inahusiana na kumtoa Rais katika bunge. Kama hizi impeachment of the President watasikiza wao kitu yeyote ambayo ni Constitutional kwa mfano mtu ana-challenge jambo fulani katika Constitution itakuwa inasikizwa na Supreme Court. Matatizo baina ya wilaya mbili, kwa mfano Garissa na Wajir, wako na dispute baina yao. Basi mas'ala kama hayo itasikizwa na Supreme Court. Au pia B hapa itakuwa na Appellate jurisdiction, yaani Appeal inatoka kwa koti nyingine inaletwa juu, kulingana na sheria ambayo itakuweko.

Kwa ufupi hii ndio itakayo kuwa koti kuu katika Kenya halafu chini yake tuna the Court of Appeal, Court of Appeal itakuwa na mtu tunamwita President, kwa sasa hakuna President katika Court of Appeal lakini tutakuwa na President of Court of Appeal na ma judge wengine ambao hawajazidi kumi.

Halafu wakati inakaa lazima kuwe na ma judge watatu, tumeambiwa wote ni wangapi? Kumi na President wake, lakini wakati wanakaa wanasikiza kesi wanakuwa wangapi? Watatu, there has to be three judges. Hapa Court of Appeal iko chini ya Supreme Court, kwa hivyo uamuzi wa Supreme Court, lazima Court of Appeal isikize. Halafu tunaambiwa hapa, High Court na koti zingine zote ambazo ziko chini lazima zisikize amri au hukumu ambayo imetolewa na Court of Appeal kwa sababu ziko chini yake hapo hivi.

Halafu tunaambiwa President wa koti hii ya Appeal, akizungumza au kushauriana na Chief Justice anaweza kutengeneza ama kubuni sehemu au idara fulani za Court of Appeal. Kulingana na vile anavyotaka, kwa mfano anataka Court of Appeal wakae ma judge watatu wasikize kesi fulani, yeye ndio anaweza kusema nyinyi nendeni mkasikize hiyo kesi mahali fulani.

Hebu tuangalie uwezo wa Court of Appeal, Ahmed tusomee tena nataka kupumzika kidogo.

Ahmed Sheikh Hussein: 191 Clause 1, “the Court of Appeal is an appellate court with jurisdiction in:

- (a) Appeals from a decree judgement or an order of a High Court and
- (b) In any other appellate jurisdiction conferred on it by any other law.

- 2. An appeal to the court of Appeal lies as of a right from a judgment, decree or order of the High Court.

Com. Lethome: Sasa hizo ndio kazi za Court of Appeal, kama vile jina lake linasema Court of Appeal, hawana original jurisdiction, wanaambiwa ni Appeals kutoka kwa High Court inakwenda kwa Court of Appeal au kesi nyingine yeyote ambayo wataambiwa na sheria yeyote wanaweka kuangalia na tunaambiwa hapa, appeal yeyote ambaye inatoka kwa High Court ni haki lazima iende directly kwa Court of Appeal, yaani kutoka kwa High Court appeal inaenda kwa Court of Appeal.

Sasa tutaenda katika sehemu muhimu, kuchaguliwa kwa majaji. Majaji wanachaguliwa namna gani kwa sababu hii ndio muhimu sana, hizo zingine zilikuwako tangu zama lakini kuchaguliwa ma judge ndio muhimu sana. A decree is an order of a court or a judgment, we call it a decree also.

Haya tuingie appointment of judges, wanachaguliwa vipi? Ahmed utusaidie kidogo. Ngoja Halima aje hapo kidogo.

Ahmed Sheikh Hussein: Appointment of judges’ clause 194. When there is a vacancy in the office of the Chief Justice, the most senior judge of the Supreme Court by reference to the date of appointment shall be appointed by the Chief Justice.

Com. Lethome: Ngoja hapo kidogo, kumetokea nafasi ya Chief Justice, atachaguliwa yule ambayo ni very senior katika koti gani? Supreme Court, kinyume na vile ambayo imetokea hivi sasa alipokufa Chesoni, who was appointed as the Chief Justice, was it the senior most judge? Ni yule ambaye yuko juu sana judge? Hata hakuwa judge, amechaguliwa Bernard Chunga

ambaye alikuwa ni Prosecutor, ndio amechaguliwa kuwa Chief Justice kwa sababu Katiba ilikuwa haijasema nani anachaguliwa Chief Justice akishaondoka . Sasa tunasema anachaguliwa the most senior judge of the Supreme Court ndio anachaguliwa haya endelea.

Ahmed Sheikh Hussein: Clause 2 is the appointment of judges. When there is a vacancy in the office of the President of the Court of Appeal, the most senior judge of the Court of Appeal, by reference to the date of appointment shall be the President of the Court of Appeal.

Com. Lethome: Endelea.

Ahmed Sheikh Hussein: Clause 3, when there is a vacancy in the office of the Principal Judge of the High Court, the most senior judge of the High Court by reference to the date of appointment shall be the Principal Judge.

Clause 4, the other judges of the Superior Courts of record and the Chief Kadhi shall be appointed by the President acting in accordance with the advice of the Judicial Service Commission and with the approval of the National Council.

Com. Lethome: Sasa utaratibu umewekwa hiyo ambayo haiwezi kuingiliwa na mtu mmoja. Kwanza tumeambiwa Chief Justice ameondoka, you go to the highest courts in the country, the Supreme Court, you choose the most senior judge to take over as the Chief Justice sawa hiyo.

The President of Court of Appeal, ikiwa hayuko, you go to that same court and choose the senior most judge in that court. Halafu unaambiwa kama ni Principal Judge from the High Court anachaguliwa judge mwingine kutoka from the same court, kwa sababu how do you expect a junior person hata kama wewe mahali unafanya kazi, mtu ambaye yuko huko chini kabisa sasa yeye ndio yuko juu yako utamsikiza? Hata yeye mwenyewe hawezi kufanya kazi vizuri, kwa hivyo sasa kumewekwa hiyo utaratibu anachaguliwa mtu ambaye ni senior. Halafu ma Judge wengine wote na Chief Kadhi, wao wanachaguliwa hapa na Judicial Service Commission, yaani President atakuwa anawachagua hawa lakini in accordance with the advice, atakuwa ana shauriwa na Judicial Service Commission. Tutaangalia Judicial Service Commission ni wakina nani wako ndani yake kwa sababu tunaona ndani yake kuna watu wa kutoka sehemu mbali mbali ili kuhakikisha kuna independence katika ile kuchaguwana.

Tuangualie ni nani ambaye anawezakuwa judge, kwanza awe ni mtu ambaye ana experience ya miaka kumi na tano kama judge katika Court of Appeal, hauwezi kuingia katika Supreme Court kama judge mpaka uwe umefanya kazi katika Court of Appeal ama High Court kwa miaka kumi na tano. Yaani uwe umefanya kazi kwa muda huo wote, au wewe uwe ni wakili umefanya kazi miaka kumi na tano as an Advocate au wewe ni mwalimu wa kusomesha sheria katika University ambayo inatambulika kwa miaka ngapi tena?

Audience: Kumi na tano.

Com. Lethome: Kumi na tano. Kwa hivyo wakili ambaye amefanya kazi miaka kumi na tano, judge wa High Court wa miaka kumi na tano au mwalimu wa sheria wa miaka kumi na tano. Halafu pia tunaambiwa hapa lazima uwe na intellectual ability, lazima uwe pia ni mtu ambaye unaonyesha kuwa una ujuzi wa hiyo kazi yako, wiku mtu ambaye hana ujuzi na mwisho kabisa mtu mwenye *akhlak* tabia nzuri. Sio mnachagua judge ama sehemu zingine unakwenda kotini unakuta magistrate ni mlevi, ataweza kusikia kweli? Ama ukimuangalia tu hivi huyu pengine hakulala usiku mzima halafu anakuja kusikiza kesi au mtu ambaye maisha yake haiendi sawa sawa, atakuja kotini ama atafikiria habari ya maisha yake huko nje. Kwa hivyo, anatakiwa mtu ambaye mwenendo yake ni sawa kabisa.

Hebu tuangalie judge anaweza kutolewa namna gani akishachaguliwa. Article 197 unaambiwa, judge akiwa katika Supreme Court ama Court of Appeal ama High Court ambazo tumeziita Superior Courts of Records, tunasema anaweza kuondolewa namna hii, ya kwanza, ikiwa hawezi kufanya kazi yake, pengine mwili wake amezeeka sana au hana nguvu ni mgonjwa au akili pia, basi mtu kama huyo anafaa aondolewe kwa sababu kazi ya kuhukumu watu pengine utahukumu mtu kwenda kufungwa maisha ana watoto wake umewachia watoto wake shida lazima tupate mtu wa sawa sawa mwenye akili timamu aweze kufanya kazi kama hiyo. Unacheza na maisha ya watu, ile ni maisha ya watu, haki za watu kama sasa vile ambavyo mpaka sasa kuna hukumu ya kunyongwa hata maisha ya binadamu iko mikononi yako.

Sasa lazima uwe ni mtu ambaye akili yako ni timamu na afya yako pia ni timamu kwa sababu unatakiwa usikize vizuri kama hausikizi vizuri pengine watu wanazungumza na hausikii utahukumu namna gani. Lazima uweze kusikia na kufahamu, haki iko wapi ili uweze kuhumu. Au amevunja sheria ya uwongozi, ile code of conduct au awe hawezi kufanya kazi yake vizuri basi mtu kama huyo anaweza kuondolewa katika hiyo kazi yake.

Tuingie katika Kadhis' courts, hiyo nafikiri ni muhimu sana kwa Waislamu, lazima Waislamu wasikie hiyo Kadhis' court ama sivyo mnataka kusikia vile iko? Article 199, Ahmed hebu tusomee hiyo.

Ahmed Shiekh Hussein: The Kadhi's court, Article 199 clause 1.

- *“They are established Kadhi's court the office of Chief Kadhi, office of the Senior Kadhi and the office of Kadhi.*
- *Clauue 2, There shall be a number being not less than thirty of other Kadhis as may be prescribed by the Act of Parliament.*
- *Clause 3, a Kadhi is empowered to hold a Kadhi's court called a District Kadhi's court having a jurisdiction within a District or Districts as maybe prescribed by or under an Act of Parliament.*

Com. Lethome: Haya sasa ile Constitution ya sasa sijui iko wapi nilikuwa nataka kulinganisha Katiba ya sasa na ya zamani. Zamani kuna section moja tu ya Katiba, Section 66 ambayo inazungumza habari ya Kadhis' court, na hiyo Kadhis' courts vile

ilivyoundwa katika hiyo sehemu kwanza ukianza kama wewe ni Kadhi utakufa kama wewe ni Kadhi, hakuna daraja ama madaraka yeyote unapanda.

Sasa katika hii Katiba mpya, tumependekeza kuwe na daraja tatu ya ma Kadhi. Juu kabisa kuna Chief Kadhi, chini yake kuna Senior Kadhi halafu chini kabisa tuko na Kadhi. Kwa hivyo kumekuwa na daraja tatu na ni muhimu kujua hizo daraja tatu kwa nini zimewekwa. Okay?

Halafu tumeambiwa katika nchi yote ya Kenya kutakuwa na ma Kadhi ambao hawatapungua thelathini unajua sasa tuko na wangapi? Tuko na ma Kadhi kumi na saba, kuna sehemu zingine kwa mfano, hapa Dadaab mkitaka kwenda kwa koti ya Kadhi mnaenda wapi?

Audience: Garissa.

Com. Lethome: Mpaka Garissa au mwingine aende mpaka Wajir ama sehemu zingine. Utakuta kuwa ma Kadhi ni wachache sana, sasa tumesema lazima wawe zaidi ya thelathini Kenya nzima kwa hivyo tumeongezewa nafasi ya ma Kadhi. Halafu pia kutakuwa na Kadhi ambaye tunamwita Kadhi peke yake yeye atakuwa na ofisi yake katika District, kwa mfano, kama ni Kadhi wa Garissa, yeye ataitwa District Kadhi wa Garissa.

Baada yake tutakuwa na Senior Kadhi ofisi yake itakuwa ni Provincial halafu Chief Kadhi yeye ndio atakuwa ni mkubwa wa ma Kadhi wote. Sababu ya kuweka hizo nafasi tatu ni kuwa, sasa tuko na nafasi moja tu ya Kadhi, ukienda kwa Kadhi halafu amehukumu yeye ni binadamu ama si binadamu? Anaweza kukosea, ikiwa haujaridhika na hukumu yake unaenda wapi?

Audience: Hakuna.

Com. Lethome: Iko una High Court

Audience: Mbeleni hakukua

Com. Lethome: Iko, unaenda High Court sasa. Unaambiwa enda High Court lakini High Court ukienda hakuna sheria ya Kiislamu unaambiwa sheria ya Kiislamu kando sasa, na yule anayekaa pale si Muislamu, hajui sheria ya Kiislamu. Ndio tumesema sasa Appeal ikitoka kwa District Kadhi, inaenda kwa Senior Kadhi at the Province, ikitoka kwa Senior Kadhi inaenda kwa Chief Kadhi. Kwa hivyo tutakuwa na appeal system ya Kadhi, na ukiangalia hapa jurisdiction of the Kadhis' court, hebu angalia Ahmed hiyo, pitia. Kazi yao itakuwa ni nini? Angalia kazi ya Kadhis' court.

Ahmed Sheikh Hussein: Jurisdiction of a Kadhis' courts Article 1 clause 200. The jurisdiction of Kadhis' court extends to;

- a. The determination of question of Muslim law relating to personal status, marriage, divorce, including matters arising after divorce and inheritance and succession in proceedings in which all the parties profess Islam.
- b. The determination of civil and commercial disputes between parties who are Muslims in a manner of a small claims

court as by law established but without prejudice to the rights of parties to go to other courts or tribunals with similar jurisdiction.

c. The settlement of disputes over or arising out of administration of work properties.

Com. Lethome: Kwa hivyo hiyo ndio kazi ambayo hii sheria imepatia Kadhis' courts kuangalia ile mas'ala ambayo inaangalia mpaka sasa, mambo ya nikah, talak na uridhi na mambo mengine ambayo inahusiana na mambo ya kifamili katika sheria ya Kiislamu. Na pia mahali ambapo wote wawili ni Waislamu au ikiwa kuna mambo ingine ya watu wanadaiyana pesa au pengine kuna agreements baina ya Waislamu, hii tumeongezewa ilikuwa hakuna. Wanaweza pia kwenda kwa Kadhi, kuenda kuamua mambo kama hayo, kwa mfano Sheikh anaidai pesa na mimi ninakataa na sote wawili ni Waislamu, tunaweza kuenda kwa Kadhi atuhukumu kulingana na sheria ya Kiislamu. Hiyo si ni nzuri pia, tumeongezewa hiyo.

Halafu kuna hile mali ambayo inaitwa *Waqf*, unajua kuna baadhi ya watu matajiri zamani hapa Kenya walinunua mali nyingi wakasema hii ni *waqf* fi Sabilillah, isaidie Waislamu. Sasa inasimamiwa na watu wengine ambao si Waislamu, mali nyingi iko Coast Province, imesemekana sasa mambo yote ambayo inahusiana na hiyo *waqf* Commission ikiwa kuna matatizo yeyote, inaletwa kwa Kadhi.

Mambo ya appeal kutoka kwa Kadhi nafikiri tumezungumza vile itakuwa na utaratibu gani kutoka chini mpaka juu. Kitu ingine ambayo tumeongezewa ukiangalia the next page Sub-Article 6, kutakuwa na sheria ambayo itasaidia ma Kadhi wanapofanya kazi katika mahakama ya Kadhi, watafuata sheria gani? Zile rules of procedures, zitatengenezwa na Chief Justice, the Chief Kadhi and the Law Society of Kenya, watatengeneza rules ambazo zitasaidia ma Kadhi katika koti zao. Sasa vile iko, unakwenda kwa Kadhi, unataka kuhukumiwa kulingana na sheria ya Kiislamu lakini procedure ile anafuata, anafuata sheria ambayo si ya Kiislamu kwa sababu hakuna. Sasa hapa sheria hii imesema lazima Chief Kadhi na Chief Justice na Law Society watengeneza rules of Procedures ambazo zitafuata na ma Kadhi huko.

Ma Kadhi watachaguliwa namna gani? Tunasema Kadhi hawezi kuchaguliwa mpaka awe Muislamu, tunaweza kuchaguliwa Kadhi ambaye si Muislamu, lazima awe ni Muislamu na awe si mtoto mdogo sana. Awe na miaka thelathini na tano au zaidi, ama anaweza kuwa ni wakili wa koti ya Kenya ambayo amefanya kazi miaka kumi na ana degree kutoka katika University ya Kiislamu na anajua sheria za Kiislamu ambazo zinatumiwa katika mahakama ya ma Kadhi. Kama si advocate wa High Court kama vile tumesema hapa ambaye ana ujuzi wa mika kumi, awe ni mtu ambaye amepata degree ya sheria ya Kiislamu kutoka katika Chuo kikuu ambacho kinatambulika. Na pia ana miaka zaidi ya kumi ama isiwe chini ya kumi katika kufanya kazi ya sheria ya Kiislamu au amekuwa katika ofisi ya Kadhi.

Unajua sasa vile wanachaguliwa hata mtu anamaliza tu Madrassah, mtu yeyote ana maliza Madrassah anaweza kuchaguliwa kuwa Kadhi ama sivyo, tumeona wengi. Anatolewa Madrassah Kisauni Mombasa anawekwa ana kuwa Kadhi. Haangaliwi kama anajua sheria ya Kiislamu ama hajui sheria ya Kiislamu ama anaweza kufanya kazi ya Kadhi, hakuna mtu anaangalia siku

hizi anaweka tu mtu yeyote.

Nafikiri tuangalie hapa sasa kuhusu Judicial Service Commission ni Commission ile ambayo itakuwa inasimamia uchaguzi wa majaji. Tumeambiwa watakuwa wanachaguliwa na President halafu wanakuwa approved by the Judicial Service Commission. Hebu tuangalie ni nani yuko katika Judicial Service Commission.

Tumeambiwa kutakuwa na Chairperson ambaye atakuwa ni judge wa Supreme Court ambaye atakuwa amechaguliwa na President na pia atakuwa approved by the National Council. Kutakuwa na mwanamke Muislamu ambaye atakuwa anawakilisha jamii ya Kiislamu na atakuwa amechaguliwa na chama ya Kiislamu kukaa pale kwa sababu ya kusikiliza maslaha ya wanawake wa Kiislamu.

Attorney General atakuwa hapo, kutakuwa na judge mmoja kutoka kwa Supreme Court, kutakuwa na judge mmoja kutoka kwa Court of Appeal na kutakuwa na judge mmoja kutoka kwa High Court. Halafu kutakuwa na Chief Kadhi ndani yake kutakuwa na Magistrate wawili na kutakuwa na Advocates wawili ambao wamefanya kazi zaidi ya miaka kumi na mitano, watakuwa wamechaguliwa na ile chama ya mawakili, Law Society of Kenya. Kutakuwa na walimu wawili wa sheria na mmoja wao lazima awe ni mwanamke halafu kutakuwa na mtu mmoja ambaye atakuwa amechaguliwa na barala la elimu ya kisheria.

Kisha Chairman wa Public Service Commission pia atakuwako na kutakuwa na watu watatu wengine ambao si mawakili au hawahusiani na sheria. Kwa hivyo ndio itakuwa Judicial Service Commission na kazi yake ni kuchagua watu wale watafanya kazi katika idara ya mahakama. Hizo details zingine nafikiri mtasoma nyinyi wenyewe, lakini hapo mtaona kuwa sisi kama Waislamu tumepata sehemu kubwa sana hapo, mambo mengi ambao tulikuwa hatuna, tumepata hapo ama sivyo? Ile Chief Kadhi na Kadhi wameongezewa nguvu zaidi ambao walikuwa hawana.

Halafu tunaambiwa hapa mishahara ya watu wale wote ambao wanafanya kazi katika Judiciary itatoka kwa Consolidated fund. Hebu tuingie hapa Article 210, Public Defender. Tunaambiwa kutakuwa na ofisi moja hapa ambao tutaita ofisi ya Public Defender, mlinzi wa watu, mlinzi wa raia, ngao ya raia, hii ndio itakuwa inalinda raia. Huyu atachaguliwa na President na atakuwa ameshauriana na Judicial Service Commission na itakuwa imepitishwa na bunge, kwa hivyo atakuwa amechaguliwa na vyombo vitatu, President, Judicial Service Commission na atakuwa approved na National Council. Na atakuwa ni mtu ambaye anaweza kuwa judge wa High Court.

Hebu tuangalie kazi zake. Number nne ukiangalia Sub-Article 4 tunaambiwa kazi yake, shall be to provide legal advice and representation to persons who are un-able to afford legal services. Unajua leo hii ukienda kotini, kuna mtu tajiri ambaye anaweza kwenda kulipa wakili akamuakilishe, na maskini je utafanya nini? Na wewe Sheikh ukienda kupambana na wakili kotini hutoweza, kwa sababu wanatumia ile lugha ya sheria ambayo wewe haujui, sasa mlinzi wa watu Public Defender atakuwa anasaidia wale watu ambao hawawezi kujisaidia kotini, kwa hivyo, utakuwa na haki ya kwenda kusaidiwa na mtu kama huyo.

Okay?

Sijui kama kuna swali lolote hapo kwa sababu ninataka kuingia katika devolution of power ambao ni muhimu sana mjue, mamlaka imeletwe karibu na wananchi sasa, imeletwe mpaka level gani, kwa hivyo kama kuna swali yeyote kuhusu judiciary nataka tumalizie na hiyo devolution of power. Hiyo ni kitu mpya pia.

Haya kama hakuna nitaingia katika devolution of power na hii ndio itakuwa ya mwisho ambayo nitazungumzia na ingine Inshallah Saad utafanya bidii uwalettee Draft waweze kujisomea wenyewe kwa sababu muko na karibu mwezi mzima wa kuweza kusoma na kupendekeza yale ambayo mnataka kupendekeza.

Kwanza devolution of power maana yake kwa Kiswahili ni ile mamlaka kusambazwa badala ya mamlaka kuwa mahali moja, kuitawanya, kuigawanya, ndio tunasema devolution of power. Leo hii ukiangalia ni nani ambaye yuko na powers zote, powers zote ziko wapi, kwa President ziko kwenye ofisi moja. Kwa hivyo, utakuta watu wanatawaliwa kutoka huko juu sana, mamlaka iko mbali sana na watu, kwa hivyo devolution imelete mamlaka karibu na watu na kujaribu kuwahusisha watu.

Kwa hivyo tumeambiwa hapa devolution itakuwa hivi angalia Article 214 unaambiwa subject to the Constitution the structure of devolved authority is based on the democratic principles and the separation of power. Itakuwa hapa tunaangalia msingi ya democracia na pia kutawanya mamlaka, separation of powers ni kama vile President powers zake ni kando, isiingilie powers bunge, isiingilie powers za judiciary, hiyo ndio tunaita separation of power, kugawanya mamlaka.

Na pia itakuwa ni legislative or policy making or supervisory Councils and executive authorities are elected. Kutakuwa pia kuna majukumu ya kuunda sheria na ma jukumu ya kusimamia idara ya serikali ama mamlaka ya serikali vile itakavyochaguliwa. Halafu tunaambiwa executive authorities are accountable to elected Councils. Kutakuwa na ma baraza ambayo itakuwa imechaguliwa na watu na yule ambaye ako na mamlaka ya kusimamia idara ya serikali basi atakuwa na *mas' ulia* mbele ya hizi ma baraza ambazo zitakuwa zimechaguliwa na watu. Na hawa watakuwa ni watu ambao watakuwa wamechaguliwa na wananchi wenyewe, hizi Councils zitakuwa ni Councils ambazo zimechaguliwa wenyewe.

Lakini wacha tuangalie levels of government, serikali mamlaka yake itakuwa katika level ngapi? Ukiangalia Article 215 Ahmed ukitusomea hapo, tutaangalia mamlaka imeteremshwa mpaka sehemu gani?

Ahmed Sheikh Hussein: Levels of government Article 215, clause 1. Powers are devolved to the following levels:

- (a) Village,
- (b) Location,
- (c) District and

(d) Province.

Com. Lethome: Kwa hivyo mamlaka tumeambiwa imeteremshwa sasa kwa village, kijiji, kwa mfano hii village yenu inaitwa?

Audience: Dadaab.

Com. Lethome: Hapana kuna jina ingine ya kijiji hapa, mahali Chief anasimamia hiyo village, hiyo ni location, village yote inaitwa Dadaab. Kwa hivyo katika village kutakuwa na level ya serikali, kutakuwa na serikali ya village, kutakuwa na serikali ya location ile ambayo inasimamiwa na Chief hivi sasa, kutakuwa na serikali ya District na serikali ingine ya Province.

Village government tunaambiwa hapa, kutakuwa na kitu inaitwa Village Council ambayo itasimamia idara au mamlaka katika ile village. Kwa hivyo kutakuwa na Village Council hapo, na tunaambiwa the village decides on the system of village government including the role of the Village Council. Watu wa kijiji wanaamua wanataka kutawaliwa namna gani na wanataka mamlaka ya hiyo Village Council iwe namna gani. Hiyo ndio level ya chini kabisa ya serikali, halafu tunapanda juu kidogo, tukitoka kwa Village government tuna locational government okay, kutakuwa na Location Council ambayo itakuwa na wawakilishi wawili, mmoja atakuwa ni mwanamke ambao watakuwa wamechaguliwa na Village Council kutoka katika kwa mfano tuseme hii ni Location moja, hii Location inaitwaje?

Audience: Dadaab,

Com. Lethome: Na village ni Dadaab pia?

Ahmed Sheikh Hassan: Dadaab ni division halafu kuna Dadaab Location.

Com. Lethome: Haya kwa mfano village ya Dadaab inapeleka watu wawili kwenye location iyo kubwa, itapeleka watu wawili, mtu mmoja mwanamke na mmoja mwanaume kwenda kuwawakilisha katika Location. Unajua katika sehemu zingine za Kenya unakuta chini ya location moja, kuna village kama tano, kwa hivyo kama kuna village tano kila village itatoa watu wawili waende kwenye location Council. Na hiyo location Council sasa itakuwa na watu wangapi? Kumi hao ndio watakuwa wanaangalia maslaha ya location.

Kwa hivyo wawakilishi wakijiji wanakwenda kwenye location, wanawakilisha kijiji yao kwenye location. Hiyo mumefahamu? Tukitoka hapo tunaingia katika District sasa. Tunaambiwa hapa the legislative authority of the District is vested in the District Council. Kutakuwa na District Council ambayo itakuwa ni kama bunge ya ile District yote.

Hebu tuangalie wale watakaa katika District Council ni watu gani?

- Watakuwa ni members directly elected by the registered voters of the District,
- the District Council shall consist of not less than twenty or more than thirty members. Kutakuwa na watu ambao sio chini ya ishirini au sio zaidi ya thelathini ambao watakuwa wamechaguliwa na watu katika ile District, maana yake

tukipitisha hii Katiba mpya kutakuwa na uchaguzi pia, sio ile ya County Council peke yake, kutakuwa na pia ya District Council.

- Halafu tunaambiwa kutakuwa na mkuu wa District hataitwa DC, sasa mkubwa wa District si ni DC, yuko Garissa. Tutakuwa na District Administrator yeye ndio atakuwa anafanya kazi ya kusimamia District ndio ninawaambia pengine tukipitisha hii, itakuwa mambo ya DO, DC, PC hakuna tena.
- Halafu tunaambiwa the District Administrator is elected directly by the registered voters of the District. DC sasa nani ndio anamchagua? DC ndio anasimamia District ama sivyo? Nani amechagua yeye? Sasa huyu DC yuko Garissa mumechagua nyinyi?

Audience: Moi.

Com. Lethome: Amechaguliwa na President, he is an appointee of the President lakini chini ya Katiba mpya ni wananchi wenyewe ndio watachagua. Hakuna DO kwanza mumesikia DO, hakuna, katika Location ndio tumeweka Locational Council, hakuna DO hapo, hakuna division kwa sababu DO anasimamia division. Tunaingia katika District, hakuna DC, tuna District Administrator elected by the people themselves, anachaguliwa na wananchi wenyewe.

Halafu tunaambiwa the District Administrator with the approval of the District Council appoints Chief officers from persons who are not members of the District Council. Atachagua wale ambao watasaidiana naye kazi. Halafu vile amechaguliwa na wananchi pia anaweza kuondolewa, huyu District Administrator, leo hii munaweza kuondoa DC?

Audience: hapana.

Com. Lethome: Hamwezi kumuondoa hamjamchagua na hamwezi kumuondoa. Tunatoka sasa kwa District, tunaingia kwa Province.

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi ni Ahmed Sheikh Hussein, swali langu ni hii kutoka Dadaab. Ninauliza ma Chief ninaona bado hapo katika establishment ya levels of government ya Katiba mpya ninaona ma Chief wamelemewa kidogo hawako ndani hapo, sasa hawa Katiba mpya wamewekwa katika position gani?

Com. Lethome: Tunasema hapa ukiangalia chini ya location, si Chief anasimamia location?

Audience: Ndio.

Com. Lethome: Tumesema kutakuwa na Location Administrator, na Location Administration ngoja nisome usikie mambo yao, shall be elected by the registered voters of the location. Wanachaguliwa pia kwa hivyo Chief anachaguliwa kutoka Office of the President imekwisha, Sheikh wewe ni Chief?

Mzee: hapana.

Com. Lethome: Sasa kama unataka kuwa kiongozi wa Location utapigiwa kura na wananchi kwa sababu ya kuweka hii. Wakati mwingine unakuta mtu amewekwa na serikali pengine watu hawampendi ama sivyo? Lakini wananchi wenyewe wakipatiwa nafasi ya kuchagua, watachagua mtu yule ambaye wanampenda wao wenyewe, na wakishindwa wakiona hafanyi kazi wanaondoa. Kwa hivyo, Chief hatutamwita Chief, ataitwa Location Administrator na atakuwa anapigiwa kura.

Haya tumesema District Administrator pia anapigiwa kura, hebu tuingie kwa Province tuone PC naye mambo yake imekuaje? Tunaambiwa hapa, mamlaka ya kusimamia Province itakuwa kwenye Provincial Council, kwa hivyo kutakuwa na baraza ingine ambayo inaitwa Provincial Council ya kusimamia mkoa, halafu tunaambiwa itakuwa na wawakilishi wawili kutoka kila District Council, si tumesema kwa mfano katika Garissa District kuna District Council. Watu wa Garissa watachagua watu wawili, watu wa District ingine kama Wajir, Mandera, Ijara watachagua watu wawili pia hawa watu wawili watapelekwa kwenye Provincial Council na mnapochagua mmoja anakua mama na mwingine anakua mzee. Hao ndio watawakilisha District yenu kwenye Province.

Halafu tuangalie nani mkubwa wa Province, tunaambiwa kutakuwa na Provincial Administrator ndio atakuwa anasimamia. Atachaguliwa namna gani? Atakuwa appointed by the Provincial Council, ile Council ambayo mumepeleka watu wawili wawili kutoka kila District, kwa mfano tuseme ni North Eastern Province, iko na District ngapi?

Audience: Tatu.

Com. Lethome: Nne Sheikh umesahau Ijara, iko Ijara, Garissa, Wajir na Mandera. Wameleta watu wawili wawili, wamekuwa wangapi katika ile Provincial Council?

Audience: nane.

Com. Lethome: Watu nane. Hawa watu nane watachagua mmoja wao atakuwa ndio Provincial Administrator, sasa Province inasimamiwa na nani sasa hivi? PC amechaguliwa na nani? Na President, hiyo imeondolewa sasa anachaguliwa na wananchi wenyewe sasa. Sasa hapo mtasoma muangalie District Council iko na powers gani, Provincial Council iko na powers gani halafu nitaangalia mambo ya urban government. Kwa mfano, hii ni Garissa District kwa mfano leo petroli ikipatikana hapa ni ya watu wa Garissa ama ni ya Kenya nzima? Ama bahari ile Indian Ocean, tuko na Port pale Kilindini harbour, ni ya watu wa Coast peke yao ama ni ya Kenya nzima?

Audience: Kenya nzima.

Com. Lethome: Sasa hapa Katiba lazima ieleze hizi resources ambazo tunasema ni national resources zitatumika namna gani. Kama kuna resource hapa Garissa itumike sehemu ingine, ifaidi watu wengine na isifaidi watu wa hapa? Na pia haingii akilini itumike hapa peke yake na watu wengine wasifaidike, lazima kuwe na balance, wale watu ambao wanaishi sehemu hiyo wapate faida na watu wengine wa Kenya waweze kupata faida.

Ndio tunaambiwa hapa share of national resources, tutaweza kugawanyaje hizi national resources. Article 126 tunaambiwa hapa, *“Districts shall be entitled to a substantial share of the national revenue from local resources and for the allocation of a sixth percentage to the communities in whose areas the resources are generated.”* Tunaambiwa hapa si tumesema kuna District Council, kwa mfano Garissa ikiwa kutapatikana National resource yeyote hapa pengine mbuga za wanyama au misitu au kitu kingine chochote, ile percentage kubwa inatakiwa itumiwe hapa. Lazima kuwe na percentage fulani ambayo itatumika hapa na ingine ambayo itatumika katika sehemu nyingine ya nchi.

Tumeenda sehemu zingine za Kenya, kwa mfano wa Turkana, kuna ile inaitwa Turkwel Gorge Dam ambayo ina generate power, area hiyo yote ya Turkana wanaishi wanaona tu sijui ni wa Pokot ama ni wa Marakwet Hassan? Ni watu gani wako karibu ni Turkwel Gorge, Pokot. Wanasema wao maisha yao hawajaona stima wanaona wire tu zikipita juu yao, imetokaa kwao lakini hawatumi. Hiyo ni haki kweli, a resource, okay it is a national resource imetoka kwao lakini hao hawaonji hata kidogo. Kwa hivyo tunasema kuwe na percentage fulani ambayo itatumiwa na watu wa pale na iwafaidi watu wa pale halafu ile ingine ndio itapelekwa katika sehemu zingine za nchi.

Kwa mfano North Eastern kukipatikana petroli leo hii kwa sababu watu wengi wanasema, ukitaka kujua mahali iko petroli, ni mahali iko desert na iko Waislamu, hapo inawezekana sana kuwa petroli. North Eastern ni desert karibu na desert na iko Waislamu, kwa hivyo pengine kuna petroli ndani yake.

Ikipatikana percentage fulani itakuwa ni ya sehemu hiyo na ifaidi communities wale wako sehemu hiyo halafu percentage ingine itapelekwa katika sehemu zingine. The revenue from national resources shall be shared equitably between the Districts and the national government. Kwa sababu tutakuwa na serikali ya District na serikali ya taifa, basi tunaambiwa kuwa revenue income ile itapatikana pale, kwa mfano, ikiwa hapa kuna mbuga za wanyama, watu wanakuja kuangalia Herola, Herola si iko hapa? Wale watalii wanakuja kuangalia hapa wanalipa ama hawalipi? Ile revenue ambayo wanalipa basi unaambiwa wagawanye kwa usawa baina ya serikali ya District ile na serikali ile ya kitaifa.

Mombasa revenue from the Port ni kubwa sana, ile income inapatikana kutoka Kilindini harbour ni kubwa sana, sasa isiwe ile yote inakuja Nairobi hapana, ingine ibaki kule isaidie watu wa pale na iweze ku-develop ile area na nyingine iletwe katika national. Hiyo si mnaona ni nzuri? Kwa hivyo fanyeni bidii mambo ya Livestock pia is a national resource, revenue from that inatakiwa faida kubwa isaidie watu wa sehemu hii na faida ingine iende katika sehemu nyingine ya serikali.

The manner of distribution of revenue shall be set out in an Act of Parliament, bunge itapitisha sheria ya kuonyesha hii mali ambayo inapatikana kutoka kwa hizi resources itagawanywa namna gani baina ya serikali kuu na serikali ya wilaya. Nafikiri sasa nitakomea hapo, ulizeni maswali kidogo halafu tuachie hapo sasa.

Ahmed Sheikh Hussein: Mimi ni Ahmed Sheikh Hussein kutoka Dadaab. Tuseme sasa hii ni Katiba ambayo ni Draft,

haijakuwa ni sheria. Mwaka tuseme wa January, next government ambaye ita-form pengine ipitishie hii ama serikali ya saa hii ipitishie iwe sheria, sisi wananchi wa Dadaab au wa Lagdera constituency kuna revenue ma millions nyingi sana ambaye zetu zimeenda Treasury direct na haijafanyiwa chochote katika constituency ya Lagdera ama tuseme District ya Garissa. Sasa tunaweza ku-complain damages, compensation kutoka kwa serikali irudishe some percentage from revenue yetu tuweze ku-develop area yetu, when this draft becomes a Constitution?

Com. Lethome: Ukiangalia hapa tumezungumzia habari ya Commission ambazo zitaundwa na hii Katiba, sasa itakuwa ni kazi ya hizo Commissions kuangalia ni mambo gani ambayo inatakiwa iangaliwe ili kuleta uadilifu. Kama pale asubuhi nimesema kuna baadhi ya watu ambao wamedhulumiwa sana wamenyanyaswa haki zao, sasa ni juu ya hizo Commission kama vile Commissions ya human right, ile ya integrity ile ya justice, kuangalia ni haki gani ambayo inafaa watu kurudishiwa. Kuna sehemu ambazo zimekuwa under-developed miaka hii yote thelathini na tisa, ni juu ya Commission kama hizo na bunge pia kuangalia ni mambo gani ambayo inatakiwa ipitishie katika sheria ili kuhakikisha watu wamefanyiwa uadilifu, ile haki yao ambao wamedhulumiwa wamerudishiwa. Sasa hiyo unajua haiwezi kuwa chini ya Katiba hapa, lakini hizi Commissions ambazo zimetengezwa na Katiba hii ndizo zinafaa kuangalia mambo kama hiyo Inshaallah.

Nafikiri tutakomea hapo tumechoka na nyinyi mumechoka pia lakini fanye bidii muko na mwezi nzima msilale someni. Halafu comments zenu mnaweza kutuma direct Nairobi au kupitia kwa District Co-ordinator wenu Saadi ili ifike huko kwenye National Conference kama bunge haijavunjwa, ama delegates wenu. Mnajua muko na delegates wangapi? Iko? Na pia kuna delegate mwingine,

Hassan S. Mohammed: Ndio kuna watatu lakini mmoja anatoka constituency ingine.

Com. Lethome: Kuna mwingine pia.

Hassan S. Mohammed: Wale wengine wawili, ni Ibrahim anafanya kazi Ports and Abdullahi Haji .

Com. Lethome: Kuna mwingine pia, anaitwa Mohammed Shidiye. Honourable Mohammed Shidiye is a delegate in the Conference. Yes, not the immediate MP the current MP, all the MPs are delegates to the National Conference and that is why we are saying if Parliament is dissolved today, we can't hold the National Conference because we shall not have 222 delegates and without them we cannot have the Conference.

Haya shukran Jazakum Llahu Kheiran Inshallah Mwenyezi Mungu atujalie ili iweze kumalizika, hebu tupate Sheikh mmoja tupate dua yake halafu tumalize, Sheikh dua.

Sheikh Jibril Othowa: *Bismillahi Rahmani Rahim, Allhamdullilahi Rabil Alamin Arahmani Rahim Maliki yaumi dini iyaka naabudu wa iyaka na stahin ihdina siratal mustaqim, siratal lathina an amta aleihim khairil maqthubi alaihim wala thualin - Rabana atina fi dunya hasana wa fil akhirati hasanatan wa kina adhaba nar, wasala lahu ala sayidina Mohammad wa ala alihi wasalim taslim. AMIN.*

